Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

# BUNGE LA TANZANIA

## MKUTANO WA PILI

### Kikao cha Pili – Tarehe 9 Februari, 2011

*(Kikao Kilianza Saa Tatu Asubuhi)*

### D U A

*Spika (Mhe. Anne S. Makinda) Alisoma Dua*

**HATI ILIYOWASILISHWA MEZANI:**

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI (MHE. PEREIRA AMME SILIMA):**

Taarifa ya Mwaka *ya Insurance Market Performance Report* kwa mwaka ulioishia tarehe 31 Desemba, 2009 *(The Annual Report of Insurance Market Performance Report for the year ended 31ST Desember, 2009).*

### MASWALI NA MAJIBU

Na. 14

**Kuiwezesha *TACAIDS* Kutoa Huduma Bora**

**MHE. DIANA M. CHILOLO** aliuliza:-

Serikali inategemea kupata fedha za kusaidia shughuli za mapambano dhidi ya UKIMWI kwa takriban 90% kutoka kwa wahisani:-

Je, Serikali itaanza kutenga fedha kupitia vyanzo vyake vya ndani ili mapambano dhidi ya UKIMWI yawe endelevu hata pale wahisani wanapositisha misaada yao?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, URATIBU NA BUNGE** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Diana Mkumbo Chilolo, Mbunge wa Viti Maalum na Kamishina wa Tume ya Taifa ya Kudhibiti UKIMWI kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, janga la UKIMWI ni janga kubwa na kwa nchi zinazoendelea kama ilivyo Tanzania zinapata msaada kutoka katika mataifa na taasisi za nje ya nchi kwa sababu nyingi ya nchi zinazoendelea hazina uwezo mkubwa kiuchumi wa kupambana na janga hili peke yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ni jukumu la mataifa yote duniani hasa mataifa tajiri kusaidia nchi zinazoendelea katika kukabiliana na majanga mbalimbali likiwemo hili janga la UKIMWI ambalo limekuwa likipoteza nguvu kazi yetu. Kutokana na ukweli huo, ndio sababu kwa sehemu kubwa tumeendelea kutegemea nchi wahisani. Hata hivyo, kuanzia mwaka 2001, Serikali imekuwa ikitoa kwa *TACAIDS* shilingi kati ya bilioni 15 na bilioni 18 kila mwaka ambazo zimekuwa zikisaidiana na fedha za wahisani kukabiliana na tatizo hili.

Mheshimiwa Spika, Serikali inayo mikakati ya muda mfupi, kati na muda mrefu inayolenga kupunguza utegemezi wa michango ya wahisani na pia kuongeza mchango wa nchi yetu kukabiliana na tatizo hili.

Miongoni mwa mikakati hiyo ni kuongeza elimu kwa umma kuhusu kujikinga na UKIMWI kwani watu wakijilinda na kuepuka maambukizi mapya hakutakuwa na haja ya kutenga fedha za kudhibiti UKIMWI na pia Serikali kuongeza mchango wake kutoka kwenye Bajeti na kubuni njia nyingine za kuongeza Bajeti ya UKIMWI kama vile kuanzisha Mfuko wa UKIMWI *(AIDS Trust Fund)* ambalo ndilo kusudio tunalotaka kulifanya katika mwaka wa fedha ujao.

**MHE. DIANA M. CHILOLO:** Mheshimiwa Spika, asante. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri, napenda kuuliza maswali madogo mawili ya nyongeza.

Swali la kwanza, kwa kuwa fedha za wahisani zinaendelea kupungua kwa kiasi kikubwa; na kwa kuwa Serikali imeainisha mikakati mizuri sana ya kupambana na UKIMWI; je, Serikali itakuwa tayari sasa kuongeza fedha kutenga katika Mfuko huu wa UKIMWI kuanzia Bajeti hii ya mwaka 2011 ili kuonyesha jitihada za kupambana na huu ugonjwa wa UKIMWI?

Mheshimiwa Spika, swali la pili, kwa kuwa Halmashauri zetu huwa zinateua Mkuu wa Idara moja kusimamia ama kuratibu masuala ya UKIMWI katika Halmashauri zetu; na kwa kuwa Halmashauri hizi zinategemea fedha za wahisani.

Je, Serikali iko tayari sasa kuziagiza Halmashauri zote nchi nzima kuanza kutenga sasa fedha katika Mfuko huu wa UKIMWI ikiwa ni njia mojawapo ya kujihami ama

kuweka tahadhari wakati wahisani watakapoacha kutenga fedha kwa ajili ya kutusaidia? Asante!

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, URATIBU NA BUNGE:** Mheshimiwa Spika, ni kweli kama nilivyokiri kwamba sehemu kubwa ya fedha hizi zimekuwa zinatoka kwa wahisani, lakini kwa uwezo wetu na sisi tumekuwa tunafanya hivyo, tunatenga fedha kati ya shilingi bilioni 15 na 18 na ndiyo maana tumeamua kuanzisha Mfuko Maalum wa UKIMWI ambao kwa kiasi kikubwa utachangiwa na vyanzo mbalimbali vya ndani. Nia ni hiyo hiyo ya Mheshimiwa Diana Chilolo kwamba tunataka kwa kadri inavyowezekana Serikali ya Tanzania ichangie zaidi shughuli hii kuliko ambavyo wahisani peke yao wanashiriki. Tungependa angalau ifikie asilimia 40, lakini hili na mkakati huu utaanza rasmi katika Bajeti ya mwaka 2011/2012. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, la pili, ushauri wa Mheshimiwa Diana Chilolo ni mzuri. Kama Serikali tumeupokea, lakini si rahisi kuuanzisha ghafla kwa sababu tunajua vyanzo vya Halmashauri vya mapato vinajulikana. Lakini ukumbuke kwamba hata hizi fedha tunazozipata kwa wahisani huwa zinaenda huko huko Halmashauri, maana siyo kwamba *TACAIDS* pale haya mabilioni yote mia ngapi na hizi za Serikali zinaishia hapo.

Mheshimiwa Spika, fedha zote zinazopatikana kutoka kwa wahisani na za Serikali zinazoingia *TACAIDS* huwa tunazipeleka kuimarisha uwezo wa mapambano dhidi ya UKIMWI kupitia Halmashauri zetu. Lakini ni wazo zuri kwamba Halmashauri zetu zianze kufikiria jambo hili. Kwa hiyo, wazo hili tumelipokea. *(Makofi)*

Na. 15

### Ujenzi wa Sekondari za Kata

**MHE. DAVID E. SILINDE** aliuliza:-

Wakati Serikali ikiendelea na ujenzi wa shule za sekondari za Kata kwa kushirikiana na wananchi yapo majengo mengine ambayo hayajakamilika:-

(a) Je, Serikali inachukua hatua gani kwa majengo ambayo hayajakamilika?

(b) Kwa nini Serikali isisitishe mara moja utaratibu wa kupangia wananchi kiwango cha michango ya ujenzi wa sekondari hizo badala yake wananchi waone wenyewe kiwango wanachoweza kuchangia kulingana na vipato vyao?

(c) Je, Serikali inaonaje kuanza kujenga mabweni ya wasichana kwenye sekondari za Kata ili kupunguza ongezeko la wanafunzi wa kike kupata mimba wakiwa shuleni?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. AGGREY D. J. MWANRI)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri Mkuu, naomba kujibu swali la Mheshimiwa David Silinde, Mbunge wa Mbozi Magharibi, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kwamba yapo majengo ya shule ambayo hayajakamilika. Serikali kupitia Mpango wa Maendeleo ya Elimu ya Sekondari Awamu ya Pili imeandaa miongozo inayolenga kuboresha miundombinu ya shule ikiwemo ujenzi wa madarasa, nyumba za walimu, maabara na hosteli kwa kuzingatia miongozo iliyopo.

Serikali inasisitiza ukamilishaji wa majengo ambayo bado hayajakamilika kabla ya kuanza ujenzi wa majengo mapya ya shule. Aidha, ni jukumu la wananchi, Halmashauri na Serikali Kuu kuhakikisha kwamba miundombinu ya shule ambayo haijakamilika inakamilishwa katika kipindi cha utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo ya Elimu ya Sekondari Awamu ya Pili *(MMES II).*

(b) Mheshimikwa Spika, moja ya majukumu ya Kamati za Maendeleo ya Kata ni kuhamasisha wananchi kuchangia ujenzi wa miundombinu ya shule. Viwango vya michango vinavyohitajika katika shule huamuliwa kupitia vikao vya Kamati za Maendeleo za Kata na hatimaye katika vijiji. Kwa maelezo hayo, ni dhahiri kwamba Serikali haina utaratibu wa kuwapangia wananchi viwango vya michango ambavyo wanatakiwa kuchangia kuhusu maendeleo ya shule katika maeneo yao. Hata hivyo, napenda kutumia nafasi hii kusisitiza kwamba Bodi za Shule na Mamlaka nyingine ziweke viwango vya michango vinavyozingatia sheria, kanuni na taratibu na hali ya kipato cha wananchi.

(c) Mheshimiwa Spika, kuhusu suala la kujenga hosteli, Serikali katika Bajeti yake ya mwaka 2009/2010 imezitengea Halmashauri 28 fedha za ujenzi wa hosteli kiasi cha shilingi bilioni 7.55 kwa kuzingatia umuhimu wa kuwepo kwa hosteli katika mazingira husika. Fedha hizo ni za ruzuku za maendeleo kutoka Serikalini. Hivyo, napenda kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge kuwa suala la ujenzi wa hosteli za wasichana katika shule za sekondari ni kipaumbele cha Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba ieleweke kwamba ujenzi wa hosteli ni sehemu tu ya ufumbuzi wa tatizo la mimba kwa wanafunzi. Suala hili linahitaji juhudi za pamoja katika jamii. Ni vyema turudi katika maadili mema ya kulea watoto wetu hasa tukizingatia

kwamba tuko katika ulimwengu wa utandawazi. Serikali itaendelea kuchukua hatua kwa watu wote wanaothibitika kwamba wamechangia wanafunzi kukatisha masomo yao lilikwemo suala la kupata mimba. *(Makofi)*

**MHE. DAVID E. SILINDE:** Mheshimiwa Spika, nashukuru. Nina maswali mawili ya nyongeza.

Swali la kwanza, pamoja na majibu yote ya Mheshimiwa Naibu Waziri, lakini kuna mambo mawili, jambo la kwanza mpaka sasa tunapenda kufahamu ni lini Serikali itakuwa na uhakika kama ilivyofanya jana kwenye Kanuni za Bunge kwamba maktaba na maabara katika shule za sekondari za Kata zinafikiwa ili kuongeza kiwango cha elimu?

Mheshimiwa Spika, jambo la pili, tungependa kufahamu Wizara yake inazungumziaje michango ya shilingi 10,000/= ambayo imepangwa na Kamati za Maendeleo za Mikoa katika shule za sekondari katika Wilaya ya Mbozi Magharibi na Mkoa wa Mbeya pamoja na Tanzania nzima kwa ujumla? Tunataka kujua msimamo kwamba ilipangwa kwa kulazimisha wananchi ama wananchi wenyewe ndio walioamua?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. AGGREY D. J. MWANRI):** Mheshimiwa Spika, kuhusu suala la maabara na suala la vyumba vya madarasa na yale majengo mengine yote ambayo yanaonekana kwamba hayajakamilika, tumesema kwamba katika Mpango wa *MMES II*, mpango ambao tunauanza mwaka 2010/2011, tutahakikisha kwamba walau katika shule mbili zilizoko katika Halmashauri tunakamilisha majengo hayo na yanakaa katika sura hiyo ambayo Mheshimiwa Mbunge anaizungumzia. Kwa hiyo, *MMES II* itakwenda lakini itakwenda kwa awamu, itakwenda awamu ya kwanza, awamu ya pili, awamu ya tatu na baadae tutakuwa tumemaliza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuhusu suala la shilingi 10,000/= ambazo zinazungumzwa hapa, na hivi ninavyozungumza natokea Tabora na Kigoma. Kumekuwa na malalamiko mengi sana kuhusu michango ambayo inatolewa pale shuleni. Nataka niseme maneno yafuatayo, kwa michango ile ambayo inahusika na pale shuleni kwa maana mambo kama vile mpishi, kama mlinzi na vitu vingine vinavyojitokeza pale, hakuna mtu yeyote mwenye *mandate* wala *power* ya kuagiza kitu chochote mpaka Bodi ya Shule pale ikae na ikubaliane na wazazi kwamba kiasi hicho ndicho kiasi kilichokubalika. Kwa upande wa ile michango mingine ambayo inahusu maendeleo kwa maana ya madarasa, kwa maana ya shule inayojengwa pale, kwa maana ya nyumba za walimu, pale lazima wakae katika Kamati ya Maendeleo ambayo Mwenyekiti wake ni Diwani wa Kata ile inayohusika pale na baadae kama watataka sasa kwenda juu ya hapo, wapate *sanction* ya Wizara ya TAMISEMI pamoja na Wizara ya Elimu. Kwa hiyo, hakuna mahali popote ambapo wananchi wanalazimishwa na niseme leo hapa kwamba utawalazimisha wananchi kwamba watoe kiasi chochote, lazima wakubaliane katika hivyo vyombo ambavyo nimevieleza hapa ili wananchi wanaweza kuambiwa watoe kiasi hicho wanachokizungumza. *(Makofi)*

*(Hapa Mheshimiwa Godfrey W. Zambi alisimama)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Zambi!  Wote hao Mbozi hao! Aah, samahani Mheshimiwa Zambi! Mheshimiwa Mbowe, Kiongozi wa Kambi ya Upinzani!

**MHE. FREEMAN A. MBOWE – KIONGOZI WA KAMBI YA UPINZANI BUNGENI:** Mheshimiwa Spika, naomba kumuuliza Mheshimiwa Waziri swali moja tu la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, matokeo ya mtihani wa kidato cha nne ambayo yalitangazwa hivi karibuni yameashiria na kuthibitisha janga kubwa kwa Taifa kama hatua za makusudi hazikuchukuliwa. Baada ya mtihani ule, zaidi ya asilimia 50 ya vijana wetu waliofanya mtihani katika shule za Kata wamepata *division zero* na *division four,* asilimia 11 tu ndio wame-*pass*. Sasa vijana ambao wametupwa mtaani kwa maana hii ni wengi sana na ni janga kwa Taifa. Swali langu kwa Mheshimiwa Waziri, je, Serikali ina mpango gani wa makusudi wa kimkakati wa kuweza kuona kwamba vijana hawa zaidi ya asilimia 70 ambao wako mtaani bila kuwa na mafunzo stahiki wanawekewa mkakati wa makusudi hadi hapo sekondari zetu za Kata zitakapokuwa zimekamilika vizuri na walimu wa kutosha kuweza kutoa taaluma inayostahiki? Je, kuna mpango gani wa makusudi wa kimkakati na wa dharura wa kusaidia vijana hawa kwani wanaweza wakawa ni janga kubwa kwa taifa? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. AGGREY D. J. MWANRI):** Mheshimiwa Spika, naelewa kwamba Mheshimiwa Freeman Mbowe ana-*address* kitu *very sensitive* katika nchi yetu na jambo ambalo limekuwa na *reaction* mbalimbali kutoka kwa wananchi mbalimbali na wadau mbalimbali kuhusu suala la elimu na dunia yote inajua kwamba kama huwi mwangalifu na suala zima la *quality* ya *education* unayotoa, *then* unapata matatizo. Nataka niseme mambo yafuatayo:-

Kwanza Serikali imeona, ukiangalia takwimu, ukitumia *the normal curve distribution*, ukiangalia idadi ya watoto waliofanya mtihani huu unaozungumzwa wa *form four* kwa kipindi hiki, idadi ile ni kubwa kwa hiyo, matokeo yake yanaonyesha pia kwamba idadi kubwa wameanguka kwa kiasi hicho anachozungumza Mheshimiwa Mbowe.  *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Serikali inafanya nini, kuhusu mkakati hapa ni kwamba Wizara ya TAMISEMI pamoja na Wizara ya Elimu, sasa hivi kuna jopo ambalo limeundwa ambalo linakaa Dar es Salaam la watalaam na wadau mbalimbali ambao wanatoka katika Wizara hizi mbili nilizozungumzia ili kukaa na kuangalia kwa undani zaidi kwamba ni mambo gani ambayo tunafikiri kwamba yafanyike ili kuweza kuondokana na matatizo haya yaliyozungumzwa hapa. Kwa hiyo, nina hakika kwamba jopo hili litakapokuwa limemaliza shughuli yake, tutaishauri Serikali kwamba tufanye nini. Nataka niseme kwamba kila mmoja wetu anaiona hiyo *concern* ni jambo ambalo wakati mwingine unaweza ukasema linatokana na matokeo na manufaa ambayo sisi wenyewe tumeya-*build up*. Lakini sasa tunataka kui-*address* hiyo *problem* kama

anavyosema. Ningeomba kwa sasa hivi nisiseme chochote kwa sababu najua kwamba Serikali ina mpango huo na baadae tutaeleza kwamba nini kitakachofanyika. *(Makofi)*

**MHE. GODFREY W. ZAMBI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza niwapongeze wananchi wa Tanzania kwa kuamua kwa dhati kabisa kujenga sekondari za Kata kwa kushirikiana na Serikali na kwa maana hiyo kuwafanya vijana wengi ambao wangebaki nyumbani kuweza kupata elimu ya sekondari. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wananchi pia wameitika wito wa kuchangia ujenzi wa hosteli kwa ajili ya watoto wetu ambao wanakaa mbali na maeneo ya shule. Kule Mbozi nina hakika na maeneo mengine katika nchi hii ziko hosteli ambazo zimejengwa. Tatizo ambalo lipo, wale vijana ambao wanakwenda katika hosteli zile hawana uhakika wa chakula maana shule au Kamati za Shule zinawaambia wachangie wenyewe pesa kwa ajili ya chakula na wazazi wengi wameshindwa kuchangia. Serikali sasa ina mpango gani kuhakikisha kwamba inachangia kama si kutoa hela zote kwa ajili ya chakula ili watoto hao waweze kukaa katika sekondari hizo kwa maana ya hosteli na kwa maana hiyo waweze kusoma vizuri?

**NAIBU WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. AGGREY D. J. MWANRI):** Mheshimiwa Spika, kwa sasa tunavyozungumza shule zote za sekondari na shule zote za msingi zimewekwa chini ya Halmashauri na Halmashauri inapokuja na mipango yake inaweka pia *package* hii ya chakula anayoizungumza kwa ajili ya watoto kama alivyoeleza Mbunge. Kwa hiyo, pale shuleni kama inatokea kwamba kuna wanafunzi ambao wanatakiwa wachangie chakula pale ni kwa sababu tu sasa hivi tuko katika kipindi cha mpito, lakini mpango tulionao katika Halmashauri sasa hivi, ni kuhakikisha kwamba wakati wa mavuno chakula chote ambacho kinahitajika kwa ajili ya watoto kinawekwa katika stoo ili kuhakikisha kwamba kinahifadhiwa kama wanavyofanya katika Mashirika ya Dini, ili wakati chakula kinapoadimika tusifike katika hali hii ambayo anaizungumza hapa sasa hivi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hili ni jambo ambalo tunalifanyia kazi na Halmashauri zote zimetakiwa zihakikishe kwamba chakula kinapatikana kupitia Bajeti hii ambayo tunaizungumzia hapa. Na *package* hii ya chakula kwa ajili ya watoto nayo inakuwepo pale. *(Makofi)*

**SPIKA:** Tumetumia muda mwingi sana, dakika kumi na tano kwa swali hili tumechukua muda wa maswali mengine. Mheshimiwa Waziri Mkuu tafadhali.

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, nimeona nisimame kidogo kwa ajili ya jambo hili kwa sababu ni jambo kubwa, kuhusu alivyosema Mheshimiwa Mbowe nadhani jibu lile ni sahihi lakini nilikuwa nadhani njia nyingine bora baada ya kumaliza ile pengine ni vizuri tukaja tukatoa Kauli ya Serikali ili pengine Bunge liweze kujua tumefikia wapi.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, tutajitahidi kama si Bunge hili angalau Bunge linalokuja kwa sababu kazi ni kubwa kidogo. Lakini jambo la pili la chakula katika shule za sekondari na mimi nasema siyo sekondari tu hata shule za msingi. Sehemu zote ambako shule zimekuwa na mpango wa kuwapa chakula watoto zimekuwa na tija zaidi kuliko shule zile ambazo watoto hawapati chakula. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tatizo ninaloliona ni dhana ambayo mimi nadhani siyo sahihi sana kwamba wazazi wanaacha lile jukumu la kusaidia kuwapatia chakula watoto, wanashinda na njaa wakati wa kupata elimu ya msingi, ukiuliza sababu kusema kweli haipo. Rai yangu kwa Watanzania watoto wale wangekuwa nyumbani wangekula chakula cha mchana, jioni tena wangepata chakula na wakaenda kulala. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba nitoe wito wangu kuwa mpango ule wa kuwaomba wazazi waone jukumu hilo kwamba bado ni lao la kuchangia chakula, mahindi, maharage na vitu vingine ili viweze kuwasaidia wanafunzi pale katika shule za misingi lakini na katika shule za sekondari. Kwa sababu shule za sekondari kwa makusudi tulisema zijengwe kwenye Kata kupunguza gharama na namna moja ilikuwa ni kwamba masuala ya chakula watoto wale wa karibu wanaweza kula na wazazi wao na wale ambao wametoka mbali kidogo wazazi wachangie chakula kwa maana ya mahindi na vyakula vingine vya kawaida wakati Serikali nayo inaendelea kutoa msaada kwa namna itakavyoweza. Haiwezi kuwa jambo hili lote liachiwe Serikali kwa asilimia mia moja, hapana. *(Makofi)*

Na. 16

**Fedha za Kukamilisha Ujenzi wa Maboma ya Shule**

**MHE. DKT. FESTUS B. LIMBU** aliuliza:-

Wananchi wa Wilaya ya Magu walihamasika sana na wito wa Serikali wa kujitolea kujenga maboma kwa ajili ya madarasa na nyumba za walimu na kwamba hivi sasa kuna jumla ya maboma 138 ya nyumba za walimu na maboma 165 ya madarasa yaliyokamilika:-

(a) Je, ni lini Serikali itatoa fedha kwa ajili ya kuezeka na kumalizia maboma haya?

(b) Iwapo fedha haitatolewa kumalizia maboma haya, je, Serikali haioni kuwa itawakatisha tamaa wananchi kuendelea na moyo wa kujitolea?

**NAIBU WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. AGGREY D. J. MWANRI)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimwia Waziri Mkuu, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Dkt. Festus Bulugu Limbu, Mbunge wa Magu, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, ni jukumu la wananchi, Halmashauri kwa kushirikiana na Serikali kuhakikisha kuwa fedha za kutosha zinapatikana kuwezesha ujenzi wa madarasa, nyumba za walimu na majengo mengine muhimu kwa lengo la kuboresha mazingira ya kujifunzia na kufundishia nchini. Katika mwaka wa fedha 2009/2010 shilingi 392,677,000 zilitolewa kama ruzuku ya maendeleo kupitia mpango wa maendeleo wa elimu ya msingi katika Halmashauri ya Wilaya ya Magu kwa ajili ya kukamilisha jumla ya vyumba vya madarasa 13, nyumba za walimu 23 na matundu ya vyoo 162.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa elimu ya sekondari Halmashauri ya Wilaya ya Magu mwaka wa fedha 2009/2010 ilipata shilingi 1,062,348,748/= kwa ajili ya ujenzi wa miundombinu mbalimbali ikiwa ni ya shule mbalimbali kwa mfano ujenzi wa madarasa, vyoo, maabara, jengo la utawala, bwalo, visim virefu na hosteli.

(b) Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia maelezo niliyoyatoa katika kipengele (a) ni wazi kwamba Serikali haijawakatisha tamaa na kuwavunja moyo wananchi. Naomba kuchukua nafasi hii kupitia Bunge lako Tukufu kuwapongeza wananchi wa Wilaya ya Magu kwa kazi nzuri waliyoifanya ya kuweka miundombinu ya kuwasaidia kuendeleza elimu katika eneo lao.

**MHE. DKT. FESTUS B. LIMBU:** Mheshimiwa Spika, napenda kumshukuru sana Naibu Waziri kwa majibu mazuri lakini nina swali la nyongeza.

Mhehsimiwa Spika, Naibu Waziri amesema kwamba amechangia ujenzi wa madarasa machache sana ikilinganiswa na maboma ambayo wananchi walihamasika na wakajitolea kujenga maboma 138 ya nyumba za walimu na maboma 165 ya madarasa ukiondoa majengo ya maabara, vyoo na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, fedha hizi ni kidogo sana kusaidia nguvu za wananchi ambao bado wanakabiliwa na michango mbalimbali, kujenga hosteli, kujenga maabara, kujenga vyoo, wachangie zahanati, wachangie vituo vya polisi, mahakama za mwanzo, kuchangia maji na afya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Waziri haoni kwamba mchango huu ni mdogo sana kuwaunga mkono wananchi na kwamba Serikali inabidi iweke mkakati maalum wa kusaidia zaidi wananchi ili nguvu zilizotumika huko nyuma kuchangia ziweze kusaidiwa na waendelee kuchangia zaidi katika miradi mingine ya maendeleo. *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. AGGREY D. J. MWANRI):** Mheshimiwa Spika, labda niliweke vizuri hapa kwamba, haya maboma anayoyazungumza Dkt. Limbu, mimi ninayafahamu, nimekwenda nimeyaona, kilichotokea hapa na ndiyo maana tunamalizia hapa kwa kupongeza Wilaya ya Magu ni kwamba amefanya kazi kubwa sana yeye Mbunge pamoja wananchi pale na *almost* wame-*over mobilised* ndicho kilichotokea pale. Kuna jitihada kubwa ambayo imefanywa pale na wananchi ambayo mimi naona na Madiwani wamefanya kazi nzuri pale.

Anachokisema hapa ni kweli anaona kwamba hela hizi ninazozitaja hapa ni kidogo lakini hela zinazokwenda pale, hii Bajeti inayozungumzwa hapa ni *cash budget. (Makofi)*

Mheshimiwa Spika, *cash budget* maana yake nini, kama unakwenda Dar es Salaam una shilingi elfu ishirini maana yake utaangalia suala la nauli ya kukufikisha Dar es Salaam ukienda ukanunua vitumbua, maandazi hutakwenda Dar es Salaam utabaki hapo hapo. Kinachozungumzwa hapa na ambacho mimi nafikiri Dkt. Festus Limbu amekizungumza hapa cha maana kabisa ni kwamba hela tumezipitisha sisi wenyewe hapa, hela hizo tukasema ndiyo zikapita, akisema ni zipi tena mimi nitasema kuna hela za *Local Government Capital Development Grant* zinakwenda pale, *fifty percent* zinabaki katika Halmashauri, *fifty percent* nyingine inaondoka inakwenda katika miradi ile.

Kwa hiyo, anaweza akaangalia pale kuna hela za *Constituency Development Catalyst Fund* zinakwenda kwa ajili ya Mbunge pale. Anaweza akasema hela unazozipeleka pale inategemeana na kipaumbele unachojiwekea, kama hela zako ni kidogo basi unaweka kipaumbele, kama hela zako ni nyingi unaweza ukasema hizi peleka kwenye madarasa na kwingineko kwa sababu unazo nyingi, kama ni kidogo una-*rearrange your priorities* ili ilingane na mahitaji yako. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nataka niseme hapa kwamba Halmashauri ya Magu ikileta katika Bajeti mwaka huu ikasema sisi tunataka tumalizie maboma yote haya, sidhani kama Serikali itakataa itasema ndiyo. Kwa hiyo, mimi ninachosema hapa ni kwamba tunawaunga mkono, wamefanya kazi nzuri. *really big up* kwa upande wa Magu kwa sababu wameitikia wito wa Serikali, lakini tatizo letu ni hilo tunalozungumza la Bajeti hapa na kama wakileta kama *priority* sisi tutaipitisha hatuna tatizo kabisa na hilo. *(Makofi)*

Na. 17

**Malipo ya Vibarua katika Kazi za Maendeleo**

**MHE. VITA R. KAWAWA** aliuliza:-

Kumekuwa na miradi ya kukuza uchumi inayoendelea mahali pengi ikiwemo ya ujenzi wa barabara, majengo ya aina mbalimbali, viwanda na hata kwenye migodi ya machimbo ya madini lakini kiasi wanacholipwa vibarua kwenye kazi hizo ni kidogo mno ikilinganishwa na kazi kubwa na ngumu wanazozifanya:-

Kwa mujibu wa sheria ya kazi, je, ni kiasi gani kibarua anapaswa kulipwa kwa siku katika sekta hiyo ya ujenzi?

**NAIBU WAZIRI WA KAZI NA AJIRA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Vita Rashid Kawawa, Mbunge wa Namtumbo, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kifungu cha 14(1) cha Sheria ya Ajira na Mahusiano Kazini Na. 6 ya mwaka 2004 kuna aina tatu za mikataba ambayo ni:-

(a) Ajira ya Mkataba Usiokuwa na Muda Maalum *(Contract of Employment with Unspecified period of Time);*

(b) Ajira ya Mkataba wa Muda Maalum *(Fixed Term Contract);* na

(c) Ajira ya Mkataba wa Kazi Maalum *(Contract of Employment for Specific Task).*

Mheshimiwa Spika, hivyo hakuna ajira za vibarua (*Casuala Employees*) kwa mujibu wa sheria za kazi.

Mheshimiwa Spika, mfumo wa malipo (*mode of payment*) kwa mikataba iliyoainishwa kisheria waweza kuwa wa mwezi, wiki, wiki mbili au kwa siku kutegemeana na makubalianao ya pande husika yaani mfanyakazi na mwajiri.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa tangazo la Serikali Na. 172 la mwaka 2010, ambalo lilianza kutumika tarehe 1/5/2010 mishahara imewekwa kwa kuzingatia sekta. Aidha, vima vinavyoonyeshwa katika sheria hiyo vinaweza kuboreshwa kupitia majadiliano baina ya wafanyakazi na waajiri katika sehemu zao za kazi *(collective bargaining)* kama inavyoelekezwa kwenye sehemu ya sita ya sheria hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kima cha chini cha mshahara katika sekta ya ujenzi ni shilingi 80,000/= kwa mwezi ambapo ni sawa na shilingi 3,080/= kwa siku. Serikali imeona ukubwa wa shughuli za sekta hii hivyo ipo kwenye mchakato wa kuunda Bodi ya Sekta ya Ujenzi ambapo mishahara na mazingira ya kazi vitaangaliwa kwa umakini zaidi na hatimaye kuishauri Serikali ipasavyo. *(Makofi)*

**MHE. VITA R. KAWAWA:** Mheshimiwa Spika, asante kwa kunipa fursa hii kuuliza maswali mawili ya nyongeza:-

(a) Kwa kuwa miradi hii ya ujenzi hususani ya barabara inaendelea kwa kasi nchini na nia ya Serikali ni kuwawezesha wananchi kiuchumi hususani pale kwenye miradi hiyo ya barabara wananchi wanaozunguka kwenye maeneo hayo wapate ajira inayokidhi maisha yao ya sasa na kwa kuwa bei ya sukari imepanda, bei ya unga imepanda, bei ya mafuta ya kupikia imepanda, bei ya mkate imepanda na bei ya mahitaji mengine yamepanda.

Je, Serikali haioni ipo haja ya kurekebisha kipato hicho cha shilingi 3,080 kwa siku kabla ya kuunda bodi hiyo ili wananchi hao waweze kukidhi mahitaji yao ya maisha kwa sasa?

(b) Kwa kuwa kiwango cha shilingi 3,080 kwa siku ni kidogo na ndicho kinachowafanya wafanyakazi wa ujenzi wa barabara kutengeza *organise crime* ya kuiba mafuta kama tulivyojionea katika barabara ya Iyovi - Iringa, wizi wa mafuta wa shilingi bilioni mbili, hivyo Serikali inaweza kulitizama hili kwa karibu sana ili kupunguza uwezekano wa kuendelea kwa hujuma hizo katika miradi mingine?

**NAIBU WAZIRI WA KAZI NA AJIRA:** Mheshimiwa Spika, mimi nakubaliana kabisa na *concerns* za Mbunge kuhusu kiwango hicho cha chini na hata katika majibu yangu ya msingi nilisema ni kiwango kidogo kulingana na kazi kubwa iliyopo kwenye sekta hii ya ujenzi, ndiyo maana nimesema Serikali ipo katika mchakato wa kuunda bodi ya sekta hii ya ujenzi ambayo ilikuwa haijaundwa na mimi ni matumaini yangu kwamba bodi hii itaundwa mapema. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kusema kwamba labda tupandishe kabla ya bodi kuundwa na wakati ambapo tayari tumeshaweka utaratibu wa kuundwa kwa bodi hizi itakuwa si vyema. Namshauri Mbunge na hawa wafanyakazi ambao kwa kweli kwa lugha ya mjini wanasema wanahenyeka sana, wasubiri ili bodi hii iundwe na viwango hivi viweze kupanda. *(Makofi)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, naomba maswali ya nyongeza yawe mafupi maana wengine wanafanya hotuba.

**MHE. PINDI H. CHANA:** Mheshimiwa Spika pamoja na majibu mazuri sana ya Waziri naomba niulize swali la nyongeza kama ifuatavyo, kwa kuwa vijana ni 60% ya idadi ya watu wa Tanzania, na kwa kuwa vijana wanahitaji sana shughuli mbalimbali za kujikimu pamoja na bodi hiyo ambayo itaundwa, Wizara ina mpango gani wa kuanzisha *job centres* kila Mkoa, kila Wilaya na kuweka sera nzuri ili vijana wakatafute ajira hizo za uhakika kwenye *job centres* kwenye taasisi ambazo zina *insurance,* taasisi ambazo zinalipa riba na haki zao ziweze kuzingatiwa. *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA KAZI NA AJIRA:** Mheshimiwa Spika, alilolisema ni kweli kabisa kwamba vijana ni asilimia kubwa sana ya nguvu kazi ya Taifa hili, na suala la ajira ni tatizo lao kubwa namba moja. Pendekezo lake ni zuri la kuanzisha, sisi tunasema *employment desks* katika maeneo hasa kwenye Halmashauri zetu. Sisi kama Serikali tumeshaliona hilo na tumeanza *pilot programmes* katika mikoa kadhaa katika Halmashauri kadhaa hasa za Kusini ambapo tunataka ikiwezekana katika Halmashauri zote tuanzishe hizi *desks* kwa ajili ya ajira.

Mheshimiwa Spika, unaposema ajira ni ajira kwa vijana. Sisi kwenye Wizara kwa maana ya Makao Makuu tayari tunalo *desks* hili kwa sababu tuna idara lakini vile vile tuna *TaESA* ambayo inatoa maelekezo na inaunganisha wanaotaka ajira na wale wanaotaka waajiriwe, lakini pamoja na kuwa na ofisi katika Kanda kadhaa bado haijatosheleza vijana kuweza kupata ushauri nasaha kuhusu namna wanavyoweza kupata ajira.

Kwa hiyo, suluhisho kama unavyosema kwa kweli ni kuanzisha hizi *employment desks* ambazo zitakuwa kila Halmashauri na wale wanaoweza ningeomba waanze sasa hivi kuweka hizo *desks* za kushauri vijara namna ya kupata ajira na vile vile kuweza kuwaunganisha na waajiri ambao wako tayari kuwaajiri hawa vijana. *(Makofi)*

Na. 18

**Vijana Wanaohitimu Elimu ya Juu**

**MHE. NEEMA M. HAMID** aliuliza:-

Serikali imefanya jitihada kubwa kuhakikisha kuwa vijana wengi wanapata elimu ya juu kwa udhihirisho wa kuwepo kwa Vyuo Vikuu vingi hapa nchini:-

(a) Je, Serikali imejiandaa vipi kutumia nguvu kazi hiyo kwa maendeleo ya nchi?

(b) Je, Serikali inafuatilia vipi vijana wanaomaliza masomo yao katika fani mbalimbali kuona kama wameweza kujiajiri au kuajiriwa?

**NAIBU WAZIRI WA KAZI NA AJIRA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Neema Mgaya Hamid, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Kwanza, tunamshukuru Mbunge kwa kutambua juhudi kubwa za Serikali kuongeza Vyuo Vikuu nchini na udahili wake. Nakubaliana pia na Mbunge kwamba ili nchi iendele tunahitaji nguvu kazi yenye uwezo wa kujiajiri na kuajiriwa. Kwa upande wa sekta ya umma mfumo wa ajira umeboreshwa kwa kuanzisha Sekretariati ya Ajira katika Utumishi wa Umma. Hata hivyo, wahitimu wenye taaluma adimu kama madaktari, walimu na maafisa kilimo wanapangiwa kazi moja kwa moja baada ya kumaliza mafunzo yao.

Mheshimiwa Spika, ili kuwaunganisha watafuta kazi na waajiri, Serikali pia imeanzisha Wakala wa Huduma za Ajira Tanzania (*TaESA*) iliyoko chini ya Wizara ya Kazi na Ajira, kwa upande wa sekta binafsi, Serikali imeweka mazingira mazuri ya kisera na kisheria ili kukaribisha uwekezaji wa mitaji ya ndani na nje ya nchi kwa lengo la kupanua wigo wa fursa mbalimbali za ajira katika sekta zenye uwezo wa kuzalisha ajira nyingi kama vile uzalishaji na usindikaji wa mazao ya kilimo na ufugaji, mawasiliano, ujenzi, madini, biashara na uvuvi.

Aidha, vyuo vya elimu ya juu vimehimizwa kuingiza masuala ya ujasiriamali katika mitaala yao. Baadhi ya vyuo vimeanzisha *enterpreneurship centres* ili kutilia mkazo suala la kujiajiri kwa wahitimu hao, tukitambua kuwa hata kwa wahitimu wa Vyuo Vikuu fursa kubwa iko kwenye ajira ya kujiajiri kuliko kuajiriwa.

(b) Wizara yangu kwa kushirikiana na Ofisi ya Taifa ya Takwimu imekuwa ikifanya tafiti na kutoa taarifa ya nguvu kazi kila baada ya miaka mitano ili kujua

mchango wa nguvu kazi hiyo katika uchumi wa Taifa. Kwa vile utaratibu huu ni wa muda mrefu, hautuwezeshi kupata taarifa za kila mwaka.

Hivyo Serikali inaboresha mfumo wa ukusanyaji wa taarifa za kila mwaka. Hivyo Serikali inaboresha mfumo wa ukusanyaji wa taarifa za soko la ajira kwa kushirikiana na wadau kama Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi (Vyuo Vikuu, Bodi ya Mikopo, Tume ya Vyuo Vikuu), Wizara ya Mambo ya Ndani (Wakala wa Vitambulisho vya Taifa) itakapokuwa imekamilika, Wizara ya Fedha na Uchumi (Ofisi ya Taifa Takwimu) na Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma (Sekretarieti ya Ajira). Kwa kupitia utaratibu huu Serikali itaweza kufahamu wahitimu wako sehemu gani na wanajihusisha na nini.

**MHE. NEEMA MGAYA HAMID:** Mheshimiwa Spika, kwa kuwa vijana wanaomaliza elimu ya Juu kwa wingi wao wote hawawezi kupata ajira Serikalini ama katika mashirika binafsi. Kwanza, je, Serikali ina mkakati gani katika kuwawezesha vijana hawa kuwapatia nyenzo mbalimbali ambazo zitaweza kuwawezesha wao kujipatia wenyewe na kujipatia maendeleo? Pili, ni vipi sera ya uwezeshaji inavyowagusa vijana hawa wanaomaliza Vyuo Vikuu?

**NAIBU WAZIRI, KAZI NA AJIRA:** Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba vijana wanaomaliza Chuo Kikuu, wanahitaji nyenzo kwa wale ambao hawawezi kupata ajira moja kwa moja. Lakini naamini kabisa nyenzo hizi zitakuwa zina manufaa kama vijana hawa watakuwa wanao uwezo, ujuzi wa kuendesha biashara zao na ndio maana nimesema kwamba kwa kweli ni vema vyuo vyetu vikaanzisha kwa wingi *course* za *entrepreneurship* ili vijana wakitoka pale waweze kutafuta namna ya kutafuta nyenzo na Serikali inaweza kuwaelekeza namna ya kupata mikopo. Tayari Mifuko mbalimbali ya kusaidia vijana kupata nyenzo imeshaanzishwa ingawaje bado haitoshelezi.

Kuhusu uwezeshwaji, nadhani ndio swali hilo hilo kwamba vijana wanahitaji kuwezeshwa. Lakini katika kuwezeshwa maana yake ni kwamba kupata elimu ya ujasiriamali, kuwezeshwa ni pamoja na kuwaweka vijana kuwa tayari kujiwezesha kuweza kufanya kazi au shughuli zinazoweza kuwainua kimapato. Lakini kuwawezesha vilevile ni kuwaelekeza namna wanavyoweza kupata mitaji kwa wale ambao wanafanya kazi za biashara au uzalishaji. Hiyo nadhani katika yote hayo Serikali imeweka mikakati mbalimbali ya kusaidia vijana. Jambo la msingi vijana wajitokeze katika kufuatilia fursa hii ambazo zipo.

Na. 19

**Utekelezaji wa Miradi ya MCC na REA kufikisha Umeme Vijijini**

**MHE. GEORGE B. SIMBACHAWENE** aliuliza:-

Inafahamika kuwa miradi ya *MCC* na *REA* ilikwishafikia hatua nzuri kiutendaji wakati Bunge la Tisa likimaliza muda wake na kwamba wananchi wanasubiri kwa shauku kubwa kufikisha umeme hasa walioko vijijini:-

Je, ni sababu zipi zinazosababisha miradi hiyo kusuasua au kuchelewa kuanza?

**WAZIRI WA NISHATI NA MADINI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa George Boniface Simbachawene, Mbunge wa Kibakwe, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, miradi ya *MCC* na *REA* haijasuasua wala kuchelewa kuanza. Utekelezaji wa miradi muhimu kama hii ya umeme inahitaji kukamilika kwa maandalizi yote muhimu kabla ya kuanza utekelezaji wake. Zipo hatua na kanuni za msingi ambazo hazina njia za mkato.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa *MCC* naomba kueleza kuwa jambo la kwanza lilikuwa ni kuandaa nyaraka timilifu na taratibu za zabuni za mradi mzima wa ukarabati na upanuzi wa miundombinu ya kusafirisha na kusambaza umeme katika Mikoa ya Mbeya, Iringa, Dodoma, Morogoro, Mwanza na Tanga. Makabrasha ya zabuni kwa ajili ya kumpata mkandarasi wa ujenzi yalikamilika na kisha kutangazwa tarehe 15 Machi 2010. Zabuni zilifunguliwa tarehe 9 Julai 2010 na watalaam wetu kufanya tathmini za zabuni zilizowasilishwa ili kumpata mshindi kulingana na kanuni za ushindani wa uwazi.

Mheshimiwa Spika, kulingana na matokeo ya uchambuzi wa zabuni zilizowasilishwa tarehe 13 Septemba, 2010 Wakandarasi wawili yaani kampuni ya *SYMBION power LLC* kutoka *Washington DC* Marekani kwa Mikoa ya Mwanza, Tanga, Morogoro, Iringa na Mbeya na Kampuni ya *PIKE electronic,* kwa Mkoa wa Dodoma kutoka *North Carolina* Marekani zilitangazwa washindi na kuingia mikataba nazo.

Mheshimiwa Spika, mpaka wakati huu ninapojibu swali hili, wakandarasi wote wawili wameshafungua ofisi zao na wako kwenye maeneo ya miradi wakifanya tathmini na uhakiki wa maeneo ya kazi ikiwa ni pamoja na kufanya *detail survey* ya njia zote za umeme wa msongo wa kati na msongo mdogo ikiwa ni pamoja na kuandaa usanifu wa njia hizo na nyaraka muhimu na michoro ya kufanyia kazi.

Mheshimiwa Spika, baada ya kukamilika kwa zoezi linaloendelea sasa na kupata baraka za Mhandisi Mshauri akishirikiana na Kampuni ya *TANESCO* na *MCA* – T kazi rasmi ya kusimika nguzo kama sehemu ya ujenzi wa mradi itaanza. Taratibu na malipo ya fidia kwa walioathiriwa na mradi huu zitakamilika mwezi Mei, 2011. Inatarajiwa kwamba miradi hii itakamilika mwezi Novemba, 2012.

Mheshimiwa Spika, tunapenda kuchukua nafasi hii kuuomba uongozi wa Mikoa na Wilaya zinazohusika na wananchi kwa ujumla kutoa ushirikiano wa hali ya juu ili miradi hii iweze kukamilisha kama ilivyopangwa. Jibu hili linawakilisha Mikoa yote

niliyoitaja kwa wale ambao wanahusika akiwemo Naibu Spika, Mheshimiwa Job Ndugai pamoja na Waheshimiwa Wabunge wa Majimbo mengine ambako mradi wa *MCC* unatekelezwa.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa miradi inayofadhiliwa na *REA* kwa maana ya Wakala wa Nishati Vijijini, mikataba kati ya wakandarasi na *TANESCO* juu ya ujenzi wa miradi hii ilikwishakamilika miradi ipo kwenye hatua mbalimbali za utekelezaji katika Mikoa kumi na sita na inategemewa kukamilika mwishoni mwa mwaka 2011. Kwa hiyo, miradi ya *REA* yote Waheshimiwa Wabunge, kama wanavyofahamu kutoka kwenye Majimbo yao iko kwenye hatua mbalimbali za utekelezaji na itakamilika ndani ya mwaka huu. Kazi zilizokwishafanyika ni pamoja na kukamilika kwa usanifu, upimaji na usafishaji wa njia ambamo miundombinu ya umeme itajengwa. Kazi zinazoendelea ni pamoja na upelekaji wa vifaa kwenye maeneo ya kazi, tathmini ya ulipaji wa fidia na usimamishaji wa nguzo za umeme msongo mkubwa katika baadhi ya miradi.

Mheshimiwa Spika, miradi ya umeme ni miradi mikubwa yenye taratibu mbalimbali ambazo haziepukiki. Nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge na wananchi wa Kibakwe, Bunge lako Tukufu na Watanzania kwa ujumla kwamba miradi hii itakamilika katika muda uliopangwa.

**MHE. GEORGE B. SIMBACHAWENE:** Mheshimiwa Spika, kwanza nimshukuru Mheshimiwa Waziri kwa kuteuliwa tena na Mheshimiwa Rais na kuwa Waziri tena wa Wizara hii na hivyo kufanya mwendelezo mzuri wa mambo yetu ya umeme. Naamini anaweza sana.

Mheshimiwa Spika, kwa kweli *MCC* na *REA* ukiangalia kasi yake angalau kidogo *REA* wanakwenda kwa *speed* kubwa. Lakini *MCC* hapa tumezungumza miaka mitano yote imepita na Mheshimiwa Waziri anasema kwamba mchakato wake ni mrefu.

Kwanza, je, ni lini sasa tutaanza kuona kazi kwenye *site* pale kuna shughuli inaendelea ili wananchi na sisi tujue majibu ya kuwapa?

Pili, Miradi hii ilichukua muda mrefu sana katika usanifu na taratibu zake kama alivyosema kuna mambo mengi sana ya kuangalia. Lakini *design* na mambo mengine yote yalipofanyika yamekaa muda mrefu na kuja kukuta wanapokwenda kwenye *implementation* tayari imepitwa na wakati. Mazingira yaliyokuwepo wakati ule yamebadilika sana na ndio maana Mheshimiwa Waziri, nilikuuliza swali katika kipindi cha Bunge la Tisa kwamba kwa nini sasa badala ya ile *line* ya kutoka Kibakwe-Chamtumile-Kidenge-Mungui hadi Pwaga hali yake imebadilika kutoka maendeleo mengi katika vijiji vya pembeni na hivyo ukiweka leo umeme katika *line* ile unaonekana ni mtu wa ajabu kweli kwa sababu unaacha huduma hii muhimu kwa sehemu ambazo zimeendelea za Ikuyu, Luhundwa, Pwaga, Lumuma, hadi kuelekea Idole kwa Mheshimiwa Mkullo kule ambako kuna *centre* kubwa ya kibiashara na kilimo cha umwagiliaji. Huko Lumuma, maana yake tuna-*share* mimi na Mkullo. Je, Mheshimiwa Waziri baada ya swali langu kujibiwa kwenye Bunge la Tisa na baada ya mazungumzo

ya mimi na yeye hali ya kupitisha umeme Kijiji cha Ikuyu, Luhundwa, Lumuma hadi Idole makubaliano yetu yako vile vile au ndio mambo mapya tena yanaanza?

**SPIKA:** Naomba majibu kwa kifupi sana.

**WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Spika, kwanza nimshukuru sana Mheshimiwa George Simbachawene kwa kunipongeza kwa uteuzi huu kwa mara nyingine na naendelea kumshukuru Mheshimiwa Rais. Kuhusu utekelezaji kama nilivyosema ni kweli, kwa matarajio ya kawaida tunaweza kuona miradi hii imechelewa lakini kama nilivyosema taratibu zake ni ndefu. Lakini hapa tulipofikia ni mahali pazuri kwa sababu utekelezaji wa miradi hii inayofadhiliwa na *MCC* umeshaanza na tunakubaliana na Waheshimiwa Wabunge wote, ambao wanafaidika na mradi huu.

Mheshimiwa Spika, nafahamu kuna changamoto Mkoa wa Kigoma pale kwa sababu katika ile Malagarasi kulitokea tatizo la kimazingira lakini hilo linafanyiwa kazi na Waheshimiwa Wabunge na wananchi wa Mkoa wa Dodoma wanafahamu sasa inafanyiwa tathmini katika eneo lile la Igamba *three* ili mradi huo uendelee. Utakuwa umechelewa kidogo. Lakini kuna maeneo mengine kwa kumjibu Mheshimiwa Simbachawene ni kwamba utekelezaji utaanza tukishakamilisha kuwalipa fidia walioathirika ambapo nimesema ni mwezi wa tano. Hizo heka heka za kuona mitambo inasimikwa kwa mfano, nguzo zinasimikwa sasa katika maeneo ambako miradi hiyo itafanyika itaonekana wakati huo. Kwa maeneo ambayo ulipaji wa fidia utawahi kidogo kazi hiyo inaweza kuanza mapema zaidi.

Kuhusu makubaliano yetu na Mheshimiwa George Simbachawene kwa maeneo ambayo ameyataja Ikuyu mpaka Idole, makubaliano yetu yako pale pale hayajabadilika. Niseme tu kwamba, kwa maeneo ambayo yameathirika na hayapo sasa katika utekelezaji kupitia mradi wa *MCC* yatatekelezwa kupitia Wakala wa Nishati Vijijini. Hilo ndio ambalo tuliongea na Mheshimiwa Simbachawene naendelea kumhakikisha kwamba utekelezaji wake upo kupitia Wakala wa Nishati Vijijini.

**MHE. JENISTA J. MHAGAMA:** Mheshimiwa Spika, kwa kuwa miradi hii ya *MCC* ni miradi mikubwa sana katika nchi yetu na inakwenda sambamba na ile miradi mingine mikubwa kama ule wa kupeleka umeme wa *grid* ya Taifa katika Mkoa wa Ruvuma ukitokea pale Makambako. Mheshimiwa Waziri anakumbuka kwamba hii ni kero kubwa sana kwa wananchi wa Mkoa wa Ruvuma na mradi huo utasaidia sana kuleta maendeleo katika Kata za Wino, Mahanje, Mkongotema, Gumbiro, Wilaya ya Mbinga, Namtumbo na Tunduru. Je, Mheshimiwa Waziri anaweza kunisaidia kujua ni lini mradi unaweza kuanza kwa sababu imekuwa ni historia ya miaka takriban saba sasa? *(Makofi)*

**WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Spika, ni kweli mradi unaojulikana kama Makambako Songea kwa jinsi ulivyobuniwa na taratibu za makabrasha ukawa umechukua muda mrefu, lakini kama nilivyosema miradi hii inachukua muda mrefu kwa sababu ya taratibu zake. Lakini kikubwa sasa hivi tulishamaliza, Wizara ya Fedha, chini ya Mheshimiwa Waziri Mkullo na watalaam wetu kwa ujumla walishasaini mikataba yote inayohitajika. Mradi huu una thamani ya dola za

Kimarekani milioni 70.4. Tumepata msaada kwa kiwango kikubwa sana kutoka kwa marafiki zetu nchi ya Sweden kupitia Shirika la Maendeleo *SIDA*.

Mwezi huu, wiki ijayo atapatikana Mshauri Mwelekezi atakayesimamia zoezi la kuwapata Wakandarasi kwa sababu mradi ule ni mkubwa, kilomita zaidi ya 250, unakwenda mpaka unaunganisha Mkoa wa Ruvuma mpaka Songea Mjini lakini unakwenda pia Wilaya za Mbinga kwa Mheshimiwa Captain Komba. Lakini pia mpaka Namtumbo kwa Mheshimiwa Vita Kawawa na maeneo mengine unakopitia. Mradi huu utahitaji Wakandarasi zaidi ya mmoja katika hali ya kawaida. Kwa hiyo, tenda itakapotangazwa, washindani watashindana lakini kwa utaratibu wa tenda ni siku 45 wakati mwingine zinaweza kuwa siku chache zaidi. *(Makofi)*

Ninachotaka kusema katikati ya mwaka huu wananchi wote wa Mikoa hiyo ambayo watanufaika na mradi huu wakiwemo wananchi wa Wilaya za Ludewa wataona heka heka zinaanza kwa sababu utekelezaji utakuwa umeanza wakandarasi watakuwa wameshapatikana. Kwa hiyo, utekelezaji wa mradi huu unaendelea vizuri.

Na. 20

**Sababu zilizochangia tatizo la Njaa Wilayani Rombo**

**MHE. JOSEPH ROMAN SELASINI** aliuliza:-

Moja kati ya sababu zilizochangia Wilaya ya Rombo hasa uwanda wa tambarare kukabiliwa na tatizo la njaa mara kwa mara ni pamoja na ukame mkubwa hasa maeneo ya tambarare, ukosefu wa kitengo cha Hifadhi ya Chakula na kiwango kikubwa cha uharibifu wa mazao unaotokana na tembo kutoka nchi jirani ya Kenya:-

(a) Je, Serikali ina mpango gani wa kuanzisha hifadhi ya chakula Wilayani Rombo?

(b) Je, Serikali ina mikakati gani ya makusudi ya kudhibiti tembo ambao mara kadhaa huchangia uharibifu mkubwa wa mazao?

(c) Je, ni utaratibu gani umewekwa wa kuwalipa fidia wananchi ambao mazao na mali zao zimeharibiwa na tembo hao?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Selasini Joseph Roman, Mbunge wa Rombo, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Serikali imejenga na inanunua na kuhifadhi chakula katika maghala ya kuhifadhia chakula yanayosimamiwa na Wakala wa Taifa wa Hifadhi ya Chakula *(NFRA)* katika kanda saba nchini. Maghala hayo yapo katika Ofisi za Kanda *NFRA*

zilizopo Arusha Dodoma, Shinyanga Sumbawanga, Makambako, Songea na Kipawa Dar es Salaam. Kanda ya Arusha inahudumia Mikoa ya Arusha, Manyara, Kilimanjaro na Tanga. Hivyo, Wilaya ya Rombo inahudumiwa na ghala lililopo katika Kanda ya Arusha. Kutokana na utaratibu huo, kwa sasa Serikali haina mpango wa kuanzisha Hifadhi ya Chakula Wilayani Rombo kwa kuwa tayari Wilaya hiyo inahudumiwa na *NFRA* Kanda ya Arusha.

(b) Ili kuwadhibiti tembo ambao wanafanya uharibifu wa mara kwa mara wa mazao ya wakulima Wilayani Rombo, Serikali imejenga kituo cha kudumu cha kudhibiti wanyamapori waharibifu wa mazao katika Kijiji cha Ngoyoni na imekipatia askari wa wanyamapori na gari la doria. Aidha, Serikali imeanza utaratibu wa kuwahusisha wananchi katika udhibiti na kupanga mikakati na mbinu mbadala za kuwadhibiti wanyama hao. Mbinu hizi ni pamoja na matumizi ya uzio wa kamba iliyopakwa mchanganyiko wa pilipili na *oil* chafu kuzunguka shamba. Mbinu nyingine ni matumizi ya matofali ya kinyesi cha ndovu kilichochanganywa na pilipili ambacho moshi wake ni mkali na hivyo hufukuza ndovu mashambani.

(c) Serikali kupitia Wizara ya Maliasili na Utalii katika mwaka 2007 ilitoa mwongozo wa viwango vya vifuta jasho na machozi kwa wananchi ambao wao wenyewe jamaa zao au mazao yao yameharibika au kudhuriwa na wanyamapori. Kufuatia mwongozo huo mwezi Julai, 2010 wakulima 514 walilipwa fidia ya jumla ya shilingi milioni 51.4 kama kifuta jasho kwa kiwango cha Sh.100,000/= kwa kila mkulima. Aidha, jumla ya Sh. 400,000/= zililipwa kwa ndugu wa familia mbili za marehemu wawili waliouawa na ndovu.

Mheshimiwa Spika, Wizara yangu itaendelea kushirikiana na wakulima, Serikali za Vijiji na Wizara ya Maliasili na Utalii kuhakikisha kwamba wananchi na mazao yao wanalindwa dhidi ya wanyama wote waharibifu. Aidha, wananchi watafundishwa mbinu shirikishi za kujikinga na madhara ya wanyama hao. Kwa niaba ya Serikali natoa pole kwa Mheshimiwa Mbunge, ndugu jamaa na marafiki wa wananchi ambao jamaa zao waliuawa na wanyama hao.

**SPIKA:** Ahsante. Tembo na Ndovu ni hao hao. *(Makofi)*

**MHE. JOSEPH ROMAN SELASINI:** Mheshimiwa Spika, kwa kuwa tembo wanaendelea kuingia kwa makundi katika Wilaya ya Rombo na wiki iliyopita zaidi ya tembo 300 walivamia Kata ya Mahida, Mamsela, Ngoyoni na kuleta uharibifu mkubwa na madhara kwa mwanafunzi ambaye sasa amelazwa katika hospitali ya Mawenzi Mjini Moshi na kwa kuwa kituo anachosema Waziri ukweli bado hakijakamilika hakuna askari, hakuna gari kama taarifa ilivyotolewa.

(a) Je, Serikali sasa ambayo wananchi wa Rombo wanaamini kabisa kwamba itawasaidia iko tayari kuharakisha kukamilika kwa kituo hiki kupeleka askari wa kutosha pamoja na gari ili kusaidia katika kuhakikisha kwamba tatizo hili limeleta unafuu kwa wananchi?

(b) Mheshimiwa Spika, kulingana na utaratibu wa fidia wanaofidiwa ni wale ambao mashamba yao yameharibiwa kwa ukubwa wa zaidi ya eka moja. Lakini Wilaya ya Rombo kutokana na uhaba wa ardhi wananchi wengi mashamba yao ni robo eka na nusu eka ambao hawakupata kuingia katika utaratibu huu wa fidia. Wale waliopata maafa kiwango chao cha fidia inaonekana ni kidogo sana kulingana na uhalisia wa mambo. Je, Serikali iko tayari kuangalia uwezekano wa kuwafidia wananchi hawa kulingana na hali halisi ya uharibifu unaotokea?

Mheshimiwa Spika, kama nilivyojibu katika jibu la msingi, ni kweli kabisa kwamba barabara hii yenye urefu wa kilomita 109 ni muhimu katika kuendeleza maeneo hayo. Lakini pia natambua kuwa maeneo hayo mvua zinanyesha sana na kutokana na hayo ndiyo maana tunafanya kwanza *feasibility study* na baada ya *feasibility study* tutafanya *detail design* na baadaye ndipo tutatangaza tenda kwa ajili ya *construction* yenyewe katika eneo lote. Kwa hiyo *feasibility study* itaangalia pia uwezekano kwa namna gani barabara hiyo inaweza ikatengenezwa au ikajengwa hata kwa nyakati za mvua kwa sababu ni kawaida hata kwenye nchi nyingine ambazo kila siku mvua zinanyesha lakini barabara za lami zinatengenezwa.

Kwa hiyo kuwa na mvua zinanyesha haizuii barabara kutengenezwa kwa kiwango cha lami. *Actually* inakuwa vizuri zaidi hata kwa lami yenyewe kukomaa mapema wakati inamwagiwa maji na hasa kama wanatumia utaalam wa pozolana au *cement stabilization* katika ujenzi wa barabara.

Kwa hiyo, hayo yote Mheshimiwa yatazingatiwa. Lakini pia si vyema kumtumia mkandarasi aliyeko kule kuanza kufanya *feasibility stud*y kwa sababu *feasibility study* tutafuata taratibu zote za *Procurement Act* kwa kutangaza tenda, lakini hatazuiliwa mkandarasi aliyeko kule naye kuomba kazi hiyo ya kufanya *feasibility study* kama anaweza atafanya hivyo na kandarasi aliyeko kule ilikuwa ni kampuni moja inaitwa *China Civil Engineering Construction.*

Na. 24

**Kuanza kwa Ujenzi wa Barabara ya**
**Geita-Kharumwa Hadi Kahama**

**MHE. HUSSEIN NASSOR AMAR** aliuliza:-

Barabara ya kutoka Geita kupitia Kharumwa hadi Kahama na barabara ya kutoka Kharumwa hadi Busisi, Kahama na barabara ya kutoka Karumwa hadi Busisi, Ferry ni muhimu sana katika uchumi na maendeleo ya Jimbo la Nyang'hwale hata Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete aliahidi kujengwa barabara hiyo kwa kiwango cha lami:-

(a) Je, ni lini upembuzi yakinifu utaanza?

(b) Je, ni lini mradi huo utaanza?

**WAZIRI WA UJENZI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Hussein Nassor Amar, Mbunge wa Nyang'hwale lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, barabara ya Geita – Kharumwa na Kharumwa hadi Kahama na barabara nyingine ya kutoka Kharumwa hadi Busisi, *Ferry* ni barabara za Mkoa zinazohudumiwa na Wizara yangu kupitia Wakala wa Barabara wa Mkoa wa Mwanza.

Mheshimiwa Spika, utekelezaji wa mradi huu utafanywa kwa awamu tatu kuanzia na upembuzi yakinifu na usanifu wa awali, usanifu wa kina na uandaaji wa nyaraka za zabuni na hatimaye ujenzi wa barabara yenyewe.

Kazi ya upembuzi yakinifu wa barabara hii inatarajiwa kuanza katika mwaka wa fedha wa 2011/2012. Hata hivyo, katika mwaka wa fedha wa 2010/2011 jumla ya shilingi milioni 164.13 zilitengwa kwa ajili ya matengenezo ya kawaida ya barabara hizo.

Wakati jitihada za kutafuta fedha kwa ajili ya ujenzi kwa kiwango cha lami zikiendelea Serikali itaendelea kuzifanyia matengenezo ya kawaida barabara ya Geita – Kharumwa na Kharumwa hadi Busisi *Ferry* ili zikiendelea kupitika katika majira yote ya mwaka.

**MHE. HUSSEIN N. AMAR:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa majibu mazuri ya Waziri wa Ujenzi lakini nina maswali mawili ya nyongeza.

Moja, je, Serikali inachukua hatua gani kutoa maelekezo kwa wananchi wa Jimbo la Nyangh'wale sehemu ambayo barabara itapitishwa ili wananchi wasiendelee kujenga nyumba ili kuepusha hasara ambayo inaweza kuja kupatikana wakati wa ujenzi? *(Makofi)*

Pili, kwa kuwa Jimbo la Nyangh'wale limo katika Wilaya 18 mpya na kutangazwa kwamba Wilaya mpya Makao Makuu yake yatakuwa Kharumwa, ni hatua gani ambazo zimechukuliwa ili kuwaelimisha wananchi wasiweze kuendelea na ujenzi wa nyumba ili michoro ya barabara iweze kuandaliwa na wananchi waweze kuandaa majengo yao ili kuepusha hasara ya ubomoaji utakaoweza kujitokeza baadaye?

**WAZIRI WA UJENZI :** Mheshimiwa Spika, maelekezo ambayo naweza kuyatoa kwa wananchi wa Nyangh'wale na wananchi wote wa Tanzania ni kwamba wazingatie Sheria ya Barabara. Sheria ya Barabara ya mwaka 1967 ambayo imeanza kutumika kwa muda mrefu inayotokana na *Cap.* Na. 167 na ambayo ilifanyiwa mabadiliko kupitia Sheria Na. 13 ya Barabara ya mwaka 2007 inazungumzia kuhusu upana wa barabara. Upana wa barabara kwa Sheria ile ya *Cap.* No.167 ni mita 22.5 kila upande wa barabara ukitoa tofauti ya Dar es Salaam. Lakini maeneo mengine yote ya Tanzania upana ulikuwa hivyo lakini ukafanyiwa mabadiliko kupitia *Road Act No.* 13 ya mwaka 2007 na sasa upana wa barabara umekuwa mita 30 kila upande.

Kwa wale ambao wataguswa waliokuwa nje ya mita 22.5 ya Sheria ya zamani kwa mabadiliko ya sasa hivi wale wana haki ya kulipwa fidia kwa mujibu wa Sheria hiyo. Lakini pia kwa mujibu wa Sheria zingine ikiwepo Sheria Namba 4 na Namba 5 ya mwaka 1999 ya Sheria ya Ardhi na mabadiliko yake ya Sheria Namba 6 na Namba 7 ya mwaka 2007.

Kwa Dar es Salaam upana wa barabara ni tofauti. Kwa sheria hiyo hiyo ukitoka *Askari Monument* mpaka Ubungo upana ni mita 22.5 ambazo zimeongezwa ambazo ni futi 30. Baada ya Ubungo upana wa barabara ni futi 300 kila upande mpaka kwa kilometa 10, baada ya hapo mpaka kwenye daraja la Kibaha upana wa barabara unaongezeka kuwa futi 400 kila upande. Baada ya Kibaha mpaka kwenye Daraja lile la reli upana wa barabara unashuka tena unakuwa futi 75, kwa sasa hivi ni mita 22 ambazo zimefanyiwa *amendment* kwa Sheria Na. 13 kuwa mita 30, pale kwenye daraja la reli upana tena unaongezeka futi 300. Kwa hiyo ni matumaini yangu wananchi wa Nyangh'wale watazingatia Sheria hii na kwa sababu imepitishwa na Bunge na inatumika. Lakini pia katika kuzingatia utawala wa Sheria.

Na. 25

**Dawa za Kupunguza makali ya Virusi vya UKIMWI**

**MHE. LUCY F. OWENYA** aliuliza:-

Makali ya virusi vya UKIMWI yamepungua kwa kiasi kikubwa ikiwa ni pamoja na kutumika dawa za kupunguza makali ya virusi vya UKIMWI.

Je, ni vigezo gani vinatumika kuchagua dawa za kumpa aliyefikia muda wa kuanza kutumika dawa za kupunguza makali ya virusi vya UKIMWI?

**NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Lucy Fidelis Owenya, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, vigezo vinavyotumika katika kuchagua dawa za kumpa mgonjwa anayestahili kuanza kutumia dawa za kupunguza makali ya virusi vya UKIMWI ni vile vilivyoainishwa kwenye mwongozo wa Kitaifa wa matumizi ya dawa za *ARV's* ambao umetokana na mapendekezo ya Shirika la Afya Duniani. Vigezo hivyo ni kama ifuatavyo:-

(i) Dalili za UKIMWI na magonjwa nyemelezi;

(ii) Ushahidi wa kuharibiwa kwa mfumo wa kinga, ikiwa ni pamoja na wale wenye kinga za chini ya *CD4 200;*na

(iii) Utayari wa mwathirika kutumika dawa za kupunguza makali ya VVU na kufuata masharti yote. Hii ni kwa sababu mgonjwa akianza kutumia dawa hizi hatakiwi kuziacha katika kipindi chote cha maisha yake.

Mheshimiwa Spika, pamoja na vigezo hivyo hapo juu, vile vile mgonjwa hupimwa kuangaliwa kiasi cha damu alichonacho na picha halisi na damu yake kwani kuna baadhi ya dawa mfano *Zidovudine* ambazo mgonjwa mwenye damu kidogo hapaswi kupewa. Pia wagonjwa hupimwa ufanyaji kazi wa ini ili kuona kama halina tatizo lolote kwa kuwa dawa kama *Nevirapine* hazipaswi kupewa wagonjwa wenye matatizo ya ini. Hali kadhalika, wagonjwa wanaokuja kuanza dawa wakiwa na magonjwa mengine nyemelezi kama kifua kikuu hawapaswi kupewa dawa za *ARV's* aina ya *Nevirapine* kwa kuwa hupunguza uwezo wa dawa za kutibu kifua kikuu.

Mheshimiwa Spika, naomba kulitaarifu Bunge lako Tukufu na wananchi kwamba sasa dawa za kupunguza makali ya UKIMWI zinatolewa bure na zinapatikana katika vituo vyote vilivyopitishwa kwa ajili ya kutoa huduma hizo.

**MHE. LUCY F. OWENYA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili madogo ya nyongeza. Namshukuru Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri na ametueleza kwamba kigezo kimojawapo ni pamoja na kucheki damu ya wagonjwa na kucheki kama ini linafanya kazi.

Mheshimiwa Spika, katika makala tofauti zinazohusu masuala ya VVU wamekuwa wakiandika kwamba kuna usugu wa virusi vya UKIMWI yaani VVU kwa watumiaji wa *ARV*. Je, Serikali haioni kama kuna umuhimu wa kuwapima watu wanaoanza *ARV* kwa mara ya kwanza ili kuangalia *sensitivity* ya dawa za *ARV* ili kupoteza ukuaji wa usugu wa dawa hizo?

Swali la pili, ningependa Mheshimiwa Spika, Naibu Waziri atueleze. Je, usugu wa virusi vya UKIMWI yaani VVU ukoje katika nchi yetu ya Tanzania ?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri tunategemea majibu yatakuwa mafupi sana.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII:** Mheshimiwa Spika, usugu wa *ARV's* kwa wagonjwa ambao wanaanza matibabu naomba nilijulishe Bunge lako Tukufu kwamba wagonjwa wengi wanaokuja kupimwa katika vituo vyetu wanakuwa hawajawahi kutumia hizo dawa. Kwa hiyo kama mgonjwa hajawahi kutumika hizo dawa hawezi akawa na usugu wa dawa. Tunafanya *test* ya usugu wa dawa kwa sababu mgonjwa anapoanza kutibiwa tunapima *CD4 count.* Baada ya kipindi cha wiki sita tunaendelea tena kuangalia kwamba huyu mgonjwa anaendelea vipi, maendeleo yakiwa mazuri maana yake *CD4 count* yake inakwenda juu. Idadi ya zile *cells* za *CD4* inaongezeka. Kama tunaona kwamba hali ya mgonjwa hakuna kupunguka kwa magonjwa nyemelezi, hakuna kuongezeka kwa *CD4* sasa hapo ndiyo Daktari anayemtibu anakuwa na sababu ya kuweza kufuatilia usugu wa hiyo dawa kwa sababu tunafanya *test* za usugu kwenye vituo vichache sana na ni gharama kubwa. Kwa hiyo, tunafanya pale ambapo tunaona kwamba mgonjwa haendelei vizuri.

Swali la pili, ameuliza kwamba hali halisi hapa Tanzania usugu wa *ARV* ukoje. Ningependa kumweleza Mheshimiwa Mbunge kwamba, katika hali halisi hapa Tanzania bado hatujawa na tatizo kubwa la usugu wa dawa kwa sababu wagonjwa wetu wanaopewa dawa wanakuwa wanapata ushauri nasaha mzuri na wengi wao wanatumia dawa vizuri, hivyo usugu wa virusi vya UKIMWI kwa hizi dawa unakuwa ni mchache sana.

Tatizo kubwa tulilo nalo ni wagonjwa kupata *reaction* ya dawa. Ndiyo inakuja sasa kwamba inabidi tuondoke kwenye *line* ya kwanza ya dawa kwenda kwenye line nyingine kwa sababu mgonjwa mwili wake umeshindwa kupatana na dawa katika *line* ya kwanza, dawa ambazo tunazinunua kwa bei rahisi. Inapofikia hapo basi ndiyo tunabadilisha tena zile dawa ambazo mgonjwa anapewa na siyo kwa sababu ya usugu.

**SPIKA:** Tayari ushauri nasaha huo. Tunaendelea na swali linalofuata.

Na. 26

**Hitaji la Wataalam Katika Zahanati kwa Kila Kijiji**

**MHE. ANNE K. MALECELA** aliuliza:-

Ilani ya uchaguzi imeweka bayana kuwa kila kijiji kiwe na zahanati.

Je, Serikali inaweza kuthibitisha kwamba zahanati hizo zitapata watalam husika ikiwa ni pamoja na Wakunga mara tu zitakapokamilika?

**NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Anne Kilango Malecela, Mbunge wa Same Mashariki, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kwamba katika Ilani ya Chama cha Mapinduzi ya Uchaguzi ya mwaka 2010-2015 imeweka bayana kuwa kila kijiji kiwe na Zahanati ifikapo mwaka 2015. Serikali inaendelea kutekeleza Mpango wa Maendeleo ya Afya ya Msingi (MMAM) wa 2007-2017 na madhumuni ya mpango huu ni kusogeza huduma za afya kwa wananchi kwa kuwa na Zahanati katika kila kijiji na Kituo cha Afya kwa kila Kata. Utekelezaji wa Mpango huu kwa maana ya ujenzi wa Zahanati unahusisha TAMISEMI kupitia Halmashauri za Wilaya. Sekretarieti za Mikoa, Serikali za Vijiji na wananchi kwa ujumla. Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii ina jukumu la kuhakikisha upatikanaji wa wataalam wa afya katika vituo vilivyopo na vinavyojengwa. Hatua zinazochukuliwa na Wizara yangu ili kuhakikisha kwamba wataalam wanapatikana ni kama ifuatavyo:-

(1) Kudurusu mitaala ya kufundishia wauguzi ngazi ya cheti na stashahada na kufupisha muda wa masomo kwa kozi ya stashahada ya Uuguzi kutoka miaka

minne hadi mitatu na ngazi ya cheti cha uuguzi kutoka miaka mitatu hadi miwili bila kuathiri kiwango cha elimu. Lengo ni kuhakikisha wataalam hawa muhimu wanapatikana kwa uharaka zaidi.

(2) Kufungua vyuo vitatu vya Nachingwea, Nzega na Kibondo vilivyokuwa vimefungwa ambavyo sasa vinatoa mafunzo ya uuguzi na kufungua vyuo vipya vya uuguzi vya Lugala, Mbalizi, Murungwanza, Berega na Bulongwa.

(3) Vyuo 28 vya ngazi ya cheti vilivyokuwa vinaendesha mafunzo ya kujiendeleza *(upgrading)* vimeongezewa jukumu la kutoa mafunzo kwa wauguzi watarajali *(pre-service).*

(4) Kurejeshwa upya kwa kada za matabibu wasaidizi *(Clinical Assistants).* Naomba nifafanue kwamba *clinical assistants'* zamani walikuwa wanaitwa Waganga Wasaidizi wa Vijijini au *Rural Medical Aids* na wauguzi wasaidizi ambazo awali zilikuwa zimefutwa.

Mheshimiwa Spika, kufuatia utekelezaji wa mpango huu na kwa kuzingatia ongezeko la idadi ya wadahiliwa wa kada zote za utabibu na uuguzi ngazi ya cheti na stashahada wanaojiunga na vyuo vya afya kila mwaka, ni matarajio yetu kuwa hadi kufikia mwaka 2017 idadi ya wataalam wa afya wakiwemo wauguzi katika soko la ajira itaongezeka na hivyo kurahisisha upatikanaji wao katika vituo mbalimbali vya kutolea huduma ikiwa ni pamoja na Zahanati mpya zinazojengwa.

Hata hivyo, kutokana na sera ya soko huria, changamoto tuliyonayo ni kwamba wataalam wanaozalishwa siyo lazima wafanye kazi katika vituo vya Serikali kwa kuwa wanaweza kuajiriwa na sekta binafsi.

Mheshimiwa Spika, naomba nitumie fursa hii kuzihamasisha sekta binafsi ziongeze juhudi za kutoa mafunzo kwa kuongeza idadi ya udahili ili kuchangia ongezeko la wataalam wanaohitajika katika utekelezaji wa mpango huu.

**MHE. ANNE K. MALECELA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru majibu ya Serikali lakini naomba niulize maswali mawili madogo ya nyongeza kwa sababu napata tabu kidogo.

Mheshimiwa Spika, Jimbo langu la Same Mashariki lina sura mbili, tambarare na milimani na wananchi wanaoishi milimani ndiyo wengi zaidi ni Kata 10. Nina vituo vya afya viwili tu. Kituo cha afya cha Kata ya Vumta ni kimoja na kinahudumia karibu Kata zote 10, lakini hakina gari la wagonjwa. Je, Serikali haioni kwamba ni muhimu na ichukue hatua ya dharura sana kunipelekea gari la wagonjwa kwa sababu wanawake wengi wanapoteza maisha yao kwa sababu hakuna gari la kuwakimbiza kuwapeleka katika hospitali ya Wilaya wanaposhindwa kujifungua katika njia ya kawaida?

Swali la pili, Mheshimiwa Spika, naomba kuuliza hivi sasa wananchi wa Tanzania wanapata kazi nyingi sana za kuchangia maendeleo yao wenyewe. Sasa hivi

wanajenga Zahanati, wanajenga na vituo vya afya kila Kata. Je, Serikali haiwezi kufanya kama wanavyofanya Wizara ya Elimu kwamba Serikali nayo ichangie kama vile MMEM na MMES kwenye upande wa kujenga madarasa?

**NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII:** Mheshimiwa Spika, swali la kwanza, Mheshimiwa Mbunge ameeleza kwamba ana vituo viwili tu vya afya katika eneo lake na anasema kwamba kutokana na wingi wa wagonjwa na kutokuwepo kwa gari la wagonjwa, wagonjwa wetu hawapati huduma zinazostahili hasa wanapopata rufaa. Naomba kumjulisha Mheshimiwa Mbunge na Bunge lako Tukufu kwamba katika mpango wa MMAM tuna mpango wa kuhakikisha kwamba kwenye kila kituo cha afya mpaka ifikapo mwaka 2015 kunakuwepo na *theatre* ya kuweza kutoa *emergency* hususan *section* ya akina mama wajawazito ili tuweze kupunguza vifo vya akinamama wajawazito na watoto wachanga. Iko kwenye mpango wetu na ndiyo sababu tumefungua vituo, tumeongeza udahili wa wanafunzi wa *Clinical Officers* pamoja na *Assistant Medical Officers* ili tuweze kupata *Assistant Medical Officers* kwenye hivi vituo watakaoweza kufanya kazi nzuri ya kuokoa maisha ya akinamama wa Tanzania na wagonjwa wengine.

La pili, ili kuweza kurahisisha ile kazi ya *referral*, wagonjwa waweze kupelekwa kwa matibabu ya *speciality* katika hospitali za Wilaya, Wizara imeagiza pikipiki ambazo zitakuwa ni pikipiki za *ambulance*, tutazipeleka katika vituo vya afya ambavyo viko vijijini. Kwa hiyo Mheshimiwa Mbunge, naomba nikuambie kwamba awamu ya kwanza itafika kuanzia mwezi Machi na naomba nikuhakikishie kwamba vituo vyako vitakuwa ni vimojawapo miongoni mwa vituo ambavyo vitapata hizi *ambulance* za pikipiki.

Mheshimiwa Spika, swali la pili, Mheshimiwa Mbunge ameuliza kwamba, kwa nini Serikali isitoe ruzuku ya kumalizia ujenzi wa Zahanati na vituo vya afya kama inavyotoa ruzuku katika ujenzi wa mashule. Naomba niseme kwamba katika awamu hii ya kuboresha sekta ya Afya kupitia Mpango wa MMAM na kupitia kwenye Serikali za Mitaa, Halmashauri, Serikali iko tayari kushirikiana na wananchi kuwaongezea uwezekaji wa Zahanati pale ambapo watakuwa wamejenga na wamejenga kwa kufuatana na *plan* ambazo Wizara ya Afya imezitoa na kwa kushirikiana na uongozi wa Afya pamoja na Kamati za Afya katika Wilaya zao.

Mheshimiwa Spika, hilo nafikiri lipo, ni sehemu ya kuboresha kupitia Mpango wa MMAM. *(Makofi)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge muda wa maswali umekwisha. Nasikitika kwamba maswali ya Wizara ya Uchukuzi mawili hayakujibiwa na naomba itumike nafasi hiyo kwa Wizara hiyo ku-*edit* maswali yake kwa sababu majibu ni marefu mno. Kwa hiyo bado nasisitiza Mawaziri kupunguza urefu wa majibu na nyie Waheshimiwa Wabunge mpunguze maswali ya nyongeza ambayo yanakuwa ni hotuba, matokeo yake hatufiki kila mahali. Hiki kipindi siyo cha hotuba, ni maswali na majibu. Naomba tuzingatie hili. Baadaye tutakuwa tunawaambiwa kabisa. Nimewaacha siku mbili kwa sababu ya ugeni wenu, lakini naendelea kuwaambia acheni kuhutubia watu kwenye kipindi cha maswali. Uliza tu maswali yako.

Sasa baada ya kusema hayo. Nina matangazo machache. Kwanza kabisa tunakusudia kusitisha shughuli za Bunge mpaka saa 11.00 ili kipindi hiki kitumike kwa kufanya uchaguzi wa Wenyeviti wa Kamati mbalimbali. Kwa hiyo, Kamati ya Fedha na Uchumi itakwenda kukaa, natangaza nafasi ya kufanyia mikutano hiyo. Kamati ya Fedha na Uchumi watakwenda *CDA*, mtaongozwa na Katibu huko. Kamati ya Hesabu za Serikali itakwenda Ukumbi wa Msekwa B. Kamati ya Hesabu za Serikali za Mitaa watakwenda Manispaa. Kamati za Hesabu za Mashirika ya Umma watakwenda kwenye ukumbi wa *LAPF*. Kamati ya Sheria Ndogo itakwenda chumba 219, hapa hapa Jengo la Utawala. Kamati ya Nje, Ulinzi na Usalama watakwenda chumba namba 227. Kamati ya Huduma za Jamii itakwenda *VETA.*

Kamati ya Maendeleo ya Jamii itakwenda Dodoma Hoteli. Kamati ya Ardhi, Maliasili na Mazingira watakwenda Dodoma Hoteli. Kamati ya Kilimo, Mifugo na Maji watakwenda Ukumbi wa Msekwa A. Kamati ya Nishati na Madini watakwenda *Basement* hapa chini. Kamati ya Viwanda na Biashara watakwenda *Basement* hapa chini. Kamati ya Miundombinu watakwenda chumba 231. Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala watakwenda *Basement.* Kamati ambazo siyo Kamati maana yake zitaingiliana kwa sababu Wajumbe wote wanapaswa kuwa kwenye Kamati hizi lakini kuna Kamati zina nyongeza, Wabunge wake wana Kamati mbilimbili, lakini siyo za msingi. Siyo Kamati zile Mama. Kamati ya Masuala ya Ukimwi watakwenda chumba 231. Kamati ya Haki, Maadili na Madaraka ya Bunge, Ukumbi Na. 227.

Kwa hiyo Waheshimiwa Wabunge, sasa tunasema Kamati hizi nilizozitaja za mwanzo zinakutana kuanzia saa 5.30. Halafu Kamati zile nilizotaja Kamati ya Sheria Ndogo, Kamati ya Haki na Maadili na Kamati ya Ukimwi zitakutana saa 7.00. Hizo *time* naomba mzingatie kwa sababu msigonganishwe bila sababu. Maana yake ni kwamba wale watakaokuwa wamechaguliwa Wenyeviti tutakuwa na Kamati ya Uongozi saa 8.30 maana ni wale Wenyeviti watakaokuwa wamechaguliwa, Mheshimiwa Spika, Naibu Spika, Kiongozi wa Shughuli za Serikali Bungeni, Kiongozi wa Kambi ya Upinzani, Mwanasheria Mkuu, na Wenyeviti tutakutana nimesema saa 8.30 kwenye *Board Room* ya Spika.

Halafu tarehe 14 tutafanya uchaguzi wa Tume za Huduma za Bunge, yenyewe ni Wajumbe watano. Uchaguzi wa Mjumbe wa APRM *African Pie Review Mechanism* mjumbe mmoja, tutafanya tarehe 14. Tarehe 15 tutachagua wale wawakilishi kwenye vyuo vikuu. Sasa fomu za kugombea chaguzi hizi zinatolewa Ofisini kwa Katibu wa Bunge. Zinatolewa kuanzia leo na zitarejeshwa saa 10.00 jioni siku ya Jumatatu tarehe 14. Kwa hiyo wale wanaopenda kugombea vitu hivi waende wakachukue fomu, zitaanza kurejeshwa saa 10.00 siku ya Jumapili na Jumatatu. Lakini leo mnaanza kwenda kuchukua hizo fomu kwa wale wanaotaka kugombea.

Pia nina tangazo lingine hapa linatoka kwa Katibu wa Chama cha Mapinduzi, Mheshimiwa Jenista Mhagama, anasema niwatangazie Wabunge wa CCM kuwepo kwa kikao cha dharura leo hii mara baada ya kutangaza hapa katika Ukumbi wa Msekwa, yaani mkitoka hapa muende Ukumbi wa Msekwa. Kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge napenda kusitisha shughuli hizi mpaka saa 11.00 jioni.

*(Saa 4.48 Asubuhi Bunge lilistishwa mpaka saa 11.00 jioni)*
*(Saa 11.00 jioni Bunge lilirudia)*

*Hapa Naibu Spika (Mhe. Job Y. Ndugai) Alikalia Kiti*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, mkiangalia *Order Paper* zenu mtaona kwamba kuna ajenda moja ambayo itabidi tuiruke, nayo ni ya uchaguzi wa Wenyeviti wa Bunge, ambayo tutaifanya wakati mwingine kadri tutakavyotaarifiwa. Tutaendelea na hoja ambayo imeshasomwa na Katibu ya kuhusiana na kujadili hotuba ya Rais. Makatibu wangu wamechanganya kidogo orodha ya wachangiaji, ngoja wa-*sort out* kidogo.

Waheshimiwa Wabunge, naomba kuwataarifu kwamba Kiongozi wa Serikali Bungeni, kwa sasa ni Mheshimiwa Samuel Sitta, kwani Mheshimiwa Waziri Mkuu amesafiri kikazi Dar-es-Salaam na atarejea leo jioni. Naomba tutambue uwepo wa Mheshimiwa Samuel Sitta. Ahsante sana. *(Makofi)*

Basi katika orodha yangu, tunaanza na Mheshimiwa Maida Abdalla, atafuatiwa na Mheshimiwa Martha…

**WABUNGE FULANI:** Mheshimiwa Maida ameshachangia.

**NAIBU SPIKA:** Eeh, ameshachangia! Makatibu wangu mmefanyaje hii kazi? Si hapa mmekata?

Basi ngoja kazi hii niifanye mimi mwenyewe. Mheshimiwa Martha Mlata amechangia au bado?

**WABUNGE FULANI:** Bado.

**NAIBU SPIKA:** Na hayupo? Mheshimiwa Selemani Zedi?

**MHE. SELEMANI J. ZEDI:** Mheshimiwa Naibu Spika, bado.

**NAIBU SPIKA:** Basi, tumuombe Mheshimiwa Selemani Zedi aendelee, Mheshimiwa Herbert Mntangi ajiandae na tutaendelea kuweka vizuri orodha yetu. Mheshimiwa Selemani.

**MHE. SELEMANI J. ZEDI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kupata fursa hii kuchangia katika Bunge hili Tukufu, ikiwa ni mara ya kwanza kuchangia. Naomba nichukue fursa hii niwashukuru kwa dhati wananchi wa Jimbo la Bukene kwa kuniamini na kunichagua kuwa mwakilishi wao katika Bunge hili la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hotuba ya Rais aliyoitoa wakati akizindua Bunge hili la 10 ilikuwa na vipaumbele 13. Ukivitazama kwa makini vipaumbele vile 13 utagundua

kwamba vime-*cover* mambo yote ya muhimu ambayo yakifanyiwa kazi ipasavyo, kwa kweli nchi yetu katika kipindi hiki cha miaka mitano itapiga hatua ambayo wananchi wanaitarajia.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nichangie na katika kuchangia nijikite kidogo kwenye suala la upungufu wa chakula. Juzi wakati tunapata *briefing,* Jumatatu iliyopita tarehe 07/02/2011 tulipata fursa ya kupata ripoti ya Waziri wa Kilimo na Chakula. Katika ripoti hiyo Waziri wa Kilimo na Chakula aliainisha mikoa 13 na katika mikoa hiyo aliainisha Halmashauri 36 ambazo Wizara ya Kilimo na Chakula baada ya kufanya tathmini imeziainisha kwamba zina upungufu mkubwa wa chakula na hivyo kuna hatari kubwa ya njaa. Sasa katika Halmashauri hizo ipo Halmashauri ya Wilaya ya Nzega ambayo ina-*cover* Jimbo langu la Bukene. Sasa taarifa ile inaonesha kwamba Nzega kama Wilaya ina watu 545,000 na ripoti hiyo inaonesha kuwa ni watu 14,000 tu ndio wanaokabiliwa na njaa, ambao ni kama asilimia tatu ya wananchi wa Wilaya ya Nzega.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilikuwa huko Jimboni juzi, kwa kweli hali halisi kule, nadhani inawezekana wakati tathmini hii inafanywa labda mwezi mmoja au miezi miwili nyuma hali ilikuwa hivyo lakini hadi sasa hivi tunavyoongea sikubaliani na ile ripoti kwamba ni asilimia tatu tu yaani watu 14,000 tu kati ya watu 545,000 wa Wilaya ya Nzega ndio wanaokabiliwa na njaa. Kilichopo ni kwamba hali kwa kweli sio nzuri, wananchi wa Nzega, wananchi wa Jimbo langu la Bukene tulijiandaa tukalima, mvua kidogo ikanyesha tukapanda lakini baada ya hapo ikakatika kabisa. Kwa hiyo, hali kwa sasa hivi inatisha kabisa.

Mheshimiwa Naibu Spika, naishauri Serikali kwamba suala la upungufu wa chakula, suala la njaa liwe *treated* kama suala la dharura, maafa. Kwa hiyo Idara ya Maafa iliyo chini ya Waziri Mkuu inapo *handle issue* ya njaa iwe *treated* kama maafa kweli na wala kusiwe na urasimu kama vile unashughulikia jambo la kawaida. Kwa hiyo, njaa ni janga, njaa ni maafa, kwa sababu wananchi wa Nzega wa Jimbo la Bukene, hali hii ya njaa hawakuitarajia na wala hawakuitaka. Walijiandaa, wamelima, wamepanda, mvua imekuja kidogo lakini baadaye imekata kabisa mpaka sasa. Kwa hiyo, ni janga ambalo limewapata bila wao kutarajia hawakuwa wamejipanga; kwa hiyo, ni maafa. Kwa hiyo, Idara ya Maafa ya Waziri Mkuu, nasisitiza na naomba kwamba ilichukulie na hii sio kwa Nzega na Bukene bali kwa Halmashauri zote 36 ambazo zimeainishwa na tathmini ya Wizara ya Chakula na Kilimo kwamba zina njaa basi Idara ya Maafa chini ya Waziri Mkuu iifanyie kazi kama maafa na wala sio jambo la kawaida ambalo linashughulikiwa kwa utaratibu wa kawaida.

*(Hapa kengele ililia)*

**MHE. SELEMANI J. ZEDI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naona kengele ya kwanza imelia. Lakini nashukuru kupata fursa hii, mchango wangu ni huo, nasisitiza kwamba njaa ishughulikiwe kama maafa, isishughulikiwe kwa utaratibu wa kawaida. Kwa hiyo, taratibu za kuhakikisha kwamba wananchi wa Nzega na Jimbo la Bukene wanapelekewa chakula hata kama wale ambao wameainishwa 14,000 sasa hivi taratibu za kuwapelekea chakula zifanyike wakati tathmini nyingine zikiendelea. Kwa sababu,

naamini Wilaya ya Nzega watu wanaokabiliwa na njaa kuanzia sasa hivi ni zaidi ya hiyo asilimia tatu, zaidi ya 50%.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru na naunga hoja mkono. Naomba kuwasilisha.

**MHE. MWIGULU L.N. MADELU:** Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote niwashukuru sana wananchi wa Jimbo la Iramba Magharibi kwa kunichagua kuwa mwakilishi wao na pili nikushukuru kwa nafasi hii. Jambo lingine la katika hotuba ya Mheshimiwa Rais, kama nafasi itaruhusu naomba nichangie kwenye elimu pamoja na suala la uchumi. Waheshimiwa Wabunge na Watanzania kwa ujumla, naomba mnisikilize kwa makini katika suala hili la elimu ili msije mkatafsiri tofauti.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kuanzia niipongeze Serikali ya Awamu ya Nne kwa kufanikisha suala zima la kushughulikia shule za sekondari za Kata. Hiyo ni sehemu ya mafanikio makubwa ambayo yameweka historia mpya katika nchi yetu ya kuwa na sekondari katika kila Kata. Lakini palipo na mafanikio matatizo huwa hayakosekani, kwa sababu ilikuwa ni lazima pawepo na pa kuanzia na hivyo ndivyo tulivyoanza. Naliangalia suala hili kwamba lilikuwa ni suala la mpito lakini tulilibeba kama suala la kawaida na hiyo ndiyo iliyoleta matokeo kuwa kama haya ambayo yametokea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tumeshuhudia katika sehemu nyingi kulikuwepo na upungufu mkubwa wa walimu na tumeshuhudia katika baadhi ya shule wanafunzi wanaripoti baada ya mhula wa kwanza kuwa umepita. Sasa suala la namna hii ni suala la maafa. Kwa hiyo, sababu kubwa iliyosababisha matokeo kuwa yale, naamini kwa upande wa upungufu wa walimu pamoja na upande wa *reporting.* Shule nyingine mwanafunzi hata ukichelewa wiki moja unakuwa umeshachelewa kwa kiwango kikubwa sana.

Sasa naishauri Wizara husika na Serikali kwa ujumla kutambua kwamba wazazi walituunga mkono kwa kiwango kikubwa sana katika ujenzi wa shule hizi na wanaendelea kutuunga mkono katika ujenzi wa vitu vingine vinavyohusisha kuchangia kama ilivyokuwa kwenye upande wa Sekondari, kwa mfano kwenye sekta ya afya. Sasa ili tusiwavunje moyo napendekeza kwa Wizara itambue kwamba Serikali ni lazima iwe *per-taker,* ni lazima na yenyewe ichukue sehemu katika matokeo na vilio vilivyowakumba wazazi wa watoto hawa waliomaliza mwaka huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Watanzania wa kawaida ninaowafahamu hawasomeshi kwa ziada, wanasomesha kwa kujibana, kwa hiyo, naomba Wizara ya Elimu iangalie uwezekano na kuchukulia kwamba hiki ni kipindi cha mpito, watoto waliomaliza mwaka huu wapewe fursa nyingine ya kufanya mtihani kwa sababu hawakuandaliwa katika miezi inayotakiwa. Wapewe fursa wafanye mtihani mwingine kwa gharama za Serikali, tukichukulia kwamba ni kipindi cha mpito.

Lakini vile vile tuangalie muda mwingine katika kipindi hiki suala la namna hiyo liweze kufanyika ili kuweza kuhakikisha kwamba tunawaunga mkono wazazi lakini vilevile na watoto na Walimu, maana hata watoto wenyewe wamefaulu. Kupata maksi

walizopata katika mazingira yale waliyokuwa wanasomea kwa kweli wamejitahidi na hata kuwa na Walimu wawili halafu watoto wafaulu kwa kiwango kile, ni kwamba wamejitahidi sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa katika mazingira yale yale napendekeza ufanyike utaratibu ambao ni wa dharura pia katika namna ya kupata walimu; tutaanza kutafuta wachawi, wengine watasema maslahi. Lakini nakumbuka hata Maprofesa wenye A nyingi sana walifundishwa na walimu ambao maslahi yalikuwa ni haya haya, wengine hata maslahi yameboreshwa lakini walikuwepo wa kutosha. Ikitokea vita huwa tunachukua hata mgambo hatuishii kuchukua wanajeshi tu. Sasa kwenye hili naomba Wizara husika itafute namna ambayo tunaweza tukapata watu ambao wanaweza kufanya kazi hiyo. Kwa mfano, katika hizi shule za Kata walimu ambao wamekuwa wakifundisha unakuta wengine wanajitolea, wamemaliza *form six.* Lakini wanajitolea *in an informal way*.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa Wizara na taasisi zinazohusika labda kwa kuwa zinafanya *admission* ya wanafunzi wengine wanaokwenda kwenye vyuo vya elimu wanakosa nafasi, ziwachukue wanafunzi wote wenye sifa kwa kuwafanyia *admission*, wakishawafanyia *admission* wasaini nao mkataba waende wakafundishe wakiwa wameshajihakikishia kwamba wanavyofundisha watapewa hela ya kujikimu lakini asilimia nyingine ni ada yao baada ya kuwa wameshafundisha kwa kipindi wakati Serikali inatumia utaratibu ule wa walimu ambao wanafundishwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni lazima hili jambo tulichukulie kwamba ni la mpito na jambo la mpito ni lazima tulibebe kwa muundo wa mpito. Lakini kwenye lilelile nilikuwa napendekeza kwamba hawa walimu ambao watakuwa wameshapelekwa kwenye hivyo vyuo kwa mkataba huo, watakuwa wameshapata motisha lakini vilevile tutakuwa tumepunguza wanafunzi ambao wana sifa lakini wamekosa nafasi za kwenda mashuleni.

**MHE. MWIGULU L.N. MADELU:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu naona kengele imeshagongwa, nikirejea kwenye lile suala la uchumi ambacho ni kipaumbele cha pili, mazingira ambayo Serikali ya Awamu ya Nne ilianzia kazi yanafanana kabisa na ya awamu hii kipindi cha pili. Kulikuwa na ukame mkubwa wa kiwango cha juu sana 2005/2006 na hiyo imejitokeza katika mwaka huu. Wakati ule Serikali ililisha watu zaidi ya milioni 3.7 naiomba Wizara husika isisubiri kuja kufanya tathmini, tathmini ni majibu kwamba mvua haijanyesha. Kwa hiyo, matarajio yake ni kwamba kutakuwepo na njaa na Serikali ijiandae kulisha watu zaidi ya milioni nne. Kufanya tathmini wakati watu wanasubiri chakula mtasababisha watoto wengine wazaliwe waitwe tathmini, wengine mbioni, wengine mchakato, kwa hiyo ni lazima tuwe tunapata majibu yanayohusu chakula, wakati watu wanahitaji chakula tuwe tulishayapata kabla ya hapo. Kwa hiyo, kwenye hili litakuwa ni jambo la msingi sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kulitokea na kupanda kwa bei, jambo hili viashiria vimeshaonesha kwamba tunakoelekea ni huko huko. Ukienda kwenye wazalishaji wa mafuta ukiangalia na maandamano yanayotokea katika nchi za Jumuiya

ya Kiarabu hayo yamesababisha mafuta yameanza kupanda na hiyo itakuja kwetu na bei za vitu na mfumuko wa bei utapanda sana. Kwa hiyo, kwenye hilo nalo kuliko kusubiri hali imeshakuwa mbaya nalo tuwe na maandalizi ili tuangalie jinsi ambavyo tutanusuru uchumi. Nimshukuru Rais, nimpongeze kwa jinsi alivyofanya wakati ule pamoja na Profesa…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa, kengele ya pili.

**MHE. MWIGULU L. NCHEMBA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MHE. DIANA M. CHILOLO:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda nichukue nafasi hii kukushukuru wewe binafsi kwa kunipa nafasi ya kuchangia. Nikupongeze pia kwa kuchaguliwa kuwa Naibu Spika.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitumie nafasi hii kutoa mchango wangu kupitia hotuba ya Mheshimiwa Rais, aliyohutubia kwa ajili ya kufungua Bunge mwaka jana 2010. Nampongeza sana Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, kwa jinsi alivyoitekeleza Ilani ya Uchaguzi vizuri kwa Awamu ya Nne. Utekelezaji wake mzuri ndio uliomfanya kurudishwa tena kwenye nafasi ya Urais, asingefanya vizuri Watanzania wasingemrudisha, Watanzania wana akili wana macho.

Mheshimiwa Naibu Spika, tuna kila sababu ya kumpongeza na kumuunga mkono kwa jitihada zake. Naamini kuwa madhali alifanya vizuri awamu yake ya kwanza nina hakika awamu hii ya pili atafanya vizuri zaidi. Vipaumbele vyote 13 nina hakika vitatekelezeka. Ametengeneza barabara, shule, zahanati, hospitali zimekarabatiwa, na vitu vingi Mheshimiwa Rais amevitekeleza. Mwenye macho haambiwi tazama, ndugu zangu tukubali tusikubali baba wa watu kafanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na mazuri yote lakini upungufu upo pia, lakini upungufu huo wanaomsababisha ni watendaji, watendaji wetu wako walioota viburi, wako wengine wanajiingiza kwenye siasa, wanasahau kabisa wajibu wao. Sasa naiomba Serikali iwatazame watumishi hawa kwa jicho kali ili wasimharibie Mheshimiwa Rais kwa kazi nzuri anazozifanya. Wapo waliokata tamaa kwa sababu zao wenyewe, wako wengine wazembe tu, kwa hiyo naiomba sana Serikali tusiwafumbie macho watumishi wa aina hii wataendelea kuichafua Serikali ya CCM wakati mipango yake ni mizuri na kazi zake ni nzuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda nizungumzie suala la elimu katika mambo ambayo Mheshimiwa ameyapa kipaumbele pamoja na suala la elimu, suala la elimu Mheshimiwa Rais amefanya kazi kubwa sana kujenga shule za sekondari, tulianza shule za msingi, tukaingia za sekondari na hatimaye tumejenga Chuo Kikuu kikubwa cha

Dodoma ambacho kinajulikana ulimwengu mzima, hivi hili jamani kweli si jambo la kujivunia? *(Makofi)*

Sasa udhaifu unaojitokeza lazima pia tuukemee kwa mfano, hili la wanafunzi wa kidato cha nne kufeli kwa kiwango kikubwa hata mimi nalilaani kabisa kabisa, linasikitisha kweli kweli, linatia huruma, wazazi wamejikusuru, wamejinyima wamewasomesha watoto hao, lakini kwa kiwango walichofeli walio wengi namna hii ni wazi kwamba udhaifu huo sio wa kwao lazima kuna dosari aidha, kwa watendaji ama Serikali yenyewe tumefanya uzembe fulani. Niendelee kuiomba Serikali kama walivyotangulia kusema wenzangu tuwahurumie wazazi hawa waliowasomesha watoto hawa wakijua kwamba, sasa darasa la kumi na mbili wamemaliza na kumbe wamefeli wote warudie darasa la kumi na mbili kwa gharama ya Serikali. *(Makofi)*

Tukifanya hivyo, tutakuwa tumewafuta machozi wazazi kwani sasa hivi wanahangaika wanatapatapa wanawaza watawafanya nini. Naamini Serikali ikifanya hivyo, wazazi watafarijika, watatambua ni kweli Serikali yao inawajali.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nizungumzie kuhusu suala zima la ajira kwa vijana, ndugu zangu Wabunge wenzangu migogoro hii inayopatikana kwenye vyuo vyetu hivi sioni kama wana sababu hasa ya msingi hapo walipo kwa sababu kama ni posho ya siku wanapata, kama ni mikopo ipo, ingawa kuna dosari ndogo ndogo. Nadhani vijana hawa kero yao ni mtazamo wa baadaye, suala kubwa la ajira wanaangalia hivi nikitoka hapa na *degree* yangu, *degree* hii nitaipeleka wapi? Ajira hana, mtaji hana wa kufanya shughuli yoyote ya kujiajiri. Ndugu zangu naiomba Serikali kwa hili ilitazame upya, ni kweli vijana hatujawatazama kwa jicho la huruma, tuwawekee mazingira ambayo yatawatia moyo kwamba, wakimaliza elimu za juu watapata ajira, ama watajiajiri, tukiwawekea mazingira mazuri naamini hata hii migogoro vyuoni itapungua. Migogoro inajitokeza tu kwa sababu ya vijana kukata tamaa kutokuwa na mtazamo wa mbele, naiomba sana Serikali iwahurumie vijana, iwaandalie mazingira mazuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, naamini Serikali itakuwa imenisikia na kwa kuwa Serikali yetu ni sikivu na inawapenda vijana na mkakati wa Rais ulikuwa ni kuwawezesha vijana kujiajiri na pia kupata ajira. Kwa hiyo niwaombe watendaji wa Serikali wanapotekeleza mpango huu watekeleze mpango huu kwa mkakati mzuri tuweke mipango madhubuti ambayo vijana wakimaliza elimu zao wapate ajira ama wajiajiri kwa msaada wa Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nizungumzie suala la bidhaa kupanda na hili nalo ni kero kweli, bidhaa zimepanda bila utaratibu na wakati mwingine wananchi wanakuwa hawana hata habari kwanini bidhaa hizi zinapanda. Kwa mfano, sukari imepanda bei, tena bei zenyewe utashangaa, nimeuliza bei ya sukari Morogoro nikaambiwa kilo moja shilingi 2,000, hapo Morogoro ambako sukari inatengenezwa pale. Nimekwenda Singida kilo moja shilingi 1,800, hebu niambie kwa nini bei hizi zisidhibitiwe? Kwa nini bei hizi zipishane pishane mkoa na mkoa?

Mheshimiwa Naibu Spika, nina hakika Serikali ikifuatilia au watendaji, wakifuatilia mambo haya kwa karibu, huu utaratibu wa wafanyabiashara kupandisha pandisha bei bila utaratibu utakoma, kwa sababu wananchi wanapata shida, pesa yenyewe wanaipata kwa tabu. Naomba sana na ikiwezekana kwa kuwa sasa hivi ni mambo ya kisasa, tuna televisheni na redio angalau unapitisha tangazo humo bei ya sukari inapanda kwa sababu moja, mbili, tatu, hata mwananchi anakuwa na matumaini kwamba aah, kumbe imepanda kwa sababu hii. Anaona kumbe hili ni jambo ambalo halina ubishi. Lakini vitu vinapanda kinyemelea, wananchi hawana maelezo na sisi wawakilishi wao maelezo hatuna, basi inakuwa ni tatizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nizungumzie njaa. Njaa ni kila mahali Singida kuna njaa, Iramba kuna njaa, Manyoni kuna njaa na Singida Vijijini, tukichukua tathmini polepole, naomba sana viongozi wetu huko Mkoani, kwenye Halmashauri zetu wapewe jukumu la kuandaa tathmini ya haraka kwa sababu hili ni janga, janga ambalo halihitaji lelemama.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MHE. VITA R. KAWAWA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nitumie fursa hii kukushukuru kwa kunipa nafasi ili nipate kuchangia hotuba ya Mheshimiwa Rais aliyoitoa Novemba 18, 2010 wakati akizindua Bunge letu.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, naomba niwashukuru wananchi wa Wilaya ya Namtumbo na wanachama wa Chama cha Mapinduzi, Wilaya ya Namtumbo kwa kunichagua tena kuendelea kuwawakilisha katika Bunge lako Tukufu. Nawashukuru sana na napenda niwaambie na kuwahakikishia kwamba sitawaangusha nitawatumikia kwa moyo wangu wote.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, naomba niwapongeze Baraza zima la Mawaziri na uongozi wa chini ya Waziri Mkuu, Mawaziri wote na Manaibu Mawaziri walioteuliwa na Mheshimiwa Rais kuunda Serikali katika kipindi hiki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba sasa nijielekeze katika hotuba ya Rais. Mheshimiwa Rais katika hotuba yake alitueleza Serikali atakayoiunda itakuwa na vipaumbele kumi na tatu, lakini alikwenda zaidi kwa umuhimu wa kilimo na mifugo, alitoa vipaumbele saba katika sekta hiyo. Hivyo, ushauri wangu kwa Serikali mpya kwa maana ya Baraza la Kazi la Mawaziri lazima tuwe na mikakati ya kusimamia vizuri mipango ya utekelezaji ya vipaumbele hivyo. Sababu nilivyoona, kuna mambo yanayohitaji matokeo ya haraka na muda wa kati na muda mrefu, kwa sababu tutambue watu nao wanahitaji matokeo ya haraka yatakayowezesha kumudu kupunguza makali ya maisha yao kiuchumi na kijamii.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika hotuba yake Mheshimiwa Rais ameeleza mambo mazuri tuliyofanya miaka mitano iliyopita na ametupa matumaini kwamba tutafanya vizuri zaidi katika miaka mitano hii. Dhamira yake ni kudumisha na kuyapatia ufanisi zaidi mambo ambayo tuliyatekeleza miaka mitano iliyopita katika miaka mitano

hii ijayo. Sasa hii ni changamoto kwetu sisi Wabunge na Serikali kwa maana ya *front banchers,* tunaomba *front banchers* msituangushe, mkasimamie kwa dhati kabisa utekelezaji wa dhamira ya Mheshimiwa Rais. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi ni mwakilishi wa wakulima, Rais alinikuna sana alipozungumzia matunda ya juhudi zetu yaliyoanza kuonekana katika kilimo cha mazao ya chakula na mazao ya biashara. Kwetu katika Mkoa wa Ruvuma, matokeo hayo tumeyaona leo, Serikali kwa msimu uliopita imenunua tani za mahindi ya chakula zaidi ya 43,000. Hayo ni mafanikio makubwa sana kwetu sisi mkoa wa Ruvuma. Ninachoweza kutoa ushauri wangu tuendeleze vitengo vya uzalishaji mbegu katika maeneo yetu ili tupate mbegu zinazoendana na hali halisi au hali ya hewa ya eneo la Mkoa wetu wa Ruvuma hususan katika Wilaya yetu ya Namtumbo.

Mheshimiwa Naibu Spika, sisi pale Namtumbo, kuna kituo cha utafiti wa mbegu cha Uyole, katika kijiji cha Suluti, lakini kituo kile kina majengo na kina mashamba yake, leo kimekufa kabisa ukikiona utadhani kwamba kituo kile mwenye chake amekufa na hakuna wa kumrithi. Naiomba Serikali iwekeze katika kituo kile ili kiweze kuzalisha mbegu kwa ajili ya hali ya hewa ya mazingira ya Mkoa wa Ruvuma. Leo tunauziwa na Mawakala wa Mbegu, mbegu za miezi mitatu katumani, sisi mvua zetu za miezi sita zinaanza mwezi wa kumi na moja mpaka mwezi wa tano, tunapoteza mahindi mengi sana tunapopewa mbegu za miezi mitatu, mahindi yanaoza shambani. Kwa hiyo, tunaomba sana Serikali iwekeze kwenye mbegu ili tupate mbegu zinazoendana na hali ya hewa ya Mkoa wetu wa Ruvuma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mazao ya biashara pia ambayo Rais amesema tumepata mafanikio katika zao ninalolifahamu mimi la tumbaku. Naomba ku-*declare interest* kwa mujibu wa Kanuni ya 61, mimi ni Mwenyekiti wa Bodi ya Tumbaku Tanzania. Kwa hiyo, napenda kwa kuwa zao hili nalifahamu la biashara, tumeweza kupata mafanikio makubwa kwa manufaa ya Serikali, ya wananchi na Halmashauri zetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa Serikali tu peke yake mapato yake ya *foreign exchange* kwa maana ya mapato ya fedha za nje, tumeweza kuongoza kwa mara ya pili mfululizo kuwa wa kwanza katika mazao makuu tumeuza tumbaku ya dola za Marekani 127.3. Zao la pili lililotufuatia ni pamba iliyouza dola milioni 111. Lakini pato la Serikali linalotokana na tumbaku, mwaka jana lilikuwa bilioni 98 kodi ambayo Serikali ilikusanya lakini pia Halmashauri zetu zilikusanya bilioni 13. Kwa hiyo, zao hili la biashara ni chanzo muhimu sana cha mapato yetu ya Serikali na kama kwa mapato haya ya tumbaku kama tunashindwa kabisa, kabisa, kabisa na kesi yetu ya *DOWANS* kwa mapato haya bilioni 98 tumbaku inaweza ikalipa na chenji ikabaki.

Hivyo naomba kusisitiza katika sekta hii ya kilimo tunahitaji kusimamia vizuri vipaumbele saba vya kilimo na mifugo vilivyowekwa. Mheshimiwa Rais pia alizungumza katika ukurasa wa 24…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha*

*kwa muda wa mzungumzaji)*

**MHE. VITA R. KAWAWA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MHE. GODBLESS J. LEMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana. Nataka kuchangia hotuba ya Rais lakini nitajikita kwenye eneo moja la amani, kwa sasa nitajaribu sana kuwa *constructive*.

Mheshimiwa Naibu Spika, mjadala wa jana Bungeni hapa jioni ulinifanya nirudi nilipofikia, nikaanza kutafuta nini maana ya neno amani, niliutumia muda mwingi sana nikaanza kupekua vitu vingi kwenye mitandao kujua nini maana ya amani. Ukiangalia kwenye hotuba ya Mheshimiwa Rais ame-*insist* sana mshikamano wa Taifa hili, usawa pamoja na amani. Lakini kwa bahati mbaya sana tafsiri ya neno amani nimekuja kugundua kwamba watu wengi hawaifahamu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimejiuliza Taifa ambalo asilimia 42 mpaka 50 ya watu ambao hawana uwezo ama hawafanyi kazi linawezaje likawa ni Taifa lenye amani, watu hawawezi kununua chakula milo mitatu, watu hawawezi kugharamikia matibabu, watu wanakwenda hospitalini akinamama wawili wanalala kitanda kimoja, Taifa ambalo asubuhi tumesikia mpango kutoka kwa Naibu Waziri wa Afya kwamba kuna bajaji zinatakiwa kupelekwa kwenye *dispensary* kwa ajili ya kuchukua akinamama wajawazito watakapopata matatizo, naanza ku-*question* nini maana ya amani.

Mheshimiwa Naibu Spika, msingi wa amani mahali popote duniani ni pale watu wanapokuwa na utamaduni wa kuheshimu ukweli na kuheshimu haki. Lakini vitu hivyo, vinapokosekana na ukaona kuna watu wako kimya, nina *refer* kwenye *speech* ya Martin Luther alipokuwa anatafuta uhuru wa mtu mweusi Marekani aliposema *peace is not the absence of war.* Lakini kwa nchi yetu hatuna migogoro mingi ya kusikia milio ya risasi, ndiyo sababu tunafikiri tuna amani, lakini kwenye *briefing* ya Bunge hili siku chache zilizopita zaidi ya Waheshimiwa Wabunge 30 ama 20 walisimama wakilalamika matatizo ya njaa katika Majimbo yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa najiuliza hiyo amani na mshikamano kwenye Taifa ambalo watu bado hawajaweza kula kwa miaka karibu 50 ya uhuru wa Mtanzania, kwenye Taifa ambalo unakwenda Mahakamani kuna sheria lakini hakuna haki, mfungwa ama mahabusu amekaa miaka mitano jela, hajawahi kuhukumiwa, kwenye Taifa ambalo mshahara kima cha chini haumwezeshi mfanyakazi kuishi maisha ya wiki nzima kama akiamua kuishi sawa sawa na ule mshahara, unajiuliza msingi wa hiyo amani uko wapi kama sio utulivu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba ama nashauri kwa namna yoyote ile hakuna namna ukweli unaweza ukakimbiwa na tukiona tunajaribu kukimbia kuu-*face* ukweli maana yake ni kwamba tunatengeneza bomu baya sana katika Taifa letu.

Mheshimiwa Naibu Spika, migogoro inayoonekana sasa hivi ndani ya nchi hii kwenye vyuo vikuu, kwenye kuandamana na kuna mchangiaji aliyepita hapa amesema hata wanafunzi wanaoandamana hiyo posho inatosha. Mimi niulize swali moja tu, shilingi 5000 kwa siku ya kula, kwa mwezi shilingi 150,000 inatoshaje? Unajiuliza kwamba tutafika wapi kama tutaendelea hivi?
Naomba tujikite katika misingi ya kuheshimu haki lakini kama tutaendelea kupuuza mambo ya msingi, haki itaendelea kuchezewa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukiangalia hata katika hotuba ya Mheshimiwa Rais pia amegundua suala la udini. Ni kweli katika nchi hii zimeanza kujitokeza dalili za udini na hata tukiwa Dar es Salaam kwenye *briefing* Mkurugenzi wa Usalama wa Taifa, alisema kuna viashiria vya upotevu wa amani, alitaja vitu kama hivyo pia vipo. Kwa hiyo, nashauri kwa ajili ya mshikamano wa Taifa hili, tuzingatie suala zima la haki na vilevile kwa ajili ya mshikamano na amani ya nchi hii ifike mahali sasa tujenge utamaduni wa kuanza kuheshimu haki kwa sababu haki ndiyo falsafa na ndilo tunda ambalo linaweza lika-*protect* amani na *future* ya nchi hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na hilo napenda pia kuchangia katika mambo ya maendeleo. Nilikuwa natazama rasilimali ilizonazo nchi yetu kwamba ni Taifa karibu la tatu ama tano Duniani kwa kuwa na dhahabu nyingi, ni Taifa la kwanza Duniani kwa kuwa na madini ya Tanzanite, ni Taifa lenye Mito na Bahari na Maziwa mengi lakini Taifa letu ni kati ya Mataifa hamsini bora duniani, tunazidiwa hata na Mataifa madogo yasiyokuwa na rasilimali.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukiangalia vipaumbele 13 vya Mheshimiwa Rais, kwanza nimejiuliza inawezekanaje ukawa na vipaumbele 13 halafu ukatarajia kuvimaliza ndani ya miaka mitano? Kwa sababu vipaumbele *is a sensitive things* ambavyo unatakiwa kuvifanya kwa gharama yoyote ile na unajua kwamba vitafanikiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu ya muda, sina *comments* sana juu ya Hotuba ya Rais lakini kama tunataka mshikamano na amani ya nchi hii, tujikite sana katika kupenda haki kwa sababu hilo ndiyo tunda ambalo linaweza likaendelea ku-*sustain peace* iliyopo. Nakushukuru sana. *(Makofi)*

**MHE. AHMED JUMA NGWALI**: Mheshimiwa Naibu Spika, nachukua fursa hii, kumshukuru Mwenyezi Mungu aliyetuwezesha kuwepo hapa salama. Vilevile nikushukuru wewe kwa kunipa nafasi hii ya kuweza kuchangia. Pia nimshukuru Mheshimiwa Rais kwa hotuba yake nzuri na iliyofanyiwa utafiti wa kutosha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya shukrani hizi, naomba niende kwenye kipaumbele cha kwanza. Pamoja na mambo mengine, Rais amezungumzia juu ya kuimarisha na kudumisha Muungano. Kwa bahati mbaya kabisa, Mheshimiwa Rais hakufafanua taratibu gani na njia gani ambazo atatumia katika kuimarisha na kudumisha Muungano.

Mheshimiwa Naibu Spika, imezoeleka kwamba njia kuu inayotumika katika kudumisha na kuimarisha Muungano, ni kuundwa kwa Kamati za kushughulikia kero za Muungano. Njia hii imekuwa ni njia kuu kabisa lakini tukiangalia kwenye ushahidi tunaona kwamba toka kuasisiwa kwa Muungano huu, karibu Kamati 45 zimeshaundwa kushughulikia kero mbalimbali za Muungano, 20 kati ya hizo zimeundwa miaka ishirini iliyopita.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nizitaje Kamati hizo:-

Kamati ya Baraza la Mapinduzi; Kamati ya Amini ya mwaka 1992; Kamati ya Kupambana na Kero za Muungano; Kamati ya Shamhuna ya mwaka 1997; Kamati ya Rais ya Kuchambua Ripoti ya Jaji Kisanga; Kamati ya Salum Juma Othman ambaye sasa ni Marehemu, Mwenyezi Mungu amlaze pahali pema peponi; Kamati ya kuandaa Mapendekezo ya Serikali ya Zanzibar juu ya Kero za Muungano; Kamati ya Ramia ya mwaka 2000; Kamati ya Baraza la Mapinduzi ya Sera ya Mambo ya Nje; Kamati ya Rais ya Wataalam Juu ya Kero za Muungano ya mwaka 2001; Kamati ya Baraza la Mapinduzi Juu ya Jumuiya ya Afrika Mashariki; Kamati ya Mafuta, Kamati ya Madeni baina ya SMZ na SMT; Kamati ya *Exclusive Economic Zone (EEZ);* Kamati ya Masuala ya Fedha na Benki Kuu na Kamati ya Rais ya Masuala ya Simu ya mwaka 1996-1999.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile kama haitoshi, Serikali ya Jamhuri ya Muungano iliunda Kamati nane kushughulikia kero za Muungano. Kamati ya Mtei; Kamati ya Tume ya Nyalali; Kamati ya Shelukindo Na. 1; Kamati ya Shelukindo Na. 2, Kushughulikia na Kuandaa Muafaka juu ya Mambo ya Muungano; Kamati ya *Harmonization*, Kamati ya Masuala ya Simu; Kamati ya Kisili na mwisho Kamati ya aliyekuwa Makamu wa Rais ambaye sasa ni Rais wa Zanzibar, Mheshimiwa Ali Mohamed Shein.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati zote hizi si kwa kutatua zile kero za Muungano lakini hata kutoa ripoti ambazo wananchi watajua wamefanya nini, wamefikia wapi, panahitajika nini, wapi pameshindwa, ripoti zake hazikupatikana na badala yake zilitoa maamuzi yake kwa siri bila ya wananchi kuelewa.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunapozungumzia kuimarisha na kudumisha Muungano, tunazungumzia kero za Muungano. Kwa hivyo, nadhani tutafute njia mbadala na ya uwazi ya kuweza kuzishughulikia kero za Muungano. Mheshimiwa Waziri Mkuu alileta Taarifa ya Serikali jana kuhusu mchakato wa Katiba, basi nafikiri mapendekezo haya tuuachie huo mchakato wa Katiba.

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili niseme kwamba wako baadhi ya watu, wakati mwingine Wabunge na wengine Viongozi wa Vyama vya Siasa, wamekuwa na tabia ya kukebehi mafanikio ambayo yamefikiwa Zanzibar. Dhana hii inaondoa ile dhamira ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kudumisha na kuimarisha Muungano. Tunaomba maneno haya ya kebehi yasiendelee. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, napenda kuchukua fursa ya kipekee, kumshukuru Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Jakaya Kikwete kwa uungwana aliouonesha katika ufunguzi wa Bunge la Tisa ambapo aliahidi kushughulikia na kutatua matatizo ya Zanzibar na amefanya hivyo. Muungwana ni vitendo, namwombea dua Mwenyezi Mungu amjalie umri mrefu.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MHE. MARTHA M. MLATA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa nafasi hii. Kabla ya yote, nimshukuru sana Mwenyezi Mungu kwa mapenzi yake makubwa kwa kunijalia na kuwapa moyo wananchi na wanawake wa Mkoa wa Singida, kwa kuweza kunichagua tena ili niweze kurejea katika Bunge hili na kuwawakilisha, nashukuru sana kwa hilo, Mungu awabariki sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda niungane na wale wote ambao wameipongeza hotuba ya Mheshimiwa Rais wakati analifungua Bunge. Kwa kweli, mambo yote aliyoyasema Mheshimiwa Rais na yale ambayo amekusudia Serikali yake iyafanye, ninaamini kabisa mambo mengi yatatekelezwa kwa sababu Baraza lake la Mawaziri alilolipanga, ni chapakazi, hivyo kila  kitu kitakwenda barabara, nampongeza sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia nisingekuwa mbali na Mheshimiwa Rais katika kuzungumzia suala la amani. Kuna watu wengi, kila mtu kwa tofauti yake, amekuwa akitafsiri kivyake kuhusu amani lakini mimi binafsi naomba niseme kwamba amani tunayoizungumza na amani ambayo Mheshimiwa Rais alikuwa anaizungumzia na amani ambayo tumekuwa nayo Watanzania mpaka sasa hivi, ni amani iliyo na utulivu na uhuru na mtu anaweza akafanya jambo lolote kwa wakati wowote ilimradi aweze kujipatia kipato katika maisha yake, si amani ile tunayosema kwamba kwa sababu mtu ana kipato kidogo basi amani hakuna, hapana, amani tunayoitaka sisi Watanzania ni utulivu, kuheshimiana na kuwa na staha lakini na kuwa na uzalendo wa nchi yetu. Usimchokoze mtu aliyetulia kwa kuitafuta amani. Muendee mtu kwa staha kwa kuitafuta na kuilinda amani. Kwa hiyo, nataka kuwaomba Watanzania wote, shetani ambaye ameanza kuinyemelea Tanzania yetu, anaonekana ameshaanza kuning’iniza kucha  zake kutaka kunyakua amani tuliyonayo, naomba kila mtu  kwa dini yake amkemee shetani huyu ili ashindwe katika jina la Mungu wetu. (Makofi)

**MBUNGE FULANI**: Shetani ashindwe kabisa.

**MHE. MARTHA M. MLATA:** Mheshimiwa Naibu Spika,  kingine nachotaka kuzungumzIa ni kuhusu Afya ya mama ambayo Mheshimiwa Rais aliizungumzia hasa ya uzazi. Kwanza, naomba kila mtu atafakari na aangalie tulikotoka na hapa tulipo. Serikali yetu, kwa miaka mitano ambayo  nimeingia ndani ya Bunge, imefanya kazi kubwa sana hasa vijijini. Wakati naomba Ubunge mwaka 2005, kuna maeneo ambayo sikuweza kwenda hata kwa baiskeli ilibidi nitembee lakini sasa hivi unapita kwa gari na pikipiki. Sasa mafanikio hayo tusiyabeze na sasa tunazungumzia mchakato mzima, ni namna gani tutakavyoweza kupunguza vifo vya akina mama. Kina mama zetu walikuwa wanabebwa

kwenye machela, wengine kwenye matenga, wengine kwenye vitanda lakini Serikali yetu imeona kwamba kwa sababu barabara zetu zinapitika na huwezi ukapeleka *Ambulance* kila Kata, basi hata hizo pikipiki ambazo na Mataifa mengine yanatumia zitumike. Sasa kwa nini tusishukuru hilo? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba sana Watanzania wote tulipokee hilo kwa sababu kila Kata, kila Zahanati au Kituo cha Afya kikiwa na pikipiki ambayo inaweza ikamfikisha mama mjamzito aliyeshindwa kujifungua na anahitaji msaada wa haraka, pikipiki ile itamfikisha kuliko kubebwa kwenye machela. Tukubali kwamba huwezi ukaanza kila kitu ukawa na mambo makubwa, utaanza kwa kidogo lakini baadaye utapanda, tuwe na shukrani mbele za Mungu. Hivyo, naiomba Wizara ipige mbiu, ifanye haraka ilete hizo pikipiki sisi wengine tunazihitaji ili kuokoa maisha ya akina mama, wasiozitaka waache lakini wananchi na akina mama wanazihitaji kuokoa maisha yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu suala la Kilimo Kwanza, sitaki kuzungumza mengi, naomba masharti ya kukopesha pembejeo, zile *power tillers*, trekta, hebu yapunguzwe ili watu wengine, wakulima wetu wengi waweze kukopa kwa sababu masharti yale ni makubwa mno. Huwezi ukasema mimi niwe na ekari 50, akina mama wakiungana hata kama mtu ana ekari tano, tatu au ngapi hazifikii masharti husika. Kwa hiyo, naomba masharti yapunguzwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka kuuliza ni kwa nini Bodi ya Mikopo inataka kutuchonganisha na wanafunzi? Naomba Bodi ya Mikopo ichunguzwe na ikiwezekana ivunjwe. Utaratibu wa kufikisha pesa kwa wananafunzi wetu ni mbovu, Serikali yetu inakuwa imetoa pesa lakini hazifiki kwa wakati. Naomba ichunguzwe na ikiwezekana ivunjwe na utaratibu ubadilishwe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka kumpongeza Mheshimiwa Rais kwa juhudi alizozifanya kuhusu kukuza Sanaa ya Muziki. Nataka kusema, ile *Mastering Machine* aliyoitoa, Wizara inawaeleza nini Wasanii wa Tanzania? Kwa sababu ilikokwenda imekwenda mahali ambapo Msanii hawezi kufaidika nayo au Wizara mnapanga nini kuendeleza yale ambayo Rais wetu ametoa? Kwa sababu ile mashine imekwenda mahali ambapo ukimtoa Msanii Singida kule Isanzu hawezi kufaidika nayo. Sasa Wizara naomba nijue Watanzania Wasanii wanafaidikaje na ile *Mastering Machine* aliyoitoa Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania?

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba pia nizungumzie suala la wanafunzi waliofanya mitihani ya Kidato cha Nne. Tusifu mafanikio yale kwa sababu wale waliofaulu na hata wale waliofeli, huwezi ukamlinganisha na aliyemaliza Darsa la Saba, lazima tuwe na pa kuanzia. Kwenye shule moja ya Kata unakuta wamefaulu watoto 20, ni sawa tunasikitika kwamba 70 wamefeli lakini wale 20 waliofaulu kama tungekuwa hatuna zile shule za Kata wangekuwa wapi? Kwa hiyo, ni mafanikio makubwa naomba sana kwa sababu pale ndipo tunapoanzia na kujua changamoto zetu kwamba Walimu ni wachache ili tujue tufanye nini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Mungu awabariki Watanzania kwa kuiombea amani nchi yetu, amina. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA**: Ahsante sana Mheshimiwa Martha Mlata na wale Wabunge wasiotaka Bajaji kwenye Majimbo yao, wajiandikishe kwa Naibu Spika. *(Kicheko)*

**MHE. JENISTA J. MHAGAMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nianze kwa kushukuru sana kwa kunipa nafasi ili na mimi niweze kuchangia hotuba hii ya Mheshimiwa Rais wakati akizindua Bunge letu kwa kipindi kile cha mwezi Novemba mwaka jana.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa, naomba nikipongeza Chama cha Mapinduzi kwa kushika tena madaraka ya kuiongoza nchi hii ya Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tulipoingia kwenye uchaguzi mwaka jana na hasa sisi wawakilishi wa Chama cha Mapinduzi tukiongozwa na Jemadari wetu, Mheshimiwa Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete, hatukuwa tukibahatisha, tulikuwa na maana kamili ya nini tunataka kufanya. Tulijua nini tumefanya kwa kipindi cha miaka mitano chini ya Serikali ya Chama cha Mapinduzi na hivyo tulikuwa tunaelewa tunapowaambia Watanzania tunahitaji kushika tena madaraka ya nchi hii, kukamata Serikali ya nchi hii, tunataka kwenda wapi. Kwa hiyo, kwa kweli naomba niseme nakipongeza Chama changu lakini na Rais wetu kwa ushindi mkubwa kwa kuwa yale tuliyoyakusudia yametekelezeka.

Mheshimiwa Naibu Spika, wale ndugu zetu majirani kutoka nchi ya Malawi, wana methali isemayo na huwa napenda sana kuisema, “kuanguka kwa jani ni aibu ya mti” na sisi kama Chama cha Mapinduzi kama kweli tungekuwa hatujafanya kitu, tungeanguka kama majani juu ya miti na ingekuwa ni aibu kwa Watanzania kwa sababu Chama hiki kimefanya kazi ya kutosha na hiyo sio siri.

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze kwa kusema kabisa kwa dhati moja ya moyo wangu, nikiwashukuru sana wananchi wa Jimbo la Peramiho, kwa kunichagua kwa kura nyingi sana tena za kishindo kikubwa, kwa kukiamini Chama changu na kunituma nije kushirikiana na Serikali yangu na kuunga mkono hotuba ya Mheshimiwa Rais kwa sababu imeeleza na kuelekeza yale ambayo ni kipaumbele kwa wananchi wa Tanzania wakiwemo wananchi wangu wa Jimbo la Peramiho. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Rais ametuambia hapa ana vipaumbele vyake 13, ameteua tayari Baraza la Mawaziri watakaofanya kazi kama Maamiri Jeshi wake wa kusimamia kazi hizo za kisekta. Sina shaka kwa sababu ukiangalia vile vipaumbele vilivyoainishwa na Mheshimiwa Rais kwenye hotuba yake, tunapata mwelekeo wa nini tutakakokuwa na wapi tunakokwenda.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwenzangu Mheshimiwa Martha Mlata Mbunge wa Viti Maalum Mkoa wa Singida, amezungumza sana suala la amani. Nilitaka kulisema hilo lakini naomba niliache lakini ni kitu cha muhimu na cha msingi kabisa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nijielekeze moja kwa moja kwenye hoja. Mheshimiwa Rais ameeleza kabisa katika mambo mengine ya kushughulikia ni kuhakikisha nchi yetu inakuza uchumi wa ndani na inahakikisha kwamba tunapunguza umaskini kwa Watanzania, nani asiyetaka kupunguza umaskini sasa aseme? Hakuna jambo kama hilo. Nadhani kitu cha msingi na kikubwa cha kuzungumzia, ni kujipanga na kuweka msisitizo, umaskini huu tufanye nini, tuupunguze namna gani na hasa umaskini wa kipato kwa wananchi wetu wakiwemo wananchi wangu wa Jimbo la Peramiho. Uchumi wetu tuukuze namna gani ili tuendeleze heshima ya nchi yetu ya Tanzania ndani ya nchi yetu lakini na nje ya nchi yetu ya Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mfano, Mheshimiwa Rais ameonyesha mwelekeo, kilimo chetu sasa hivi tunatakiwa kukibadilisha na sisi wote tunakubali tukiondoe kutoka katika kilimo kile cha umaskini kabisa cha jembe la mkono tukiingize kwenye matrekta na majembe ya kukokotwa na wanyama, nani hataki hilo? Bila ya kufanya hivyo, hatuwezi kabisa kuwakomboa wananchi wetu na hasa wakulima wetu vijijini. Tukitoka kwenye kuondoa kilimo hicho na tukakitengeneza kuwa kilimo bora, kazi yetu kubwa na Mheshimiwa Rais ameieleza ni kuhakikisha tunapata masoko ya mazao yetu na masoko hayo ya mazao yetu ya ndani na ya nje. Tuuze nje, tuongeze fedha za kigeni ndani ya nchi yetu na hivyo azma yetu ya kupambana na umaskini na kukuza uchumi wa nchi yetu utapatikana. Nashangaa watu wanaobeza juhudi za Chama cha Mapinduzi na wanaobeza mikakati hii imara ya kukuza uchumi wa nchi yetu. Hakuna lelemama katika suala hili la kuendeleza maisha bora kwa Watanzania wote. Tunaona kabisa bajeti yetu tunavyohangaika kuitafutia pesa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Rais wetu amesema azma nyingine kubwa ya nchi yetu ni kuongeza mapato ya ndani, nani asiyejua kwamba bila ya kujitegemea sisi wenyewe ndani ya nchi hatutaweza kuendelea? Ndiyo maana tunaunga mkono hoja hii, ni lazima tuhakikishe tunakusanya kadri tunavyoweza, mapato ya ndani ya nchi yetu na mapato ya ndani kuhakikisha tunajitegemea zaidi. Nyumba ya baba asiyejitegemea ni aibu. Ukiwa baba ombaomba hata familia yako hawaheshimiki mtaani. Kwa hiyo, mkakati wa kuongeza mapato ni agenda muhimu sana na Mheshimiwa Rais ameisema kwenye hotuba yake. Sasa anayekataa anataka tuwe ombaomba, anataka tukaombe mitaani? Cha msingi ni kuangalia haya mapato ya ndani, tunakusanya nguvu namna gani kuongeza mapato yetu. Tupunguze mianya ya rushwa, tupunguze masuala yote yanayotufanya tusikusanye mapato ya kutosha ndani ya nchi yetu ili azma yetu ya kujitegemea kwa kutumia fursa tulizonazo ndani pasipo kutegemea nje ziweze kuongezeka.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Rais wetu amezungumzia namna tutakavyoweza kujikomboa kijiografia ili kuhakikisha kwamba uwepo wetu katika Tanzania uhusianishwe na jiografia ya nchi tunazopakana nazo, kugeuza uchumi kwa jiografia tuliyonayo. Tunazungumza kabisa kujikomboa kutokana na reli, tunazungumza

kabisa kupanua bandari zetu, tunazungumza kila siku kutengeneza viwanja vyetu vya ndege na yote yako kwenye hotuba ya Mheshimiwa Rais wetu, nani hawataki hayo? Hii yote ni mwelekeo wa kuhakikisha tunapiga hatua.

Mheshimiwa Naibu Spika, bila kupoteza muda, nadhani kengele ya kwanza…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MBUNGE FULANI:** Kengele ya pili.

**MHE. JENISTA J. MHAGAMA:** Basi naomba niseme naunga mkono hoja hii na nampongeza sana Mheshimiwa Rais kwa hotuba yake. *(Makofi)*

**MHE. EZEKIA D. WENJE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana kwa kunipa nafasi ili na mimi pia niweze kuchangia katika hotuba ya Rais.

Mheshimiwa Naibu Spika, miaka sita iliyopita, nilikuwa mwanafunzi na nilipoangalia Bunge, nilisema na mimi nataka kuwa Mbunge lakini nilichosema nikija ambacho nikishasema hata nikifa leo sitakufa na deni. Pia naamini moyoni mwangu kwamba inafika wakati sisi wanadamu kila mtu anakuwa na *interest* yake na *interest* ya makundi pia lakini kuna wakati unafika nchi inakuwa kubwa kuliko mimi Wenje, nchi inakuwa kubwa kuliko Vyama tulivyonavyo vya kisiasa. Kwa hiyo, naamini kwa wakati huu tulionao kama Taifa, Taifa letu liko kwenye *crisis*, tuna matatizo mengi kama ya umeme, tuna migomo mingi, kuna njaa na kila aina ya matatizo. Wakati kama huu, ni wakati wa kuvua magwanda ya Vyama vya Siasa, tunaweka pembeni, tuitike kwa sauti moja kama Wabunge wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwamba nchi kwanza. Baada ya kusema hayo, sasa naomba niendelee na hata nikitoka hapa nikifa nitakufa bila deni. (*Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nimeangalia hotuba ya Mheshimiwa Rais, nikaangalia na vipaumbele vyake 13, naamini hata katika nchi zote zilizoendelea Duniani hapa wakati mmoja katika maisha yao ya utawala, waliwahi kuwa na Marais waliokuwa na roho ya ujasiri, waliothubutu kufanya vitu vikubwa, waliothubutu wakatengeneza *legacy* iliyotengeneza *difference* kati ya Rais aliyepita na Rais aliyekuja na atakayekuja. Ndio maana leo katika nchi ya Marekani Abrahm Lincoln anakumbukwa sana kwa sababu kipindi cha utawala wake kama Rais, ndege ya kwanza ya Marekani imeruka.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa ukiangalia leo hotuba ya Mheshimiwa Rais, nilitegemea kuona masuala yanayoonyesha uthubutu, ule ujasiri, *creativity*, kuona kitu kipya lakini hii stahili ya hotuba hata ukiangalia hivi vipaumbele 13 ni stahili ile ile, mambo yale yale, hakuna mabadiliko, hakuna *creativity* inayooneshwa humu ndani. Kwa nini nasema hivyo?

Mheshimiwa Naibu Spika, siku moja nakumbuka Mheshimiwa Rais alienda Kahama, alienda kuzindua Mradi wa Maji unaotoka Victoria unaokuja Shinyanga.

Alisema kwamba Mheshimiwa Ben Mkapa alikuwa ni Rais aliyekuwa na uwezo wa kuthubutu na aliyethubutu ku-*commit* fedha za Serikali kufanya maendeleo makubwa kama ile ya kutoa maji kule Ziwa Victoria kuja Mkoa wa Shinyanga na pesa nyingi zilizotumika ni fedha za ndani.

Mheshimiwa Naibu Spika, siku nyingine Mheshimiwa Rais alienda kuzindua daraja hilo ambalo ni la ushirika, nafikiri ni la Tanzania na Mozambique. Pale pia Mheshimiwa Rais Kikwete alisema kwamba anampongeza tena Mheshimiwa Ben Mkapa, Rais aliyeondoka alithubutu pia ku-*commit* fedha za Serikali kwenye lile daraja la ushirikiano kutengeneza kitu kikubwa kama kile.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilichotegemea kwenye hii hotuba nione, kwa mfano ukiangalia ukurasa wa 35, Rais alipokuwa anaongelea habari ya nishati, unaangalia pale kuna *statistics* fulani zimekuwa *indicated,* anasema, kwa mfano mwaka 2005 asilimia ya Watanzania waliokuwa wanapata umeme ilikuwa ni asilimia 10 lakini mpaka sasa imekua kwa asilimia 14. Anasema kwamba lengo lake ni kuikuza kwa asilimia 30 lakini sasa hii sio *realistic* tunataka kuona *timeframe* kwamba hii asilimia 30 itafikiwa lini?

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pia ukiangalia hii *trend* ya *growth,* utakuta kwamba hiyo asilimia 30 sasa kwa kuwa inakua kwa asilimia nne kwa kila miaka mitano itakuja kufikiwa basi mwaka 2030 kama tusipojiandaa leo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye hii hotuba, Mheshimiwa Rais anasema kwamba yeye alichukua madaraka pale ambapo nchi ilikuwa na migogoro na ukame na matatizo makubwa kwenye sekta ya umeme. Leo kuna dalili hapa inaonyesha kuna hii gesi asilia pia imetuongeza kwa kiasi kikubwa ambapo tunampongeza lakini tunachosema ni kwamba tunatakiwa sasa kwa sababu hii inatakiwa iwe ni kitu ambacho ni *long term may be* tufanye miaka 40 inayokuja sasa lazima tujiandae tutengeneze *reserve,* kama tutachimba mabwawa yakijaa, tunaweka ili hayo matatizo, ili hii *growth* ya asilimia nne baada ya miaka mitano hii, ni kidogo kweli itafikiwa sisi Wabunge tukishakufa sasa. Kwa hiyo, naiomba Serikali waangalie kitu kama hiki kipya, tufikirie kitu kikubwa, tuthubutu kufanya kitu kikubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, juzi Mheshimiwa Waziri wa Nishati na Madini alisema kwamba hiyo *project* ya kufanya *recycling* ya maji inawezekana lakini ni *too expensive.* Bora tu-*commit* fedha nyingi za Serikali kwenye *project* moja ambayo ni *expensive and sustainable* kuliko kufanya vitu vipande vipande ambavyo *in the long run* zinakuwa ni *very expensive* kuliko ku-*commit* fedha nyingi kwa wakati mmoja.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukiangalia ukurasa wa 36 ambapo Mheshimiwa Rais amezungumzia masuala ya rushwa, hapa naombe nisome kuna mstari hapa kidogo.

*"Rushwa kubwa zimeshughulikiwa na vigogo wamewajibishwa bila ya kuonewa muhali. Pamoja na hayo bado ipo haja ya kufanya zaidi kwani tatizo la rushwa bado ni kubwa".*

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nasema kwamba kama tunashughulikia rushwa kwa stahili hii na rushwa ndio msingi wa umaskini wa Watanzania, hatuwezi tukafika hatua ambayo ni *significant.* Sasa kama leo kuna watu bado wana kesi zipo Mahakamani, kesi zinazohusu rushwa, hawa watu leo bado wanapewa kazi za Serikali, tenda za ku-*supply* hata matrekta, sasa hapa tunachezeana au kweli tunapambana na rushwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nilichotegemea katika hotuba hii, nilitegemea kuona hali ya uthubutu katika hotuba ya Rais lakini nasikitika kwamba sijaona kitu chochote kikubwa…

**KUHUSU UTARATIBU**

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ukiangalia Kanuni ya 64(b), naongelea Mbunge hatotumia jina la Rais kwa dhihaka katika mjadala au kwa madhumuni ya kutaka kulishawishi Bunge kuamua jambo lolote kwa namna fulani.

Mheshimiwa Naibu Spika, mzungumzaji ambaye alikuwa akizungumza, ameongelea uthubutu kana kwamba katika Awamu iliyopita, hakuna jambo la uthubutu na jambo kubwa lililoonekana lakini uhalisia ni kwamba katika Awamu ya Nne, muhula wa kwanza kimejengwa Chuo Kikuu cha Dodoma kikubwa kuliko vyote, Chuo Kikuu kuliko vyote Tanzania, Afrika Mashariki na Kusini mwa Jangwa la Sahara na kimetumia gharama kubwa na uthubutu ulikuwa ni kukiondoa Chama cha Mapinduzi kwenye jengo lile na kuligeuza kuwa jengo la Utawala. Hiyo ni sehemu mojawapo.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile Mheshimiwa Wenje labda hana kumbukumbu, kutoka Dar es Salaam mpaka Mwanza sasa hivi anapitia kwenye lami, ile ilikuwepo? Hauwezi ukaenda kujenga daraja ambalo tayari ameshajenga Mheshimiwa Mkapa ndiyo maana Awamu ya Nne imeanza kujenga mengine ambayo yalikuwa hayajajengwa. Ahsante sana. (*Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Naomba niwakumbushe Waheshimiwa Wabunge Kanuni zetu katika kujadili hotuba hii na katika kufanya mambo mengine ndani ya Bunge. Kama ilivyoelezwa na mwenzetu aliyekaa chini, Kanuni ya 64 inasema:-

*"Bila ya kuathiri masharti ya Ibara ya 100 ya Katiba yanayolinda na kuhifadhi uhuru wa mawazo na majadiliano katika Bunge, Mbunge:-*

*(d) hatatumia jina la Rais kwa dhihaka katika mjadala au kwa madhumuni ya kutaka kulishawishi Bunge kuamua jambo lolote kwa namna fulani."*

Nia yangu kuwakumbusheni tu Wabunge wote mnaoshiriki katika mjadala huu na mengine baadaye kwamba ni Kanuni yetu tuzingatie. Mheshimiwa Wenje endelea.

**MHE. EZEKIA D. WENJE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niendelee kwa kusema kwamba napozungumzia suala la uthubutu nazungumzia *brain child* kwamba kama *project* inapofanyika tunaangalia *brain behind* hiyo *project*. Barabara inayotoka leo Dar es Salaam kwenda Mwanza ni *brain child* ya Serikali ya Awamu ya Tatu sio *brain* ya Serikali ya Awamu ya Nne. Kwa hiyo, hiyo *project* ilianzia huko. Naposema uthubutu, naongelea uthubutu kwa maana ya *brain* ya *creativity.*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niendelee. Kwa kuangalia huu mtiririko wa hobuta ya Rais katika sekta ya elimu, naomba kwa kuwa watoto wetu wengi wamefeli mtihani wa Kidato cha Nne mwaka huu labda sasa Serikali iimarishe Vyuo vya VETA, viwe vingi lakini pia viwe na uwezo mkubwa, tuvipanue ili kuweza ku-*accommodate* hawa watoto wengi ambao wamekosa nafasi ya kwenda Kidato cha Sita.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pia nimeona kuna suala tena Mheshimiwa Rais amegusia la kuongeza ukusanyaji wa mapato. Juzi nikiwa Mwanza kuna mtu mmoja alikuja aka-*present* kwenye Halmashauri yetu namna ya kutumia *electronics* kukusanya mapato. Mimi…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MHE. EZEKIEL D. WENJE:** Naomba uniongeze hata dakika sita kwa sababu muda wangu umechukuliwa sana, naomba niendelee.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Wenje, sasa ni nafasi ya Mheshimiwa Laizer.

**MHE. MICHAEL L. LAIZER:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili na mimi nichangie hotuba hii pamoja na kwamba nimeingia katikati ya watani zangu, aliyekaa na anayenifuata, lakini napenda kuipongeza sana hotuba hii ya Rais, nasema naunga mkono. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kukupongeza wewe kwa ushindi wako kuwa Naibu Spika, Spika pamoja na Mawaziri wote waliochaguliwa kwenye Baraza la Mawaziri la Awamu hii. Nachopenda tu kusema ni kwamba wananchi wanategemea sana Baraza hili kwa ajili ya maendeleo na sisi tunawategemea kwenye Majimbo, tutawafuata, kwa hiyo tunaomba tusaidiane ili wananchi wetu wapate maendeleo.

Mheshimiwa Naibu Spika, tukizungumzia maendeleo ambayo wengine hapa wanabeza maendeleo yaliyopatikana, nadhani katika Majimbo yetu mnajua kwamba Zahanati zimeongezeka, Vituo vya Afya vimeongezeka, barabara za lami na za vumbi zimejengwa, kwa hiyo ni maendeleo makubwa yaliyopatikana katika kipindi kilichopita. Umeme katika maeneo mengine ambayo hayakuwa na umeme yamepata na hata Longido sasa wana umeme. Jamani hata hili Jengo la Bunge ambalo tuko sasa, jamani haya si maendeleo yaliyopatikana? Tulitoka kwenye jengo la zamani, tumekuja kwenye jengo hili jipya na mnaona uzuri wake ulivyo, bado mnasema hakuna maendeleo?

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kusema kwamba tuongeze *speed* ya maendeleo tuliyokuwanayo, tuongeze zaidi. Najua kuna changamoto zilizopo sasa, hizo ndizo tupambane nazo. Kwa mfano suala la rushwa bado ni tatizo na linapunguza kasi ya maendeleo. Kwa sababu katika Halmashauri zetu, fedha zinazomegwa kwa rushwa bado ni nyingi, tuangalie kama hizo fedha badala ya kuingia kwenye mikondo mibaya ziingie kwenye miradi ya maendeleo.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine, nashukuru Waziri wa Maji yupo hapa, tuna tatizo kubwa sana kwenye miradi ya *World Bank*. Mradi wa *World Bank* ni mradi mkubwa sana. Ukiangalia vijiji kumi kwa kila Wilaya ni vijiji vingi sana, ni zaidi ya 1000 lakini mradi huo unasuasua, kuanzia 2000 mpaka kipindi hiki kuna vijiji ambavyo hata huo mradi haujaanza. Naomba sana huo mradi uangaliwe tena upya kwa sababu Halmashauri hawajui hata nini kinaendelea. Hawa watu hawako karibu sana na Halmashauri na mradi huo ni wa wananchi, naomba sana mradi huo uangaliwe upya na Serikali kwa sababu ni mradi ambao tulitegemea wananchi wengi watafaidika nao. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ambalo napenda kulizungumzia, ni suala la shule. Ni muda mrefu sana tunasema kwamba Serikali itajenga maabara. Kufeli kwa hawa watoto, maabara inachangia. Haiwezekani mtoto kuanzia *Form One* mpaka *Form Four* hajawahi kuingia maabara. Hii imekuwa ni changamoto ya muda mrefu na iingie kwenye Bajeti ya mwaka huu, maabara zote ziwe zimekamilika.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ambalo napenda kulizungumzia, hapa umesema kwamba wale ambao hawataki bajaji wajiorodheshe. Hatukatai kwa kweli lakini katika maeneo mengine bajaji haiwezi kupita. Hivi mama mzazi anayejifungua atakaa wapi na mkunga akae wapi? Katika maeneo mengine magumu kama Longido, jamani ni *ambulance* ndiyo inafaa ni kwa sababu hata magari mengine lazima yapande na *four wheels.* Kwa hiyo, tunaomba mchanganye bajaji na magari mengine yanayoweza kupita maeneo magumu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ni mifugo. Mimi ni mfugaji, suala la mifugo liko kwenye Ilani, liko kwenye Sera lakini yanabaki kwenye maandishi tu. Nashukuru sana Mheshimiwa Rais alizungumzia sana suala hili kwa urefu kidogo akasema kipindi hiki atalipa kipaumbele suala la mifugo, tunahitaji madawa, tunahitaji pembejeo, tunahitaji sana masoko na tunahitaji maji katika maeneo ya wafugaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, ndugu zangu mimi naunga mkono sana hotuba hii, ni hotuba nzuri na Awamu hii tumefanya kazi kubwa sana. Serikali ya Awamu ya Nne imefanya kazi kubwa sana na nategemea katika kipindi hiki itafanya kazi kubwa zaidi na wananchi mwaka 2015 wataichagua tena Serikali ya Chama cha Mapinduzi iongoze nchi hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MHE. TUNDU A.M. LISSU:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba na mimi kuchangia hoja ya kujadili Hotuba ya Mheshimiwa Rais wetu. Kabla sijafanya hivyo, naomba nikupongeze wewe kwa kuchaguliwa na Bunge hili kuwa Naibu Spika. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nimetumwa na wananchi wa Kijiji cha Matare ulikosomea, wameniambia niwasilishe pongezi zao kwako na nikueleze kwamba wanafarijika sana kwa hatua aliyofikia huyo mtoto wao. *(Makofi)*

Aidha, wananchi wa kijiji jirani na ulikosomea na kukulia, wameniambia vilevile nikueleze kwamba kijiji jirani na cha kwako kina Wabunge wawili katika Bunge hili unaloliongoza na kwa mara ya kwanza tangu Mungu ameumba mbingu na nchi, Wabunge hao wanatoka Chama kisichokuwa Chama cha Mapinduzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa naomba nirudi kwenye Hotuba ya Mheshimiwa Rais. Nikisema Spika, nafikiri nakutakia mema. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nijadili kipaumbele *number one* alichokisema Mheshimiwa Rais katika hotuba yake, nacho ni kudumisha Muungano wetu. Katika hotuba yake, Mheshimiwa Rais amesema kwamba umoja wa nchi yetu una sura tatu; yaani mipaka inayotambulisha Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Muungano wa Jamhuri ya Watu wa Zanzibar na Tanganyika ambao ulizaa nchi moja mpya ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na sura ya tatu kufuatana na Mheshimiwa Rais ni umoja wa wananchi wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika sura ya kwanza ya umoja wetu, Mheshimiwa Rais ametuhakikishia kwamba mipaka ya nchi yetu iko salama na wala hakuna tishio lolote la kutoka ndani au nje ya nchi yetu dhidi ya mipaka yetu. Kuhusu Muungano, Mheshimiwa Rais ametufariji kwamba Muungano wetu ni imara licha ya changamoto za hapa na pale ambazo Mheshimiwa Rais hajazitaja. Sasa naomba kwa heshima na taadhima nitofautiane na tathmini ya afya ya umoja wa nchi yetu aliyoitoa Mheshimiwa Rais.

Mheshimiwa Naibu Spika, naamini kwamba afya ya umoja wa nchi yetu si salama. Sio tu kwamba mipaka ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania haiko salama tena bali pia Muungano wetu upo katika hatari kubwa ya kuvunjika. Zaidi ya hayo, tishio kubwa dhidi ya usalama wa mipaka yetu na dhidi ya Muungano wetu sio maadui wa kusadikika wa nje ya nchi hii bali ni maadui ya Muungano waliomo ndani ya nchi hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naamini usalama wa mipaka ya nchi yetu na Muungano wa Tanzania umewekwa rehani katika kile kinachosheherekewa kama maridhiano ya kisiasa kati ya Chama cha Mapinduzi na Chama cha Wananchi CUF, naomba nielezee.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi naunga mkono muafaka wa CUF na CCM, isipokuwa kitu ambacho nakiona ni hatari kubwa kwa Muungano wa nchi hii, ni kile

kilichofuatia maridhiano haya ya kisiasa, nacho ni Sheria ya Mabadiliko ya Kumi ya Katiba ya Zanzibar yaliyoanza kutumika tarehe 13 Agosti mwaka jana.

Mheshimiwa Naibu Spika, Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ilizaliwa kwa Hati ya Muungano kati ya Jamhuri ya Tanganyika na Jamhuri ya Watu wa Zanzibar ya terehe 26 Aprili, 1964. *Articles of the Union* zilizosainiwa na Wakuu wa Nchi zetu mbili zilifuta nchi ya Jamhuri ya Watu wa Zanzibar na nchi ya Tanganyika zikaanzisha nchi moja inaitwa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Katiba yetu inaeleza wazi kwamba Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ni nchi moja. Sasa Mabadiliko ya Kumi ya Katiba ya Zanzibar, katika Ibara ya Tatu ya Katiba ya Zanzibar ya sasa, yamesema Zanzibar ni nchi ambayo eneo la mipaka yake ni eneo lote la Visiwa vya Unguja na Pemba pamoja na Visiwa vidogo vinavyoizunguka na Bahari yake ambayo kabla ya Muungano wa Tanganyika na Zanzibar ikiitwa Jamhuri ya Watu wa Zanzibar. Kwa hiyo, tuna nchi nyingine yenye mipaka inayotambulika na yenye *territorial waters*. Katiba ya Jamhuri ya Muungano inasema sisi ni nchi moja tu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sio hicho tu, Ibara ya Nne ya Sheria ya Mabadiliko ya Katiba ya Zanzibar, inasisitiza kwamba Zanzibar ni miongoni mwa nchi mbili zinazounda Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Sasa kuna Ibara ya 26(1) ya Katiba hii mpya ya Zanzibar inayozungumzia Rais wa Zanzibar. Rais wa Zanzibar maana yake ni Mkuu wa Nchi wa Zanzabar, *Head of State* na Ibara ya 2A inampa Rais, Mkuu huyo wa nchi ya Zanzibar amepewa mamlaka ya kugawa mipaka ya Wilaya na Mikoa ya Zanzibar bila kumshirikisha Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MHE. TUNDU A.M. LISSU:** Mheshimiwa Naibu Spika, namalizia kwa kusema hili ndilo tishio la Muungano. *(Makofi)*

**MHE. BENARDETHA K. MUSHASHU:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ili na mimi niweze kuchangia kwenye hoja hii iliyo mbele yetu. Awali ya yote, nipende kuwashukuru sana wanawake wa Mkoa wa Kagera, wa UWT, walionichagua na kuniwezesha kuwa Mbunge katika Bunge hili. Nawapongeze Watanzania wote waliokichagua Chama cha Mapinduzi na kikaendelea kuiongoza nchi yetu. Napenda pia nimpongeze Rais wetu, Dr. Jakaya Mrisho Kikwete kwa hotuba nzuri iliyosheheni mambo muhimu ambayo yanaonesha mustakabali wa nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nilikuwa nawasikiliza wachangiaji wenzangu, nikaanza kuwashangaa. Mtu anasema kwamba haelewi maana ya amani, kama mtu haelewi maana ya amani tunayozungumzia, tunayojivunia Tanzania, aende kule ambapo wanapigana, aangalie kule kulikotoweka amani. Mtu anaposimama hapa, haelewi vipaumbele vile 13, mimi nashangaa. Asichoelewa ni kukuza uchumi, ni kuwawezesha wananchi, ni kuboresha elimu au kuongeza usambazaji wa umeme au nini. Lakini nikakumbuka kwamba nilivyofundishwa shuleni ukitaka kuelewa vizuri lazima usikilize, uone na labda usome. Kama wote wangekuwepo, wakamsikiliza Mheshimiwa Rais, haya yote yasingetokea. Kwa hiyo, siku nyingine tukae tusikilize ndiyo tuweze kujadili vizuri

lakini unapojadili wakati hukusikiliza, ndiyo maana unafikia mahali unashindwa kuelewa vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ndugu zangu nataka kuwaambia kwamba Muungano wetu uko imara, hautetereki, tuko tayari sisi Watanzania kuulinda kwa nguvu zetu zote na tunasema kwamba maridhiano ya kisiasa yaliyopo Zanzibar kati ya CCM na *CUF* ni mazuri na yatadumisha Muungano. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kumpongeza Rais kwa dhamira yake ya kuongeza umeme. Tunakumbuka miaka ya 2000, nchi hii umeme ulikuwa unapatikana kwa wastani wa asilimia kumi, umeongezeka mpaka kufikia asilimia 12 na sasa hivi katika Hotuba hii Mheshimiwa Rais ameahidi kwamba utaongezeka mpaka asilimia 14. Wote tunajua kuwa umeme unachochea maendeleo, kwa hiyo, nampongeza sana Rais kwa kuweza kuliona hili na kwamba umeme utaongezeka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini naona kuna changamoto moja na nilikuwa naiasa Serikali kwamba wangeangalia gharama za kuvuta umeme. Kwa wale wanaotaka kuweka umeme katika maeneo yao. Unakuta labda unataka kuvuta umeme, ule umbali ni kama mita 50 kutoka kwenye nguzo ya umeme, Mtanzania anatakiwa kulipa milioni moja na ushehe, kama ni mita 100, unatakiwa kulipa kama milioni mbili. Sasa Watanzania wengi hawana fedha hizo, kwa hiyo, naomba Serikali iliangalie suala hili ili kusudi azma ya Rais ya kusambaza umeme kwa Watanzania walio wengi liweze kutimia.

Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza Rais wetu, kwenye Hotuba ameahidi kuongeza nafasi za wanawake katika ngazi za maamuzi na amekuwa akifanya kweli. Wote ni mashahidi, mmeona alivyowateua wanawake wengi wakawa Mabalozi, Makatibu Wakuu, Majaji, Wakuu wa Wilaya na kadhalika. Hata katika Bunge, mkumbuke kwenye miaka ya 1990 asilimia ya uwakilishi wa wanawake katika Bunge ilikuwa ni asilimia mbili lakini kufika kwenye miaka 2000 tulishafika asilimia 20 na sasa hivi tunajivunia kwa sababu ya utashi wa kisiasa wa Serikali ya Chama cha Mapinduzi na Rais wake, sasa tumefika sio chini ya asilimia 35. Kwa hiyo, tunaishukuru Serikali wameahidi kuongeza ushiriki huo tuweze kufikia 50 kwa 50. Tunaikumbusha Serikali kwamba nchi za *SADC* waliahidi kwamba ifikapo mwaka 2015 watakuwa wamefika 50 kwa 50 kwa hiyo tunategemea Serikali yetu kwa sababu ni sikivu wataweka mikakati ya makusudi kusudi hiyo 50 kwa 50 iweze kufikiwa sio kwenye Bunge tu lakini kwenye nyanja zote. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuzungumzia suala la elimu. Napenda kumpongeza Mheshimiwa Rais pamoja na Serikali ya Awamu ya Nne na Awamu ya Tatu na ya Pili, kwa jinsi walivyojitahidi kuboresha elimu. Nampongeza sana Mheshimiwa Kikwete, kwa jinsi alivyoweza kuboresha elimu ya sekondari mpaka sasa hivi tunajivunia tuna sekondari kila Kata. Kwenye miaka ya 1999/2000, tulikuwa na shule za sekondari kama 900, leo hii tunajivunia Watanzania tuna shule zaidi ya 4,000. Hayo si maendeleo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika nchi yoyote iliyoendelea, hawa watu wa ngazi ya kati *(Middle Cadre)* ndiyo wanaoendeleza nchi, hawa watakaomaliza kidato cha nne ndiyo watakuja kuiendeleza nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ndugu zangu niwaambie, kabla ya Shule za Kata katika Kata zetu, mimi Kata ninayotoka, kabla ya shule hizi za sekondari za Kata, walikuwa wanachaguliwa watoto wanne, watano; siku ya matokeo, ni kilio, wazazi wanalia, watoto wanalia kwa sababu ampeleke wapi mtoto aliyemaliza darasa la saba na hawezi kuendelea mbele. Mlikuwa huko majimboni mwezi Desemba wakati matokeo ya darasa la saba yametoka, kila mahali ni furaha. Watoto wamechaguliwa kuingia sekondari, kwenye Kata moja unakuta watoto mpaka 80, mpaka 100 wote wanaenda sekondari. Hayo ni mafanikio, lazima tuyatambue. Kila mafanikio yana changamoto tusiyabeze, tunasema hata Roma haikujengwa kwa siku moja. Kila mtu lazima awajibike, Serikali iendelee kuongeza walimu, vifaa vya kufundishia, maabara na vifaa vya sayansi, walimu wapewe motisha na wazazi waendelee kudhibiti nidhamu ya watoto wao vile vile na kusaidiana katika kuendeleza sekondari zetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilipenda nilizungumzie suala la mitihani. Tunasema shule za *private* zinafanya vizuri kuliko za Serikali. Shule za *private* kwa kila ngazi, kwa kila muhula mtoto anafanya mtihani akishindwa haendelei mbele. Kwa hiyo, labda Serikali tungeiangalia hii kama changamoto, mtoto anapomaliza kidato cha kwanza akashindwa, je, aendelee au akalili mpaka ajue ndiyo aendelee? Mimi nilikuwa nafikiri tukiliangalia hili, hata shule za Serikali zitaweza kufanya vizuri kama za *private*. Vile vile kuna ofisi za ukaguzi ambazo ziko kule majimboni, ziko kwenye Wilaya, ninaomba Serikali iziangalie ili kuziwezesha, ziweze kufanya kazi zinazotakiwa kufanywa kama nilivyokwishasema.

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka kuzungumza tena suala la amani; naona kuna dalili sasa za uchochezi, za kuwagawa Watanzania Kidini na kupoteza amani. Kampeni zimekwisha, watu wanataka maendeleo.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MHE. KABWE Z. ZITTO:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuchukua fursa hii, kwanza, kuwashukuru Wananchi wa Jimbo la Kigoma Kaskazini, kwa kunichagua tena kuwa Mbunge wao kwa kipindi cha pili. Kitu pekee ambacho napenda kuwaahidi ni kuwatumikia kwa uaminifu na uadilifu mkubwa na kuhakikisha kwamba, tunafanya mabadiliko. Wao wanafahamu kwamba, miaka mitano iliyopita tuliitumia kwa ajili ya kuimarisha miundombinu; tumejenga barabara na kufungua maeneo ambayo yalikuwa hayafikiki. Miaka mitano ijayo tutaielekeza kwenye kuhakikisha kwamba, vijiji vyetu vinapata nishati *(Rural Electrification)* ili na Watu wa Kigoma nao wajione ni sehemu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kukupongeza wewe binafsi, kwa kuchaguliwa kuwa Naibu Spika na napenda kuwapongeza Wabunge wote kwa umoja wetu bila kujali

vyama vyetu, kwa kuweza kufika hapa Bungeni na kuwa Wabunge wa Bunge hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nitajikita kwenye kipaumbele namba mbili katika Hotuba ya Rais; kipaumbele cha ukuzaji wa uchumi na nikipata muda, nitagusia kidogo kipaumbele namba tatu. Kwa kipindi cha miaka 10 iliyopita, uchumi wa Taifa letu umekuwa ukikua kwa wastani wa asilimia saba, lakini takwimu zinaonesha kwamba, katika kipindi hicho hicho, hali ya umaskini wa wananchi wetu imepungua kwa asilimia 2.5 tu. Wenzetu Uganda ambao uchumi wao umekuwa ukikua kwa asilimia sita katika kipindi cha miaka 10 iliyopita, wamepunguza umaskini kwa asilimia 25. Nchi za *South East Asia* kama Malaysia ambao miaka ya 1970 tulikuwa nao sawa, ambapo zaidi ya asilimia 56 ya watu wao walikuwa ni maskini, leo ni asilimia tatu tu ya wananchi wao ni maskini. Tanzania asilimia 37 ya wananchi ni maskini.

Mheshimiwa Naibu Spika, tuna tatizo kubwa sana la kutoweza kutatua *issue* ya *inequality* katika nchi yetu. Tumejikuta tunatengeneza mataifa mawili; taifa la matajiri na taifa la maskini na mgawanyiko huu umetanuka mpaka kwenye huduma. Leo kuna shule za maskini na shule za matajiri, *crisis* tunayoizungumza leo ya watoto wa kidato cha nne kufeli sana au wa darasa la saba kufeli sana, siyo watoto wa Wabunge, siyo watoto wa watu wenye uwezo, ni watoto wa maskini kabisa. Watoto wa watu wenye uwezo wako kwenye shule za *academies* na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye afya hali ni hiyo hiyo, wakati zamani ilikuwa huduma ya afya ya msingi ni ya kila raia kuipata, leo wenye uwezo wa fedha wana hospitali zao na maskini wana hospitali zao. Huduma za usafiri hivyo hivyo na kila kitu, kwa sababu tumeshindwa kuhakikisha ukuaji wa uchumi wa Taifa letu una-*address* hali nzima ya kutokuwa na usawa (*inequality)* na hilo hatulizungumzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tunapata *investment* nyingi sana, nimesikia kule Mchuchuma na Liganga wanakuja watu, *ten billion dollars investment* lakini haita-*penetrate* chini. Hatujawa na sera mahususi za kuhakikisha tunawainua watu wa chini na njia pekee na aliniambia Mahatri Mohamed juzi nilipokuwa Malaysia, hatujengi mikakati ya ku-*create jobs*. Vijana wengi sana hawana ajira na hii ni *time bomb, we don't address this*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Rais, katika kipaumbele chake cha tatu anazungumzia kujenga *middle class*. Sina *problem* na hiyo, mimi ni mjamaa, naamini katika ujamaa kwa hiyo, ningepaswa kutokuamini katika kuwa na *middle class*. Unajengaje *middle class* wakati bado hatujaweza ku-*address* tatizo la watu wa vijijini ambao ndiyo maskini zaidi! *Reason is very clear*, taarifa za Serikali zote, Waziri wa Fedha yuko hapa, taarifa zote za MKUKUTA, mipango yetu yote inaonesha kwamba ili tuweze kuwavuta watu maskini, tuwaondoe, tuwapandishe ni lazima Sekta ya Kilimo ikue kati ya asilimia sita na nane miaka mitatu mfululizo. *For the last five years* tumekua kwa asilimia tatu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mazingira ya uwekezaji yanazidi kuwa mabaya siku hadi siku na *we a very happy*. *Some of us* ni *creators* wa hayo mazingira, kwa sababu ni lazima tukiri na kama wawekezaji kwa maana ya *internal* na *external* hawaji kuwekeza, *where will people get jobs*? Kama *private sector* haipati mazingira mazuri ya kufungua viwanda, ya kufungua mashamba na kadhalika; *where will people get jobs and this is not addressed*? Tutapigana vijembe vya kisiasa tu, lakini tukumbuke hatima yake Watanzania watatuuliza mmekaa miaka mitano mmefanya nini? Lazima sote, *both sides of the Houses;* sisi Kambi ya Upinzani na watu wa Chama cha Mapinduzi, tukubaliane tuhakikishe kwamba ni wapi tunataka kulipeleka hili Taifa. Tuweke pembeni kabisa hizi tofauti zetu, *otherwise,* tutakwenda kupata matatizo makubwa sana. Nisingependa niishi katika umri wangu uliobakia nione nchi inasambaratika, ningependa nione Tanzania inakuwa imara zaidi na zaidi. *(Makofi)*

Mheshimikwa Naibu Spika, la pili la *energy*: Rais amezungumza kuongeza *access to electricity* mpaka asilimia 30. Sasa hivi Tanzania asilimia 14 tu, katika kila nyumba 100 Tanzania ni nyumba 14 tu zina umeme, *50 years after Independence*. Uzalishaji wetu wa umeme bado ni mdogo na Waziri wa Nishati na Madini kila siku anatutajia miradi humu Bungeni na nje kwenye *press conferences;* hatuambii ni Mradi gani utatekelezwa lini! Lazima tukubaliane kama Bunge, tuseme tuchague basi angalau Mradi mmoja, tunapofika tarehe 9 Desemba, tunasherehekea miaka 50 ya Uhuru, tunasema sasa angalau tumevuka 1000MW za umeme zinazozalishwa kwa uhakika. *Otherwise, we can't go anywhere*.

Sasa hivi nchi hii ina *deficit* ya umeme 2000MW, yaani umeme ambao unapaswa uwe umezalishwa hauzalishwi; haiwezekani na hatuwezi kuendelea. 1992 sisi na Malaysia wote tulikuwa tuna *power cut*; wenzetu leo wana *surplus 7000MW*, sisi tuna *deficit 200MW – 300MW*. Lazima tukae tukubaliane ni namna gani ambavyo tunataka kui-*transform* nchi hii, vinginevyo tutaishia kuwa nchi ya maneno, tutaishia kuwa nchi ya kurushiana vijembe na kuzungumza tu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, na mimi naamini kuwa, mimi na vijana wenzangu ambao tuko humu Bungeni, hatutakubali. Naomba vijana wenzangu wa pande zote mbili tukae, maana hii ndiyo nchi yetu. Sisi ndiyo tutakaoishi muda mrefu zaidi kama Mungu akipenda; akina Mzee Cheyo hawa sasa hivi tayari ni Alasiri, ndiyo ukweli huo. Tukae, tuone ni namna gani ambavyo tutavuka mbele zaidi. *Energy* na *growth* ni *very important*.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana. *(Makofi/Kicheko)*

**MHE. DEO H. FILIKUNJOMBE:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa, naomba nimshukuru Mwenyezi Mungu, kwa kutujalia sote afya njema ambayo kwayo leo sisi sote tuko hapa ndani tukiwa tunashiriki kwenye Bunge hili la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, naomba niwashukuru sana wananchi; kwanza kabisa, Wanachama wa Chama cha Mapinduzi Wilaya ya Rudewa, pamoja na wananchi wote wa Wilaya ya Rudewa, kwa kunipa ridhaa yao, kwa kunipa kura zao nyingi ambazo

mimi nazitafsiri kwamba wamenipa matumaini makubwa. Ninapenda kusema kwamba, nitawashika mkono sitawaangusha, nitawafikisha pale ambapo wao wana matarajio, pale ambapo wao wana matumaini.

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka niwahakikishie Wananchi wa Rudewa kwamba, nitashirikiana nao bega kwa bega. Nataka niwaombe wao kitu kimoja tu kwamba, muda wa kampeni sasa umekwisha, tushirikiane kwa pamoja, tuache tofauti zetu za vyama mbalimbali, tushikamane, tufanye kazi tulete maendeleo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka kuchangia kwenye suala la elimu. Inasikitisha kuona vijana wetu wamefeli kwa idadi hiyo kubwa. Mimi ningependa kuunga mkono wenzangu waliopita wakisema kwamba, wazazi wetu watakata tamaa pamoja na vijana hawa. Ninataka kutoa rai kwa Serikali kwamba, uundwe utaratibu maalum ambapo vijana hawa wataweza kurudia tena kusoma, wafanye mitihani upya kwa gharama ya Serikali ili waweze kufaulu, wasikate tamaa kule waliko.

Mheshimiwa Naibu Spika, changamoto nyingine ninayoiona hapa ni kwamba, tumefanya makosa kufuta mitihani ya kidato cha pili. Mimi napenda kutoa rai kwamba, mtihani wa kidato cha pili ubaki pale pale kwa sababu mwanafunzi anajipima, anasoma zaidi ili afaulu na hiyo ina mfanya pia asome na afaulu mpaka kidato cha nne. Mimi nilisoma seminari, tunafanya mtihani kila baada ya mwaka mmoja tunachujwa na ndiyo siri pekee ya shule za seminari kufaulu wanafunzi wake. Kwa hiyo, nataka kusema kwamba, ule mtihani wa kidato cha pili, Serikali iurudishe ili wanafunzi waweze kufanya vyema kwa sababu watakuwa wanasoma kwa jitihada zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye makazi bora; Serikali ifike mahali sasa itengeneze *standardization* ambapo Halmashauri pamoja na Mipango Miji waweze kushirikiana pamoja na Wizara husika, Wizara ya Ardhi, kuona kunakuwa na *harmonization* na *sensitization* katika ardhi pamoja na nyumba zetu ambazo tunajenga. Makazi ambayo yanajengwa sasa hivi hapa, kila mmoja anajenga kivyake kwa staili yake anavyotaka yeye, lakini ingewezekana kabisa tukasema Ilala wote tujenge nyumba ghorofa mbili au ghorofa moja na Manzese ziwe ghorofa saba na watu wafanye hivyo na eneo hili nyumba iwe ya aina hii. Kwa hiyo, Mipango Miji, Halmashauri pamoja na Wizara ya Ardhi, wakae pamoja kuhakikisha kwamba hili linafanikiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, wananchi wetu wa vijijini ni maskini sana, lakini wananchi hawa wakiwemo Wananchi wa Rudewa ambao ni asilimia 37 ya Watanzania wote, wana mtaji wa kutosha, tuna ardhi, lakini mpaka sasa tunavyozungumza ni asilimia 10 tu ya nchi nzima ya Tanzania imekuwa *surveyed* na imepimwa. Nataka kutoa changamoto kwa Serikali kwamba, ufike wakati sasa wananchi hawa tuwakomboe kwa sababu ardhi wanayo, kwa hiyo, ardhi ipimwe, tutekeleze Ilani yetu ya Chama cha Mapinduzi, tumeahidi kufanya hivyo ili kuweza kuwaongezea wananchi hawa ardhi hii iwe kama mtaji kwao kwa sababu ndiyo utajiri pekee ambao anautegemea leo Mtanzania na mtu ambaye anaishi kule Rudewa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa nafasi ya pekee, mimi niseme kwamba, hivi tunavyozungumza sasa hivi hapa tuna mgao wa umeme. Waziri wa Nishati na Madini anazungumzia gesi asilia, kununua mitambo, ukitizama sana tunaongelea *ad hoc strategy* na tunaongelea *long term strategy* za kuhakikisha kwamba tatizo hili linamalizika. Ukienda Rudewa tuna makaa ya mawe zaidi ya tani milioni 150 ambazo zinaweza kuzalisha umeme zaidi ya 1200MW kwa miaka zaidi ya 100 ijayo. Hivi sasa ninavyozungumza, kuna mwekezaji amepatikana, Sichuan kutoka China. Rai kwa Serikali kuhakikisha kwamba, mwekezaji huyu tunamtia moyo na ule mradi unaanza mapema.

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka nizungumzie jambo la amani na utulivu. Nataka kusema kwamba, wananchi wetu wametutuma, sisi ni wawakilishi wao humu ndani, kuna matarajio wanayotegemea kutoka kwetu mojawapo ikiwemo ustaarabu. Sasa unashangaa kuna baadhi ya rafiki zetu, kikao cha kwanza wametoka nje, kikao cha pili wametoka nje, halafu leo wanakaa chini kuchangia hotuba ambayo kwanza hawakuisikiliza, sijui wameipata wapi! Mtu ambaye hukutaka kumsikiliza, mtu ambaye wewe unasema humtambui, leo unachangia hoja kusema tunataka utusaidie hili, tunataka jambo hili liende huku; tuwe wastaarabu.

**KUHUSU UTARATIBU**

**MHE. TUNDU A. M. LISSU:** Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu utaratibu.

**NAIBU SPIKA:** Kuhusu utaratibu.

**MHE. TUNDU A. M. LISSU:** Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu utaratibu. Kanuni ya 64(1)(b): “Mbunge hatazungumzia jambo ambalo haliko kwenye mjadala.” Tunazungumzia Hotuba ya Mheshimiwa Rais, siyo waliotoka.

Mheshimiwa Naibu Spika, hatuko kwenye mjadala wa wale waliotoka!

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Deo Filikunjombe, yupo sawasawa kwa vile suala linalohusu mjadala wa Mheshimiwa Rais linahusiana na hotuba aliyoitoa siku hiyo na siku hiyo hiyo kuna waliotoka. Endelea. *(Makofi)*

**MHE. DEO H. FILIKUNJOMBE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nataka kusema kwamba, tabia hii tunayoionesha sasa, mimi nashukuru sana hivi viti having’oki na havitoki; naogopa sana tutarushiana viti siku moja humu ndani kwa *trend* hii tunayokwenda nayo; tutatoka mpaka lini?

Waheshimiwa Wabunge, nataka kuwaambia kwamba, Watanzania waliopo kule nje wametupa ridhaa, wametuheshimu sisi, hebu tuwe wastaarabu kwa sababu tukitoka kwenye ustaarabu ndipo tutapata amani na utulivu na tukomae kifikra na kimtizamo pia, tuwathibitishie wale Wananchi na Watanzania wote kwamba hawakukutuma Bungeni ili tuwe tunatoka nje kwenye kila kikao; ni jambo la aibu sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuunga mkono hoja ambayo inaendelea hivi sasa. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. DAVID Z. KAFULILA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Awali ya yote, nawashukuru Wananchi wa Jimbo la Kigoma Kusini, kwa namna ambavyo nilishikamana nao katika mchakato mzima wa kampeni. Nilifanya kampeni kwenye mazingira magumu nilikuwa kijana mdogo maskini lakini nikaweza kufanya kile ambacho kimetokea; nawashukuru sana. Zaidi, nawashukuru sana wananchi wote wa Mkoa wa Kigoma, kwa namna ambavyo wameweza kuitikia mabadiliko ndani ya Mkoa wao, sisi kama Wabunge wa Mkoa wa Kigoma tutajitahidi kwa kadiri iwezekanavyo, kufanya kazi na Serikali hii kuhakikisha kwamba yale ambayo waliyakusudia yanatimia kweli. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla sijaingia Bungeni nilikuwa nikiwaza sana kwamba, pengine eneo hili ni eneo ambalo watu wanaweza kukaa wakijadili masuala ya msingi kwa maisha ya watu, watu ambao wamekwisha kata tama. Kuna wakati inasikitisha, tumo ndani ya Taifa maskini, watu wanahangaika, wamekata tamaa, tunapewa nafasi ya kuja kuwawakilisha lakini badala yake tunafanya vijembe tunawakatisha tamaa zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nayazungumza haya kwa sababu ni *experience* yangu ya kwanza kuingia hapa Bungeni na sikutarajia kuona hali ambayo imejitokeza jana na hata leo. Ndoto yangu wakati nakuja Bungeni nilitegemea kwamba, kambi zingekuwa mbili tu hapa; tungekuwa na Serikali kama kambi moja na Wabunge kama kambi ya pili. Tungekuwa na kambi ya Wabunge ambao kazi yake ni kuibana na kuisugua Serikali bila kujali vyama vyetu; wawe Wabunge wa CCM, wawe wa CHADEMA, CUF, NCCR au TLP, sote tufanye kazi ya kuibana Serikali ili Waziri yeyote yule ambaye anapwaya ama yeye mwenyewe ajiondoe au tumwondoe sisi; ndicho kitu ambacho nilifikiria. Bahati mbaya sana kwamba, kwa namna moja ama nyingine, kambi zote eti kila mtu anapigania Chama chake; hasara kubwa sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimesoma Hotuba ya Rais, kuna mambo kadhaa ambayo kama Taifa tunahitaji kuyafanya. Hotuba hii haitofautiani sana na Hotuba ambayo aliitoa kwenye Bunge la Tisa na ndiyo maana ukisoma misingi ya Hotuba hii amesema ni mitatu; msingi wa kwanza ni Umoja wa Kitaifa, msingi wa pili ni uchumi kwa maana ya uhusiano kati ya uchumi mkubwa na uchumi mdogo na msingi wa tatu ni Utawala Bora. Misingi hii Rais amesema kwamba, ndiyo ambayo aliizungumza kwenye Bunge la Tisa na akasema anaona kuna umuhimu wa misingi hii iendelee kuwepo.

Mheshimiwa Naibu Spika, changamoto ndugu zangu ambayo tunayo siyo Hotuba, changamoto ambayo tunayo ni kwa namna gani tunaweza kusimamia maneno haya ambayo tunayazungumza yaweze kuingia kwenye utekelezaji. Tuna tatizo la namna gani tunaweza tukatafsiri uchumi mkubwa kwenda kwenye uchumi mdogo. Hili ni tatizo ambalo tangu Rais Mstaafu Mkapa anaondoka aliliacha na mpaka sasa linaendelea. Hawa watu ambao wanaona wanafika mahala wanaamua kuandamana, wanafanya fujo, wanafanya vurugu, mnaweza mkadhani ufumbuzi wake ni kuongeza idadi ya Polisi,

nilikuwa nazungumza na RPC mmoja anasema tuongeze idadi ya Polisi lakini msingi wa vurugu zote hizi ni watu kukata tamaa na watu wanakata tamaa kwa sababu kuna tofauti kubwa sana kati ya sisi na wao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati wa Mwalimu Nyerere, ingawa watu walikuwa wanapanga foleni kwenda kununua sukari wakiishi maisha magumu kabisa, lakini kwa sababu sura za Viongozi hazikuwa tofauti sana na wale wanaowatumikia, waliamini kwamba hii ndiyo hali yetu. Tatizo la sasa ni kwamba, sisi na wao waliotuchagua tuna tofauti kubwa mno. Mwalimu alisema uongozi ni utumwa lakini leo uongozi ni ubwana siyo utumwa. Sisi siyo watumwa, hamna mtumwa humu. Sioni Mbunge ambaye anafanya kazi kama mtumwa, ni lazima tukubaliane kwamba tuna tatizo la msingi tumeshindwa kulitafutia majibu na tusipoangalia ndiyo hili hili ambalo linaweza likasababisha machafuko na upotevu wa amani ya nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, mtu aliyekata tamaa ni mtu ambaye hata akiambiwa uongo atakwenda barabarani kwa sababu amekata tamaa, utabaki unasema tu huyu mchochezi kwa nini amekubali kuchochewa. Anakubali kuchochewa kwa sababu amekata tamaa na ni hatari sana tukifika mahali tukajenga taifa la watu ambao wamekata tamaa.

Mheshimiwa Naibu Spika, tuna mambo makubwa mawili, watalaamu wa uchumi wameshazungumza kwamba njia pekee ya kuondoka kwenye *equation* hii ya kutafsiri ukuaji wa uchumi kwenda kwenye maendeleo ya uchumi ni kujielekeza kwenye sekta ambazo zinabeba watu wengi. Wanasema kwamba, tunahitaji kuwekeza zaidi kwenye Sekta ya Kilimo, Sekta ya Biashara Ndogo Ndogo kama msingi wa kufanya ukuaji huu wa uchumi uweze kubeba watu wengi. Ukuaji huu wa uchumi wa asilimia saba siyo mdogo duniani ni mzuri lakini unabebwa na nani? Marekani ni nchi ambayo uchumi wake ni mkubwa kuliko nchi yoyote duniani lakini maendeleo yake ya kiuchumi yapo chini ukilinganisha na baadhi ya Nchi za *Scandinavia* kwa sababu inawezekana sehemu kubwa ya mapato yao wanaelekeza kwenye vita, wanapeleka Iraq, wanapeleka Afghanistan.

Kukuza uchumi ni jambo moja, lakini kufanya huo uchumi utafsiri maisha ya watu ni jambo lingine na kama sisi Wabunge tukiacha uchumi huu ambao unakua ukabaki ukitumika kwenye matumizi ambayo ni ya anasa, ukiacha uchumi huu ambao unakua ubaki unaendelea kutumika kwenye vitu ambavyo tungeweza kuvizuia; kwa mfano, ukiangalia mfumo mzima wa umeme Tanzania karibuni kila kampuni hizi za kukodi tunazilipa *capacity charges*, lakini kuna nchi ambazo hawalipi *capacity charges*, lakini sisi *IPTL* kila siku milioni mia tatu, hivi ndiyo vitu ambavyo wananchi wakisikia wanakasirika. Tulikuwa na *Dowans* kila siku tulikuwa tunalipa milioni 152 nchi zingine ambazo hazilipi wanafanyaje; kwa nini sisi tulipe? Kulikuwa na kitabu hapa wanaonesha ni kwa namna gani ambavyo matumizi ambayo ni *unnecessary* ambayo tungeweza kuyaelekeza kwenye maisha ya watu walau ingepunguza tofauti hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, tuna changamoto ya kuwezesha sekta ambazo zinabeba watu wengi; Sekta ya Kilimo, Sekta ya Biashara Ndogo Ndogo, ziweze

kutatua suala la ukuaji wa uchumi kwenda kwenye maendeleo ya uchumi na njia pekee ya kwanza kabisa ya kuwezesha Mapinduzi haya ya Sekta ya Kilimo na Biashara Ndogo Ndogo kuweza kuanza kukua lakini pia kuchangia sehemu kubwa ya uchumi; ni lazima tukubaliane kwamba tunahitaji Sekta ya Nishati iliyo imara.

Mheshimiwa Naibu Spika, Benki ya Dunia inasema kwamba, Sekta ya Umeme inachangia asilimia 40 ya Uchumi wa Dunia. Kwa hiyo, hauwezi ukaendelea kama hauna umeme wa uhakika, leo Tanzania nchi ambayo ina miaka takriban hamsini tangu tupate Uhuru, mpaka leo tuna chini ya megawati 1000 za umeme. Nchi ambazo zina fujo kila siku kama Zimbabwe wanakwenda megawati 2500; ni aibu. Unakwenda kutatua mgogoro wa kisiasa wakati kwako mgogoro wa umeme umekushinda! *(Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tunahitaji kuwekeza kwenye Miradi ya Umeme.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Kafulila. Mheshimiwa Mhandisi Stella Manyanya, atafuatiwa na Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed.

**MHE. ENG. STELLA M. MANYANYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ili nami nichangie Hotuba ya Rais. Kwanza, nampongeza yeye pamoja na ninyi Mheshimiwa Spika na Naibu Spika, Viongozi wa Bunge letu Tukufu, bila kuwasahau Mawaziri ambao wamepata nyadhifa mbalimbali. Naamini wote tunaanza kwa nguvu moja, lakini kwa kasi zaidi, ari zaidi na nguvu zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi leo nisingependa kuongea mengi sana kwa sababu wakati bado tunao, lakini kama ambavyo vijana wanajivunia nguvu yao katika kuendeleza Taifa hili na sisi watu wa makamo tunaona tuzielekeze busara zetu katika kupooza na kuhakikisha kunakuwa na ustawi wenye maadili katika Taifa letu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa bahati nzuri mimi ni Mwenyekiti wa Kamati ya Ushauri ya Makumbusho ya Taifa ya Maji, ambayo sherehe zake tunafanya kufikia tarehe 27 Mwezi wa Pili kila mwaka na mwaka huu nawakaribisheni Wabunge, karibuni Ruvuma mjionee maendeleo ya Mkoa wa Ruvuma. Mkoa wa Ruvuma ni miongozi mwa Mikoa ambayo imejizatiti kuhakikisha kwamba, Mkoa wetu wenyewe kwanza unajikomboa kuhakikisha hakuna njaa, lakini pia kuwasaidia wenzetu ambao wanapata mvua zisizoaminika.

Mheshimiwa Naibu Spika, niseme wazi maadili yetu yanaanzia na utamaduni wetu, nasikia mara nyingi tukichangia Wabunge tunasema hii ni jadi ya Uingereza, hii ni jadi ya wapi, lakini hivi kweli kuna raha ya kuiga kila kitu, kwa nini tusijivunie na sisi utamaduni wetu? Leo tunasikitika wanafunzi wana migomo kila siku, mimi nakubali kwamba migomo yawezekana kuna matatizo ya msingi, lakini ni lazima tugome katika njia hizo? Isitoshe, kinachosikitisha zaidi ni pale tunapoona hata sisi Wabunge tumeshindwa kutumia busara zetu katika lile tunashauri na kuonesha migomo.

Sisi humu ndani ni *role models,* kila anayeangalia Bunge anajua Bunge linajiheshimu vipi, Wabunge wanafanya nini, lakini mara ya mwisho ni lazima nikiri, hakuna asiyekubali kwamba CHADEMA, CUF au chama chochote ni wadau muhimu sana katika maendeleo lakini ni lazima nikiri na ninalaani kitendo kilichooneshwa siku ile mbele ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, anayeheshimika popote duniani kwa mambo aliyoyafanya. Kubwa zaidi, inanisikitisha kwa sababu nchi hii ndiyo kielelezo cha amani na ukombozi wa Afrika na pengine popote duniani. Watu siku za nyuma wamekuwa wakiiga kutoka kwetu Tanzania, wakisoma mifano kutoka Tanzania, leo sisi tunaamua kuacha yale mazuri waliyokuwa wakiiga wenzetu na kuanza sasa kujifunza utovu na vurugu kutoka nchi nyingine, suala hilo mimi sitaliunga mkono hata kidogo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa bahati nzuri, kwa sababu Wabunge Wapinzani nathamini sana mchango wao na ninafahamu wana uwezo mzuri sana kama Chama cha Mapinduzi, basi hili naona ni vema tukashirikiana kurudisha hali nzuri katika Bunge letu ili tuweze kushirikiana katika hoja za msingi na wananchi wanapenda kuona Bunge lenye hoja za msingi. Tusipofanya hivyo, tutajikuta tunaanzisha chuki kati yetu wenyewe. Nilipokuwa nakwenda kwenye Mikutano ya *SADC* nikiongozana na Mhehsimiwa Dkt. Slaa, watu walikuwa hawajui kwamba Msheshimiwa Dkt. Slaa anatoka Chama Pinzani na mimi ni Chama Tawala, walikuwa wanaona tunashirikiana, tungetamani hali hiyo iendelee. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nichangie suala la Elimu; kwanza, niseme kabisa na mimi sijaridhika na matokeo kwa sababu hayafanani na viwango vyetu vya ufaulu na kumuwezesha mtoto kuendelea na masomo yake. Kwa misingi hiyo, nasema kwamba, juhudi kubwa zifanyike na nikiwa kama mzazi, naiomba na kuitaka Serikali yangu kuhakikisha kwamba, bajeti ya safari hii na wadau wote wanaohusika katika kuboresha shule zetu, watenge pesa ya kutosha ili kuziwezesha shule hizo kufanya vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna hali ya watu ya kushindwa kujivunia yale ambayo wanakuwa wamefanya wakafanikiwa na hilo naomba niliongee leo na niongee na wazazi wenzangu popote Tanzania. Ninaomba tujivunie, tulikuwa na hatari kubwa sana kwamba, tulikuwa tunapiga hatua hasi kwenda kwenye wimbi la umaskini. Mtu kama hana Elimu ni chanzo cha umaskini, tulikuwa tunakwenda wote kwa pamoja, hali kadhalika mbali ya kusema tulikuwa tunakwenda kwenye umaskini vipi, ulikuwa unazaliana katika sura mbalimbali; mtu anapokuwa haendi shule huyo huyo ndiye anayeolewa hata kabla ya muda, huyo huyo ndiye anayemuoa mtoto mwenzake, huyo huyo ndiye anarudisha mzigo wa familia yake kwa wazee, huyo huyo ndiye anayeshindwa kumpeleka mtoto hospitali, kwa hiyo tunakuwa na matatizo mengi yanazaliana na bado tulikuwa tunaona sisi tupo salama; hatukuwa salama hata kidogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini tulikuwa kila wakati tunasema bora kutoa Elimu yenye ubora kwa kuangalia watu elfu hamsini, watu laki moja, bila kuangalia wale ambao wanakuwa wamekosekana wanakwenda wapi na hao sasa hivi ndiyo tunaowazungumzia. Kwenye *reseach* yoyote ile huwezi kupata tiba bila kujua tatizo. Tanzania tumejua tatizo, tulikuwa na watoto wengi ambao wamekuwa wakizaliwa bila

mpangilio, haifanani na idadi yetu ya ukuaji wa kiuchumi, kwa sababu kwenye kujifungua hata wazazi wenzangu wakinisikiliza watasema, hakuna unayejadiliana naye leo nitajifungua au sijifungui lakini kwenye uchumi tunasema mbona sijaletewa daftari, mbona sijapewa hiki, mbona sijafanyiwa hivi, wakati wa sisi kujifungua hatupangi na Serikali. Hilo naliomba hata wanaohusika na masuala ya upangaji wa uzazi hilo walione pia ni tatizo. Sasa tumefikia mahali tumegundua tatizo ni mwanzo wa tiba, tushirikiane; mzazi yeyote mdau wa elimu katika nafasi yake, wasiishie tu kulalamika shule hazina vifaa, hebu fikiria umezijenga shule elfu tatu kwa mara moja walimu huna, unategemea wangefaulu kwa mara moja haiwezekani!

Wenzetu wanasema kwamba hamkufanya vizuri lakini kwa upande mwingine wanatujengea hofu. Sawa sawa na mtu asiyejua kufurahia mafanikio yake, anasema unaona ulivyo, unaona imekuwa hivi, wewe Manyanya unajua wewe mfupi! Kwa hiyo, nikisema nafikiria siwezi kufanya lolote kumbe mimi ni mfupi lakini Mungu amenipa nguvu na sauti inaweza ikatumika na nikafanya kazi. *(Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa misingi hiyo, nasema Tanzania tupo kwenye njia sahihi, tulichofanya tumeisimamisha ile ya kwenda kwenye umaskini, sasa tuongeze nguvu tuhakikishe tunarudi kwenye maendeleo. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. HAMAD RASHID MOHAMED:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, nakushukuru kwa kunipa nafasi, kwa sababu ya dakika kumi, sitaendelea na shukrani nyingi.

Mheshimiwa Naibu Spika, jana nilibahatika kuwa na wageni wawili; mmoja anatoka Israel na mwingine anatoka Swaziland. Huyu wa Swaziland, *partner* wake ni *largest producer* wa maziwa duniani. Alipoingia hapa akasema tulipotoka huko tulikuwa na wasiwasi sana juu ya usalama wetu. Tumesafiri kutoka Dar es Salaam mpaka Dodoma, inaonekana tunaweza kufanya *investment* kwa sababu kunaonekana kuna ishara ya amani hapa. *(Makofi)*

Walisema jambo moja tu, *experience* yao kwa mara ya kwanza kuja Afrika, habari wanazozipata kwamba *bureaucracy* ina matatizo. Akamwambia Waziri Mkuu kama wangeweza kutatua hilo sisi tuko tayari ku-*invest* katika uzalishaji wa maziwa. Ombi langu la kwanza kwa Serikali, matatizo makubwa ya kiuchumi pamoja na *bureaucracy* bado hayajabadili *mindset. Investors* wengi wanakuja wanarudi kwa sababu bado *bureaucracy* haijataka kubadilika. Naomba Mawaziri mlisimamie suala la *bureaucracy. (Makofi*)

Ukienda Ghana leo unataka kuomba kitu unapewa *timesheet* unajulikana leo unatakiwa u-*produce* kitu gani, utakutana na nani na tarehe ngapi utapewa leseni yako. *It is there in writing*. Hakuna siku unakwenda ukakosa kufanyiwa jambo lako. Kwetu sisi *bureaucracy* ndiyo kila mkubwa wa nchi hii. Naiomba sana Serikali, kama tunataka kubadilika na kuona Watanzania wanabadilika kiuchumi, kwanza, tupambane na tatizo la *bureaucracy*. Serikali iseme kwamba mtumishi yeyote atakayekuwa katika ngazi yake

hakumpandisha daraja mfanyakazi awajibike. Mfanyakazi anakaa miaka kumi hapandishwi cheo na hakuna anayejali. Mfanyakazi anakopwa mshahara unaotoka kwenye *Consolidated Funds* lakini husikii Waziri kakopwa wala Mbunge kakopwa, wala hata Mkurugenzi kakopwa, lakini watu wa chini wanakopwa *why*? Hili lazima tulisimamie litatupunguzia migogoro.

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili, juzi tulikuwa na semina tukaambiwa kwamba, suala la rushwa linafanyiwa kazi. Mkurugenzi anasema ana kesi nyingi alizofanya lakini DPP anamkwamisha. Hebu sasa tuletewe takwimu hapa Bungeni; ni kesi ngapi za rushwa zinazoanzia milioni 20 na kuendelea Mkurugenzi amemaliza na amezipeleka kwa *DPP? DPP* ameshazifikisha mahakamani kesi ngapi? Tupate hizi taarifa badala ya watu hawa kutupiana mpira kumbe hatujui ukweli uko wapi. Hili nalo naliomba sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, la tatu, wataalam waliokuja jana walisema kwamba, hii TEKNOHAMA sijui kama nimeitamka sawa, suala hili la mitandao linaweza kuongeza *GDP* kwa asilimia 1.3 lakini lazima uingie kwenye teknolojia mpya. Sisi hatuja-*move* huko. Bei tulizonazo leo za simu wanasema zinaweza kuteremka kwa asilimia 50 lakini maamuzi hayatoki. Kwa hiyo, bado tunaendelea kung’ang’ania vitu ambavyo vinasababisha uchumi wetu uwe ghali bila sisi wenyewe kujielewa tunakwenda wapi. Naomba Serikali iangalie maeneo hayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Kenya wamewekeza hapa si chini ya viwanda au makampuni 200, Tanzania tuna makampuni saba Kenya. Namwomba Waziri anayehusika, alikuwa Spika wangu hapa, hebu angalia tuna tatizo gani Watanzania kushindwa ku-*invest* katika hizi nchi jirani wakati wenzetu wana-*invest* kwa wingi hapa Tanzania; ni sababu zipi za msingi? Naomba na hilo nalo lifanyiwe kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo kubwa ambalo linaajiri watu ni kilimo. Wachina wana hekta 1900,000 za umwagiliaji maji za mpunga, zinatoa wastani wa tani 12.5 kwa hekta, sisi tuna wastani wa hekta sita hivi sasa. Juzi Rais alipokwenda Advos alisema kuna hekta 350,000 wanatafuta wawekezaji wakubwa ili kuja kuzalisha chakula. Sisi tuna hekta 331,000 tunazozimwagilia maji, hii ni kwa mujibu wa Taarifa ya Kilimo, zinazalisha wastani wa tani sita. Ningeshauri badala ya ku-*invest* kwenye *new project*, hebu tuangalie hizi hekta 331,000 zilizopo hatuwezi tukazalisha mara mbili au angalau tukafikia tani tisa. Kwa hiyo, utakuwa umetumia muda mfupi kwa kuongeza mbegu nzuri kwa sababu *infrastructure* tayari ipo ili tupate hii *production* ya chakula ituondoe. Kwa sababu ndiyo sehemu kubwa ya mfumko wa bei ilipo, hili ni tatizo katika nchi yetu. Hiyo, itakuwa imetusaidia kutupungumzia mfumko wa bei. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tunazo taasisi nyingi za elimu hapa Tanzania, wenzetu wa India wameunda Bodi ya kufuatilia *private schools* juu ya gharama, lakini vile vile namna ambavyo raia anaweza kulipa, sisi tumeziachia tu kiholela. Hakuna *regulatory authority* inayosema hizi *private schools* au *colleges* nazo tuna mkakati gani. Zinajipangia wenyewe tu, matokeo yake ndiyo tunaziona hizi *crisis* zinazotokea na hatufaidiki sana kwa mtu wa kawaida katika zile *private schools.* Wenzetu wa India wameliona hili wakaweka *regulatory authority* ambayo inaangalia kwamba na mtu wa

kawaida aweze kusoma katika hiyo *private school* yako. Naomba sana Serikali iliangalie hili nalo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Rais alizungumzia suala zima la demokrasia. Kwanza, nalishukuru sana Bunge lako kwa kazi nzuri waliyofanya jana wamepanua demokrasia. Tunahitaji kuendelea kufanya kazi hiyo, wako watu walidhani tunahitaji vyeo, hatukuhitaji vyeo tulihitaji kuweka misingi mizuri. Nampongeza sana Mheshimiwa Mrema, Mheshimiwa John Cheyo na Mheshimiwa Kabwe Zitto, kwa kukamata zile Kamati za *Oversight* na nawapongeza Wenyeviti wote na Makamu Wenyeviti waliochaguliwa, tunategemea watafanya kazi nzuri ya Bunge letu. *(Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, wako watu wanadhani Muungano utaweza kuvunjika; Muungano huu hautavunjika kwa sababu ya Katiba. Bunge hili lilikaa siku moja likabadilisha Katiba likamwondoa Rais wa Zanzibar kutokuwa Makamu wa Rais wa Muungano, ambapo kwenye *Articles of Union* ilieleza kabisa kwamba, Rais wa Jamhuri ya Muungano akitoka Bara, Rais wa Zanzibar *automatically* anakuwa Makamu wa Rais; kikaondolewa kifungu hicho na kilikuwepo katika *Articles of Union;* Muungano haukuvunjika na hautavunjika maisha. *(Makofi)*

**MHE. ASSUMPTER N. MSHAMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninashukuru kwa kupewa nafasi hii. Kwanza kabisa, nasimama mbele yenu kumshukuru sana Mungu kwa kunipatia nafasi kuwemo katika Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Katika hilo, namtukuza Mungu kweli kweli.

Jambo lingine nasimama tena kushukuru sana Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa kusimamia kwa dhati kuhakikisha kwamba, wanawake tunapewa nguvu na tunaweza kugombea majimbo na hatimaye tukashinda; katika hilo Mungu ambariki sana. Pia napenda kuwashukuru Wananchi wa Nkenge, kwa kuniamini kwamba, naweza kuja hapa nikawakilisha mawazo yao na nawaahidi nitalifanya hilo na nitawatendea haki; naomba waniombee nisimame niweze kuwawakilisha. *(Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kumpongeza Rais kwa mambo matatu; kwanza kabisa, kwa kuhakikisha kwamba anatoa mwelekeo wa taifa letu na kwa namna ya pekee kwa suala la elimu ndiyo tuko hapa tunaongea kwa namna tofauti kila mtu ana mawazo. Mimi ningeomba kusema kwamba, kwa suala la elimu tumepiga hatua nzuri. Kwa nini nasema hivyo?  Hapo zamani katika kijiji chetu wakati mimi nashinda, tulishinda watoto wawili tu, lakini sasa hivi kuna watoto zaidi ya 35 wameweza kushinda na kwenda sekondari. Kwa hilo nampongeza sana. (*Makofi*)

Labda niongee namna gani tunaweza kuongeza nguvu na kuboresha, tazama hata gari linapoondoka huwa haliondoki na *gear* namba tano, unaanzia *gear* namba moja unakwenda mpaka namba tano. Kwa hiyo, nina uhakika kuanzia hapa tulipoanzia tunaweza kufanya vizuri. Labda nishauri tu, kwa mfano, kama kutafuta mshindi si lazima tutafute mshindi kwa kuangalia matokeo ya mwisho. Nchi zingine zinaangalia *progress* ya mtoto. Mtoto kuanzia vidudu alikuwa anapata nini, alipokwenda darasa la saba alifanya vipi, alipokwenda kidato cha kwanza alikwendaje, alipokwenda *form four*,

mtihani wa mwisho unaweza usiupime kama kigezo cha kushindwa kwa sababu inawezekana ali-*panic* au alikuwa anaumwa, mazingira hayakuruhusu kufanya vizuri; hivyo, nilikuwa nashauri tuangalie kwa tatizo hili lililotupata tunaweza kufanya nini kuliko hata kurudia hawa watoto tulikuwa nao tangu vidudu walikuwa wanafanya nini, tukaweza kuwaokoa kuliko kusema wameshindwa tuwarudishe nyuma na kadhalika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mchango mwingine katika elimu, nilikuwa ninajaribu kutafuta namna ya pekee ya kusaidia watoto wetu wa Chuo Kikuu. Mimi sielewi wazazi tunachangia vipi kwa misimamo ya watoto wetu wanapoanza migomo kwa sababu kila mtoto ana baba, ana mama na anao ndugu; ni namna gani wanachangia kuleta maendeleo au mabadiliko katika nchi yetu? Watu walio vyuo vikuu siyo watoto ni watu wazima, ni watu ambao tunategemea kuwatumia kwa kizazi kijacho; je, hawa watu tunawatumia namna gani na tunawashauri vipi?

Mimi nilikuwa najiuliza; wakati wa kampeni wazee walipokuwa wanaongelea sana habari za Serikali nikasema bahati mbaya Taifa letu hatuna *limit* ya Serikali itakusomeshea watu wangapi, kila mtu anaweza kuzaa tani yake kama watoto 20, 30, lakini wote tukasema Serikali iwasomeshe mpaka Chuo Kikuu, kitu ambacho hakiwezekani; nchi nyingine wanaweka *limit*. Hivyo, nilikuwa naomba tuangalie katika familia zingine watoto saba wote wamesomeshwa na Serikali, lakini hao hao ndiyo wanaogoma kule Chuo Kikuu; ni namna gani tunaangalia kutoa uwiano watoto wengine wasome na wengine wasome kwa familia zote? Tuseme labda kila familia watoto watatu, wawili wapate *offer* ya Serikali na wengine wazazi tujitahidi kuchangia kuwasomesha watoto wetu katika suala la elimu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine ambalo nilikuwa naliangalia kufuatana na wale wanao-*graduate* wanamaliza wamechukua mikopo; tuna utaratibu gani wa kujua kwamba ile mikopo watailipa au hawatailipa na tukiwapatia nafasi ya kwenda kufanya kazi vijijini wanakataa? Tunaweka mkakati gani wa kwamba anapokuwa amemaliza Chuo Kikuu kwa mkopo wetu tukimpeleka Biharamulo aende na tumpe miaka mitano kwanza kabla hajakwenda kokote anakotoka yeye atuchangie kwa ile kazi tuliyompatia. Mimi katika suala la elimu nilikuwa nachangia kwa namna hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, pale Nkenge tunao Mto Kagera lakini hatuufaidi kama Mungu alivyokusudia. Mungu kuuleta ule mto kule alikusudia Wanankenge wafaidi wapate samaki, walime kwa maji yale na wapate maji ya kunywa. Sasa hivi hatuwezi kwa sababu uwezo wa kuyatumia yale maji hatuna. Hivyo, nashauri Serikali iangalie namna gani inaweza kutusaidia ule Mto tuufaidi kama Mungu alivyokusudia. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ningependa kuchangia kuhusu umeme. Kule kwetu Nkenge, umeme umetoka Uganda umepitiliza mpaka Bukoba Mjini lakini umesahau mpaka wa Mtukula pale na ni aibu kubwa, ukiangalia Mtukula kwetu Tanzania ni kweusi usiku, Mtukula ya pili Uganda taa zinawaka. Mimi nilikuwa naomba Mheshimiwa Waziri anayehusika, atusaidie kuondoa hiyo aibu, huo umeme upatikane kama alivyoahidi ili Tanzania na Uganda zote zionekane ni Nchi za *East Africa*. Katika

habari za umeme mimi unisaidie sana maana ulikuwepo siku ile uliahidi kabisa. Nakuomba kwa kuwa na Rais alichangia pale utusaidie ule umeme upatikane mapema ili watu waone kweli kazi nimeifanya. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nimepata tatizo kidogo, nilipokuwa najiunga na hili Bunge nilikuwa najua ni mahali ambapo watu wote wana mshikamano. Jambo lililonisikitisha ni kuond mtu mkubwa wa nchi anaongea kwa namna ya kawaida tu, kwa nidhamu ya binadamu yeyote, unatoka nje na hakuna lolote linalotendeka na bado unarudia kufanya hivyo watu wanakuachia tu. Naomba utupe mwongozo; hivi Wabunge wa CHADEMA wakianza kuondoka, siku nyingine *CUF* wakaondoka, siku nyingine *TLP;* hili litakuwa ni Bunge la namna gani?

Mimi naomba tuweke msimamo, kama Mheshimiwa Rais yupo au Kiongozi yeyote; lazima tumheshimu kama kanuni inavyosema. Mimi naomba tuelezwe ni nini kitatokea kama mtu ataamua kuondoka mbele ya umati kama huu? Watu wengi wametuheshimu, tuko mahali hapa kwa ajili ya kujenga taifa, mtu anaamua kwa jeuri anatoka nje halafu anarudi na hakuna kitu kinafanyika! Hayo ndiyo masikitiko yangu, lakini naamini kwamba tutarekebisha na Mungu atatusaidia. (*Makofi*)

Niseme tu hayo machache kwa kuwa ni mgeni, naomba mbarikiwe. Mimi naitwa Mchungaji Assumpter, Mungu awabariki sana. *(Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mchungaji Assumpter. Wachungaji na Maaskofu humu ndani na Mashehe, Maustadhi basi mtusaidie kutuombea kidogo.

Waheshimiwa Wabunge, katika michango mbalimbali baadhi ya Wabunge wameongelea habari ya tabia ambayo ninahakika Watanzania wote wanaangalia Bunge letu kwa umakini na kufuatilia kwa umakini mkubwa. Kuna tatizo ambalo limejitokeza la baadhi ya wenzetu kutoka nje ya Bunge, kwa lugha ya kawaida kinyemela. Nataka kusema kwamba, Watanzania wanisikie vizuri, katika Kanuni zetu Bunge, hatuna kanuni yoyote inayomkataza Mbunge yeyote; peke yake au kikundi cha Wabunge, kutoka nje.

Kwa kuwa ninyi Watanzania mmemchagua kila mmoja wetu pamoja na mimi kuja kuwawakilisha ndani ya Bunge hili; ni jukumu lenu ninyi kumuuliza Mbunge huyo aliwaomba kuja kuwawakilisha hapa Bungeni halafu badala ya kuwawakilisha anatoka nje; hili atawajibu yeye huko huko. Atakaporudi mwaka 2015 kuomba kurudishwa tena Bungeni, swali muhimu ni kwamba unataka kurudi kwenda kufanya nini na kazi yako ilikuwa kutoka nje? Unaweza ukapiga makofi miaka mitano si mingi, lakini ni moja ya tabia ambazo nina hakika, kwa niaba ya Watanzania ni za kuudhi wala hazifurahishi hata kidogo. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, leo pamefanyika chaguzi za Wenyeviti na Makamu Wenyeviti wa Kamati zetu za Bunge. Orodha halisi itatajwa na Mheshimiwa Spika kesho asubuhi, bado inawekwa vizuri. Atataja hapa Kamati kwa Kamati kwa kila Mwenyekiti na Makamu Wenyeviti wa Kamati zote. Mimi nitumie fursa hii kuwapongeza wote waliochaguliwa. *(Makofi)*

Nina hakika baada ya uchaguzi huu wa leo, hata wale waliotoka jana wakiangalia na kupima wataona kwamba, hapakuwa na sababu wanasema *with a hindsight*, ukikaa baadaye na kupima utaona hata siku ya Rais tulitoka kwa nini, ukikaa baadaye na kupima utaona hivi hata jana tulitoka kwa nini. Naamini kabisa, kwa uzoefu utakaoendelea tutazidi kuelewa kwamba Bunge hili ni Bunge ambalo linatenda haki na hata mijadala kama mmeona Wabunge wote mnapewa haki mnajadili kwa uhuru kabisa ni Bunge la kujivunia na sote tulijenge kama Mheshimiwa Spika wetu Mama Makinda alivyosema, tujenge Bunge moja, Bunge imara kabisa la kuwaletea maendeleo Watanzania.

Mwisho kabisa, naomba niwatangazie Wabunge wote kutoka Zanzibar hususan wale wa *CUF* na CCM, muhudhurie kikao kifupi katika Ukumbi wa Msekwa mara baada ya mkutano.

**TAARIFA**

**MHE. KABWE Z. ZITTO:** Mheshimiwa Naibu Spika, kuna Wabunge kutoka Zanzibar wanatoka CHADEMA. Haya mambo ya kuanza kutofautisha ndiyo mambo ya jana, tuna Wabunge kutoka Zanzibar wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA); hawaruhusiwi kuhudhuria Mkutano huo? (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Hivi ni kikao gani hicho ambacho Mwenyekiti anapewa taarifa? Narudia tena, Wabunge wa kutoka Zanzibar wote wa *CUF* na CCM, watakuwa na kikao mara baada ya kutoka hapa.

Waheshimiwa Wabunge, nawashukuru sana kwa ushirikiano mlionipa. Nawashukuru sana kwa shughuli tulizozipanga leo katika *Order Paper* zimekwenda vizuri. Kesho tutaendelea kujadili Hotuba ya Mheshimiwa Rais, pamoja na shughuli nyingine zitakazopangwa. Naomba kusema ahsante sana, shughuli zetu kwa leo zinaishia hapa, kwa hiyo, naahirisha Shughuli za Bunge hadi kesho saa tatu kamili asubuhi. (*Makofi*)

*(Saa 1. 42 Bunge liliahirishwa hadi Siku ya Alhamisi,*
*Tarehe 10 Februari, 2011 Saa Tatu Asubuhi)*